USAWIRI WA MWANAMUME KATIKA NYISO ZA JANDO MIONGONI MWA ABAKURIA.

NA

RIRO MATINDE SAMWEL

Tasnifu Hii Imewasilishwa kwa Madhumuni ya Kutosheleza baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Idara ya Lugha na Isimu Chuo Kikuu cha Egerton

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY


EGERTON UNIVERSITY

AGOSTI, 2006.

UNGAMO NA IDHINI

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo chochote kile.



18/9/2006

Riro Matinde Samwel

(AM12/1136/04)

Tarehe

IDHINI YA MTAHINI

Tasnifu hii imetolewa ili kutahiniwa kwa ushauri wangu na idhini yangu kama msimamizi wa kazi hii wa chuo kikuu



18/9/06

Dkt. Onyango Ogolla

Tarehe

Idara ya lugha na Isimu.

Chuo Kikuu cha Egerton, Njoro-Kenya

HATILINZI

Hairuhusiwi kunakili sehemu yoyote ya tasnifu hii kwa njia ya kanda, maandishi au kuhifadhi kwa njia yoyote bila idhini kutoka kwa mwandishi au chuo kikuu cha Egerton.

SHUKRANI

Kazi ya utafiti na uandishi wa tasnifu ni mchango wa watu wengi. Aidha kazi hii huhitaji subira, stahamala na bidii ya hali ya juu. Hivyo basi, ni dhahiri shahiri kuwa kazi hii isingefikia ukingoni mwake kama si jitihada za watu mbalimbali ambao walitoa mchango usiokadirika katika kuifanikisha.

Kwanza ningependa kumshukuru Maulana kwa kunijalia ilhamu, siha na raghba ya kuishughulikia kazi hii tangu mwanzo wake hadi ukingoni. Pili, natoa shukrani zangu kwa msimamizi wangu, Dkt. Onyango Ogolla kwa ushauri wake wa kitaalamu. Usimamizi na umaizi wake ulinisaidia vilivyo. Licha ya shughuli zake za kikazi na za kibinafsi hakuchoka kuisoma na kuirekebisha kazi hii. Amenilea kimasomo na mwongozo wake wa faradhi ulikuwa dira ya kuniongoza tangu mwanzo wa kazi hii. Kwa kweli, ushauri wake ulinitia moyo kuhitimisha kazi hii kwa muda maalum.

Shukrani zangu pia ziwaendee walimu wangu: Dkt. Furaha Tchai, Dkt. Beja, Dkt, Aswani, Dkt. Kitetu, Bw. Mayaka Gwachi, Bw. Nabea Wendo, Bw. Marani, Bi. Liguyani na Bi. Sheila Wandera ambao walichangia kwa njia mbalimbali katika kuyapanua maarifa yangu katika lugha ya Kiswahili. Kweli mchango wenu katika masomo haya haukadiriki.

Sitawasahau mwalimu Mahiri Mwita na Kerata Chacha kwani pamoja na kunifunza mengi hawakusita kunipa ari ya kuendeleza masomo yangu. Kwa kweli, fadhili zenu zitakuwa sehemu ya kumbukumbu yangu.

Pongezi zangu za dhati nazitoa kwa mke wangu, Bi. Roseline Mwikali ambaye alinichochea sana katika masomo haya. Alinitia shime kila nilipoelekea kulemewa na kazi hii. Aidha, kauli zake na marekebisho ya kazi hii ni mchango usiosahaulika. Ama kweli subira na stahamala zake zilinizidishia nguvu kila kulipokucha. Nawashukuru vilevile wanafunzi wenzangu: Ojuang Mwiba, Kyeu Daudi, Makori David, Kevogo Ombima, Minyori Mureithi, Kirema Kanario na Adika Stanley ambao walikuwa na mengi ya manufaa hasa katika mijadala yetu ya kiusomi darasani na nje ya darasa. Utangamano nanyi ulikuwa mchango mkubwa katika kujenga na kukuza tajriba nzuri ya kuchanganua maswala ya kiakademia. Namshukuru pia Sibuti Mwita kwa kuniunga mkono na kunipa moyo kama ndugu wa karibu kila nilipoelekea kuchoka.

Msaada wa mwalimu mkuu, walimu na wanafunzi wa shule ya upili ya St. Joseph's Ntimaru wakati nilipokuwa nikisoma ulikuwa wa manufaa makubwa. Namshukuru pia ndugu yangu, Dkt. Concord Mwita. Mchango wake katika masomo yangu ya uzamili ni ithibati

kuwa damu ni nzito kuliko maji. Nawashukuru wazazi wangu, David Riro na Mogosi Eliada kwa kumzaa huyu "mwana" mkamlea na kumsomesha.

Mbali na watu wengi (wasaidizi na wasailiwa) ambao waliacha shughuli zao za kawaida kwa minajili ya kunisaidia katika ukusanyaji wa data. Kuna wale ambao ninanuia kuwashukuru binafsi kwa mchango wao muhimu: Mwita Kirutu, Mzee Marko Matiko, Mzee Moffat Masambe, Mzee Mtundi Wairoga, Julius Juma, Ananiah Moronya na Rebecca Gimunta msaada wenu katika kazi hii utaishi kukumbukwa.

Shughuli za Utafiti huhitaji mchango wa watu wengi, iwapo baadhi yao sikuwataja naomba waniwie radhi, kwani sijafanya hivyo kwa kuwapuuza bali ni kutokana na idadi yao kubwa ambayo isingemalizika.

Ingawa kuna watu wengi ambao walichangia katika kufanikisha kazi hii, ningependa ieleweke kwamba upungufu wowote utakaobainika katika tasnifu hii ni wangu binafsi.

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wapendwa wafuatao:

Kwa wazazi wangu: Riro N. David na Mogosi Eliada. Kazi hii ni hidaya kwenu kwa mengi mliojihini kwa ajili yangu.

Kwa mke wangu: Bi. Roselyn Mwikali na mtoto wetu Maclaurine Chacha. Kazi hii ni tunu kwa subira na stahamala zenu.

IKISIRI

Nyiso za jando hutoa mfano wa haja ya Abakuria ya kuisimulia jadi yao na wakati huohuo kuifungamanisha na leo yao. Katika kufanya hivyo, nyiso hizi zimepewa hadhi maalum kama vipaza-sauti mojawapo vya utamaduni wa jamii ya Abakuria. Wahusika katika muktadha huu wa tohara wanahusika katika kujenga nafsi ya Mkuria, kauli yake na husimulia matarajio ya utamaduni wake. Utafiti wetu ulizingatia nyiso ambazo hulenga na kughaniwa kwa tohara ya wavulana. Kwa vile maisha ya binadamu hujengwa katika taashira ambazo maana na ufasiri wake umewekwa katika muktadha maalum wa jamii husika. Utafiti huu ulinuia kukusanya baadhi ya nyiso ambazo huonyesha sura fulani ya mwanamume wa Abakuria. Kwa kufanya hivyo, tumefasiri na kubainisha sura halisi inayojitokeza mintarafu ya matarajio, mielekeo, mitazamo na utamaduni wa jamii ya Abakuria kumhusu mwanamume.

Nyiso za jando ni mojawapo ya tanzu za fasihi simulizi ya Abakuria. Aidha, ni kitengo muhimu cha utamaduni wa Abakuria kinachoratibu na kuonyesha majukumu mbalimbali yanayoandamana na jinsia ya kiume au ya kike. Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili; nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi na nadharia ya Uwezo-uume. Utafiti ulifanyiwa nyanjani, deta ya kimsingi ilikuwa nyiso za jando, deta nyingine ilipatikana kutoka kwa mahojiano ya ana kwa ana na wasaili tuliowateua mintarafu ya umri wao na tajriba yao kuhusu nyiso za jando,historia na utamaduni wa jamii ya Abakuria kwa jumla. Utafiti huu utachangia katika kubainisha sura ya mwanaume wa Abakuria. Kunakili baadhi ya nyiso hizo za jando, ni mchango mahususi wa kuhifadhi mojawapo ya utanzu wa fasihi ya Abakuria.

Tansifu hii imegawika katika sura sita. Sura ya kwanza imeshughulikia usuli wa mada, mada ya utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete za utafiti, umuhimu wa utafiti na upeo wa utafiti.

Sura ya pili inahusu udurusu wa maandishi yanayohusu jamii ya Abakuria inarejelea Historia, utamaduni na fasihi yao. Maandishi yanayohusu mada ya utafiti na msingi wa nadharia zilizoongoza utafit huu aidha, yamegusiwa. Sura ya tatu imejikita katika mbinu za utafiti na uchanganuzi wa data. Katika sura hii, mmeelezwa data ya kimsingi ya utafiti na jinsi data hii ilikusanywa na namna ilichanganuliwa ili kufanikisha malengo ya utafiti.

Sura ya nne imeshughulikia asili na historia ya Abakuria. Aidha imegusia utamaduni na matarajio ya jamii kwa kila awamu ya maisha ya mwanamume kutoka utotoni hadi kifo chake. Katika sura hii pia mmejadiliwa mifumo ya kijamii, kisiasa, kidini na ya kiuchumi ya Abakuria.Sura ya tano inahakiki nyiso za jando za Abakuria ili kudhihirisha taswira ya mwanamume na nafasi anayopewa katika jamii.

Sura ya sita ni hitimisho la tasnifu. Sura hii imezingatia muhtasari, matokeo na mapendekezo ya mtafiti. Kusudi kuu ni kuonyesha kuwa mada hii ni pana na inahitaji kushughulikiwa zaidi ili kupanua mapana na marefu yake.

ABSTRACT

Circumcision chants among the Abakuria narrates about the past and at the same time incorporates their today. By so doing they are given special status as one of the expressing agent of the Abakuria culture. Singers in this context of circumission are involved in portraying and narrating the expectations of the culture of the Abakuria. This research is aimed at capturing most of the circumcision chants sang by boys during circumcision. Since human life is built up on symbols whose meaning and interpretation is contextualised within the social milieu. The main focus will be, how Kurian man is perceived in circumcision chants. Consequently this work will attempt to interpret the symbolic meanings of captured chants with reference to the perception of a Kurian man in the society. Circumcision chants is one of the genre of oral literature of Abakuria. These chants play a greater role in the structuring of gender roles. The research will also attempt to show how circumcision chants play a greater role in the creating and maintaining masculinity among the Abakuria.

This research will be guided by two theories: Critical Discourse Analysis theory and Hegemonic maculinity. The research will be done in the field: the primary data will be the captured chants, which will be supplemented by field inteviews. This study is anticipated, if accomplished, to cover the perception of a man in the Abakuria society. The captured circumcision chants will be a major contribution in the preservation of one of the genre of oral literature of the Abakuria.

This thesis is divided into six chapters. Chapter one deals with the background of the study, statement of the problem, objectives of the study, hypothesis of the study, significance of the study and scope of the study.

Chapter two deals with liteature review on the Abakuria in relation to their history, culture and literature and the contribution of all these on Hegemonic masculinity and the perception of a man in the Kuria society. Also, in this chapter is the literature review on the topic of study together with theoretical framework.

Chapter three deals with research methods and the analysis of data. The chapter explains the primary data of the study, how it was collected and how it was analyzed.

Chapter four deals with the Kuria society. In details, the history and culture of the Abakuria. It gives an account of the culture and expectations of the community in every developmental stages of a man from birth to death. The main concern is to show how every stage contributes on hegemonic masclunity and general perception of a man in the Abakuria society. This chapter also discusses the social political, religious and economic systems of the Abakuria.Chapter five has analyzed the circumcision chants in order to show the images of a man and the position he is accorded by society.

Chapter six is the conclusion of the thesis. This chapter contains summary, findings and researcher's suggestions. The main concern here, is show that this topic is very vast and hence, it calls for more research in future.

YALIYOMO

UKURASA

UNGAMO NA IDHINI ..... **ii**

HATILINZI ..... **iii**

SHUKRANI ..... **iv**

TABARUKU ..... **vi**

IKISIRI ..... **vii**

ABSTRACT ..... **viii**

YALIYOMO ..... **ix**

MAELEZO YA DHANA ZA KIKURIA KATIKA LUGHA YA KISWAHILI ..... **xiii**

UFAFANUZI WA ISTILAHI ..... **xvi**

SURA YA KWANZA **1**

UTANGULIZI WA TASNIFU **1**

1.1 Usuli wa Mada 1

1.2 Mada ya Utafiti 3

1.3 Madhumuni ya Utafiti 3

1.4 Nadharia Tete 3

1.5 Umuhimu wa Utafiti 4

1.6 Upeo wa Utafiti 4

1.7 Hitimisho 5

SURA YA PILI **6**

2.1 Utangulizi 6

2.2 Yaliyoandikwa kuhusu Abakuria 6

2.2.1 Yaliyoandikwa kuhusu Utamaduni wa Abakuria 6

2.2.2 Yaliyoandikwa kuhusu Fasihi ya Abakuria 8

2.2.3 Yaliyoandikwa kuhusu Utawala na Historia ya Abakuria 10

2.3 Yaliyoandikwa kuhusu Mada ya Utafiti 11

2.4 Msingi wa Nadharia 16

2.4.1 Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi 16

2.4.2 Nadharia ya Uwezo-uume 20

SURA YA TATU **24**

MBINU ZA UTAFITI **24**

3.1 Utangulizi 24

3.2 Eneo/Mahali pa Utafiti 24

3.3 Ukusanyaji wa Data 24

3.3.1 Njia za Ukusanyaji wa Data 25

3.3.2 Matumizi ya Kanda/Kaseti na Kinasa-sauti 25

3.3.3 Mahojiano ya Ana kwa ana 25

3.3.4 Unchunguzi-shiriki 26

3.4 Uchanganuzi wa Data 26

3.5 Hitimisho 28

SURA YA NNE **29**

ASILI, HISTORIA NA UTAMADUNI WA ABAKURIA **29**

4.1 Utangulizi 29

4.2 Historia – Simulizi ya Uzao wa Abakuria kutoka kwa "Monto" 29

4.2.1 Uzao wa Abakuria 30

4.3 Historia – Simulizi ya Uhamaji na Utengano wa Abakuria 31

4.4 Jadi ya Abakuria 35

4.4.1 Awamu ya Kuzaliwa na Malezi 36

4.4.2 Sherehe za Kumpatia Mtoto Jina 38

4.4.3 Awamu ya Tohara: "Esaro" 40

4.4.4 Awamu ya Ndoa 43

4.4.5 Ada za Mazishi/Matanga 44

4.5 Mifumo ya Kijamii, Kisiasa, Kidini na Kiuchumi ya Abakuria 46

4.5.1 Hali ya Maisha na Muundo wa Jamii ya Abakuria 46

4.5.2 Siasa na Utawala 48

4.5.3 Maafikiano na Uamuzi katika Jamii 49

4.5.4 Dini na Imani Andamizi 50

4.5.5 Shughuli za Kiuchumi za Abakuria 51

4.5.5.1 Ufugaji wa Ng'ombe 52

4.5.5.2 Ukulima 54

4.5.5.3 Biashara 55

4.6 Hali ya Jamii ya Abakuria, Leo 56
4.7 Hitimisho 56
SURA YA TANO 58
MWANAMUME KATIKA NYISO NA JANDO 58
5.1 Utangulizi 58
5.2 Taswira za Kisaikolojia 59
5.2.1 Taswira ya Jiwe 59
5.2.2 Taswira ya Kuni na Ua 60
5.2.3 Taswira ya Mjumbe 61
5.2.4 Taswira ya Mchikichi 63
5.2.5 Taswira ya Seng'enge 64
5.2.6 Taswira ya Kipaza-sauti 65
5.2.7 Taswira ya Mtetezi 68
5.3 Taswira za Kimaumbile 69
5.3.1 Taswira ya Kalamu, Rungu na Upanga 69
5.3.2 Taswira ya Nyati na Tufani 70
5.3.3 Taswira ya Chaka la Retinde 71
5.3.4 Taswira ya Kifaru..... 73
5.3.5 Taswira ya Radi..... 74
5.4 Taswira za Kiuchumi 74
5.4.1 Taswira ya Mto Mara 75
5.4.2 Taswira ya Mwavuli (Irigamero/umwigamero)..... 76
5.4.3 Taswira ya Mwangaza (oborabu)..... 77
5.4.4 Taswira ya Uyoga..... 78
5.5 Taswira za Kitamaduni na Kijamii 79
5.5.1 Taswira ya Kiongozi "Rosogiro"..... 79
5.5.2 Taswira ya "Umurisia" 81
5.5.3 Taswira ya Daraja 82
5.6 Hitimisho 84

SURA YA SITA 86
MUHTASARI, MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO..... 86
6.1 Utangulizi 86

6.2. Muhtasari 86
6.3 Matokeo ya Utafiti 88
6.4 Hitimisho 90
6.5 Mapendekezo 90

MAREJELEO **92**
Vitabu **92**
Tasnifu **96**
Makala **97**
KIAMBATANISHO A **100**
RAMANI YA WILAYA YA KURIA **100**
KIAMBATANISHO B **101**
BAADHI YA NYISO ZA JANDO ZA ABAKURIA (IBIIKA) **101**
KIAMBATANISHO C **114**
ORODHA YA WAHOJIWA **114**

MAELEZO YA DHANA ZA KIKURIA KATIKA LUGHA YA KISWAHILI

Abachuma	-	kizazi miongoni mwa Abakuria
Abagaaka	-	wazee
Abagabo	-	wapiga ramli
Abagamunyeri	-	kizazi miongoni mwa Abakuria
Abagini	-	kizazi miongoni mwa Abakuria
Abaiseke	-	wasichana waliotahiriwa
Abakare	-	mashujaa
Abamaina	-	kizazi miongoni mwa Abakuria
Abamairabe	-	kizazi miongoni mwa Abakuria
Abanyamburiti	-	kizazi miongoni mwa Abakuria
Abanyangi	-	kizazi miongoni mwa Abakuria
Abarisia	-	wavulana ambao hawajatahiriwa
Abasae	-	kizazi miongoni mwa Abakuria
Abasagane	-	wasichana ambao hawajatahiriwa
ubusurusi	-	biashara
Amagiha	-	maviga
Amakora	-	vizazi
Amasambo	-	mashetani
Baaba	-	mama
Egaini	-	fahali
Ekemaho	-	sherehe za kuchukuliwa mahari kutoka kwao mvulana
Emoori	-	mtamba
Enchera	-	njia
Eng'eng'i	-	aina ya udongo mweusi au kijivu wenye madini mengi na hutumiwa kama chumvi ya ng'ombe
Eng'era	-	nyati
Enkoba	-	radi
Entang'ana	-	maksai
Esaiga	-	hirimu iliyojikita kwenye tohara
Esaro	-	sherehe za tohara
Gendia	-	tembeza
Gooko	-	nyanya/bibi

Ibihwi	-	mizuka
Ibiika	-	nyiso
Ichinkwe	-	kuni
Ichitinyi	-	wanyama
Igikurang'ati	-	mbweha
Ikihita	-	lango la boma/zizi
Ikimwenzo	-	kafara
Imigwi	-	mishale
Indwi/embehera	-	kaburi
Inture	-	mwanaume ambaye hana uwezo wa uzazi
Inyangi	-	sherehe za harusi
Inyimbo	-	fimbo
Inyumba mboke	-	ndoa baina ya mke na mke mwenza
Iriitongo	-	baraza la utawala
Moona mokari	-	mtoto wa kike
Obohariki	-	ndoa ya wake wawili au zaidi
Obokwe	-	posa
Oboori	-	boma/zizi la ng'ombe
Obota	-	upinde
Ogosooka	-	kuheshimu
Ogoteta	-	kuoa
Okong'anya	-	kuhama
Okorema	-	kulima
Omogambi	-	mtawala/kiongozi
Omogomba	-	mwanamke ambaye hana uwezo wa uzazi
Omokari/omogaikoro	-	mwanamke aliyeolewa
Omoteti	-	mwanamume aliyeoa
Omona	-	mototo
Omoroko	-	sherehe za kufuzu kutoka jandoni
Omosaacha	-	mwanamume
Omosamba	-	kijana aliyetahiriwa na bado hajatoka jandoni
Omosari	-	ng'ariba
Omosorori	-	mototo wa pekee katika familia
Rioba	-	jua

Sokoro	-	babu
Taata	-	baba
Ugukunguha	-	kuzeeka
Ugukura	-	kulia
Ugukwa	-	kufa
Ugusumacha	-	kuongea
Ugutura	-	kuamsha mtu kutoka usingizini
Umuhio	-	upanga
Umukungu	-	mwanamke mzee
Umusimuli	-	mwasisi
Uruku	-	kifo

UFAFANUZI WA ISTILAHI

Jando

Ni kipindi cha tohara ya wavulana, kipindi hiki hujumlisha kipindi cha matayarisho ya tohara, kipindi cha sherehe za tohara hadi kipindi cha kufuzu kwa watahiriwa 'omoroko'.

Nyiso

Ni nyimbo zinazoimbwa na wavulana katika kipindi cha jando. Nyiso huwa na 'ubeti' mmoja wenye mistari miwili hadi kumi na mitano. Ubeti unaweza kuwa na wazo moja au zaidi.

Utamaduni

Ni maisha ya kawaida ya watu husika; mazoea yao kama vile mila, siasa, dini na mifumo ya kiuchumi.

Bukuria

Eneo la makazi ya jamii ya Abakuria

Taswira

Ni matumizi ya lugha yanayopambanuliwa na uteuzi mzuri wa maneno na udhahiri wa maelezo wenye kuhuzisha na kujumuisha dhana mbamimbali ndani ya dhana moja ili kujenga picha mwafaka na athari maalum kwa hadhira. Aidha picha hii hutokana na maelezo au kwa matumiziya tamathali za usemi kama tashbihi na sitiari.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA TASNIFU

1.1 Usuli wa Mada

Abakuria ni nasaba ya Wabantu, wanaoishi mpakani mwa Kenya na Tanzania. Kwa upande wa Kenya wanaishi Wilayani Kuria, ambapo makao makuu ya Wilaya ni Kehancha. Kwa upande wa Tanzania wanaishi katika Wilaya ya Mara Kaskazini na Musoma. Eneo wanaloishi ni kati ya mto Migori (Kenya) na Mto Mara (Tanzania). Abakuria kwa hivyo wamegawika katika makundi mawili makuu, Abakuria wa Kenya na Abakuria wa Tanzania. Jamii hii vilevile imegwika katika milango kumi na mmoja; Abairge, Abanyabasi, Abakira, Abagumbe, Abatimbaru, Abanchari, Abakeroba, Abasweta, Abakenye, Abanata na Abangurueme.

Utafiti huu ulinuia kukusanya, kufasiri na kuchanganua nyiso za jando zinazoghaniwa na wavulana katika kipindi cha tohara. Kabla ya kipindi hiki wanaume na wanawake wenye tajiriba ya nyiso za jando huwafunza wavulana ambao wamefikia umri na wanajitayarisha kutahiriwa.

Jamii ya Abakuria ni ya kuumeni, hivi kwamba mwanamume hupewa hadhi ya juu kuliko mwanamke. Mwanaume ndiye mkuu wa familia na uamuzi wote wa maswala ya kifamilia na ya kijamii humtegemea. Mwanamke hujitokeza kama msaidizi tu. Swala hili ni motisha ya utafiti huu katika kukusanya baadhi ya nyiso za jando ambazo hubainisha sura fulani ya mwanamume wa Abakuria mintarafu ya matarajio mielekeo na itikadi zao za kitamaduni kumhusu mwanamume.

Tohara ni hatua muhimu sana kwa wavulana na wasichana wanaotazamiwa kuingia katika kundi la watu wazima katika jamii ya Abakuria. Aidha ni sehemu mojawapo ya utamaduni wa Abakuria inayobainisha na kuendeleza tofauti za kijinsia. Mvulana ambaye hajatahiriwa huitwa "umurisia" ilihali msichana huitwa "Omosagane". Tohara ya wavulana huhusisha kiwango kikubwa cha uchungu, lengo muhimu likiwa funzo kwa watahiriwa kuthamini ushujaa, nguvu na uwezo wa kustahimili hali yoyote ile. Hivyo basi tohara ni kipengele muhimu cha utamaduni wa Abakuria katika kukua kwa mwanamume kutoka utotoni hadi utu-uzima. Hii huifanya tohara kuwa kipengele fafanuzi cha mwanaume ambacho huhalalisha na kudhihirisha utambulisho wa mwanaume katika jamii ya Abakuria.

Taswira ya manamume katika jamii za Kiafrika ni swala ambalo limeibua changamoto katika mijidala na kongamano mbalimbali, hasa kwa misingi ya uhalisia wa nadharia tete ya uwezo-uume. Tanzu mbalimbali za fasihi ya Kiafrika humsawiri mwanamume kwa njia tofauti na mwanamke. Tafiti nyingi zimefanywa katika jamii mbalimbali kwa kuzingatia tanzu mbalimbali za fasihi, hasa kwa kuangaza sura ya mwanamke. Matokeo ni kwamba mwanamke hutwezwa ilhali mwanaume hukuzwa. Kwa mujibu wa utafiti huu, ni machache yamebainishwa kuhusu taswira ya mwanaume wa Abakuria inavyojitokeza katika utanzu wa nyiso za jando kama mojawapo ya tanzu za fasihi simulizi ya Abakuria na iwapo kuna utafiti ambao umefanywa karibu na huu ni kwa madhumuni na misingi tofauti.

Ingawa wanaume kama kundi hujitokeza katika sura mbalimbali katika utamaduni mahususi, ni hivi karibuni tu ambapo wasomi na idara mbalimbali zimejishughulisha katika kuchanganua nafasi ya mwanaume katika jamii kwa misingi ya kiuana. Wanaume hupewa uwezo walio nao katika jamii kwa kipindi cha mchakato wa ujamiishaji. Matokeo yake, kadri anavyoendelea kukua na kufikia umri wa kutahiriwa, uume na uwezo wa jinsia ya kiume huendelea kujitokeza takribani maishani mwake.

Wamitila (2003) anasema, nyimbo na ushairi huwa ni hifadhi au rekodi muhimu ya historia katika jamii na hutumiwa kama nyenzo muhimu ya kupitisha thamani za kitamaduni. Nyimbo na ushairi wa jamii huakisi vipengele mbalimbali vya utamaduni na matarajio ya jamii. Hivyo basi, nyiso kama kipengele muhimu cha utamaduni wa jamii ya Abakuria hubainisha falsafa kuhusu maisha yao, matarajio yao na mitazamo yao ya kilimwengu.

Katika miaka ya hivi karibuni makongamano mbalimbali yameandaliwa; kusudi kubwa ni kuchunguza upya nafasi ya mwanaume na majukumu yake mintarafu ya uchumi, siasa na jamii. Urejeleo ukiwa kwa mamlaka anayopewa mwanaume kupitia kwa lugha, itikadi na utamaduni, mielekeo, matarajio na mitazamo ya jamii.

Nyiso za jando miongoni mwa Abakuria husheheni maadili na amali za kijamii ambazo zinaeleweka katika muktadha wao wa kitamaduni. Ukubalifu na imani kwa utamaduni wao ni kutokana na ujamiishaji wa miundo mahsusi ya kujieleza ambayo hujikita katika kufungamanisha jana, leo na kesho yao. Ni kutokana na kauli hizi ambapo utafiti huu ulichunguza taswira ya mwanaume wa Abakuria inavyokuzwa na kubainishwa kupitia kwa nyiso za jando.

Ni muhimu kutaja kuwa nafasi ya wavulana na wanaume katika jamii ya Abakuria huundwa kutokana na vipengele vya Kijamii na vya kitamaduni ambavyo humfanya mwanamume kuwa na uwezo mkubwa na kupanua uhusika wao katika shughuli za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Nyiso za jando huwa na umuhimu wa kipekee unaoeleweka katika muktadha huu wa tohara katika kubainisha na kuendeleza tofauti ya mwanaume na mwanamke

1.2 Mada ya Utafiti

Kwa zaidi ya miongo miwili dhana ya jinsia imekuwa kitovu cha tafiti nyingi katika mtalaa wa Kiafrika, swala ambalo limeibua haja ya malighafi ya kutosha kukidhi mahitaji ya watafiti wengi. Hata hivyo mwanamume amepewa nafasi finyu katika tafiti hizo kama mhusika. Hali hii inazua umuhimu wa kukusanya, kuchanganua na kubainisha taswira ya mwanaume wa Abakuria na ujenzi wa dhana ya uume katika nyiso za jando miongoni mwa Abakuria. Nyiso za jando miongoni mwa jamii ya Abakuria ni utanzu ambao fasili mahsusi ya kitamaduni ya mwanamume na uume huweza kueleweka na kuchanganuliwa. Aidha ni muhimu kutaja kuwa jamii ya Abakuria ni ya kuumeni, hali ambayo hubainisha tofauti kubwa baina ya mwanamume na mwanamke.

1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu ulidhamiria kutimiza malengo yafuatayo:

i. Kutathmini mchango wa nyiso za jando katika kujenga na kukuza uwezo uume.
ii. Kudhihirisha utambulisho wa mwanaume na jinsi anavyosawiriwa katika jamii kupitia kwa uchanganuzi wa nyiso za jando.

1.4 Nadharia Tete

i. Nyiso za jando zina mchango mkubwa katika kujenga na kuhifadhi uwezo-uume miongoni mwa jamii ya Abakuria.
ii. Mwanamume katika jamii ya Abakuria husawiriwa kwa njia chanya tofauti na mwanamke.

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ulipewa motisha na ukweli kwamba swala la usawiri wa mwanaume katika nyiso za jando halijashughulikiwa na iwapo limegusiwa ni chini ya mada na misingi tofauti. Hivyo basi matokeo ya utafiti huu ni mchango mwafaka katika tahakiki zilizoko kuhusu taswira ya mwanamume katika tanzu zingine za fasihi ya Kiafrika.

Utafiti wetu ulinuia kukusanya baadhi ya nyiso za jando; kwa kufanya hivyo utafiti huu ni mchango mahususi wa kuhifadhi mojawapo ya tanzu za fasihi ya Abakuria katika maandishi. Ni muhimu kutaja kuwa nyiso za jando hutoa mafunzo fulani kwa watahiriwa, ikizidi huwa na umuhimu wa kendeleza na kuhifadhi maadili ya utamaduni wa Abakuria. Hivyo,utafiti utachangia katika kuhifadhi sehemu muhimu ya utamaduni huu katika maandishi.

Ukwasi wa jarabati, nadharia na masuala ya methodolojia ambayo yalihusishwa katika utafiti huu kuhusu taswira ya mwanaume na uwezo-uume ni mchango muhimu katika taasisi za masuala ya kijisia

Utafiti wetu unatoa jukwaa mwafaka kwa wasomi wa Kiafrika ambao watanuia kutafiti zaidi juu ya dhana ya uume. Unanuia kuauni ushahidi wa kuaminika kuhusu uume katika jamii ya Abakuria

Utafiti huu vilevile utasaidia katika kumwezesha mtafiti yeyote yule ambaye atahitaji vipengele sawa au tofauti vya nyiso za jando miongoni mwa jamii ya Abakuria na jamii zingine zenye mila, desturi na utamaduni unaokaribiana na wa jamii hii.

Wizara ya utamaduni na jinsia inaweza kutumia matokeo yetu ya utafiti katika kupanga na kuratibu shughuli za kitamaduni katika wilaya ya Kuria pasipo kukinzana na mielekeo na matarajio ya Abakuria mintarafu ya jinsia.

1.6 Upeo wa Utafiti

Mbali na nyiso za jando kuna tanzu nyingi za fasihi ya Abakuria ambazo tungeweza kuzitafiti ili kudhihirisha jinsi zinavyomsawiri wanamume. Mfano: methali, vitendawili, nyimbo, hadithi, visasili na khurafa miongoni mwa zingine. Utafiti huu ulijikita katika utanzu wa nyiso za jando na tulijaribu kuchunguza jinsi ambavyo utanzu huu unamsawiri mwanamume wa Abakuria. Utafiti ulizingatia nyiso zinazoghaniwa na wavulana kipindi cha tohara, na ambazo zinabainisha mielekeo, itikadi, matarajio na majukumu ya mwanamume.

Hatimaye tulijaribu kuzihusisha na muktadha wa jamii hii ili kutathmini picha halisi ya mwanamume katika jamii ya Abukuria.

Utafiti wetu ulijikita katika nyiso za jando katika mlango (ukoo) wa Abairege wa Kenya ambao ni mojawapo ya milango takribani kumi na mmoja ya Abakuria. Abairege wa Kenya wanaishi katika tarafa ya Ntimaru wilaya ya Kuria nchini Kenya. Hii ni kwa sababu, haingewezekana kutafiti mada hii katika jamii nzima ya Abakuria wa Kenya na wa Tanzania hasa kwa kuzingatia muda na gharama ya utafiti.

Kwa kurejelea taswira ya mwanaume tulijikita katika maeneo ya; uchumi, ndoa, mamlaka, majukumu, utawala, mielekeo na matarajio ya jamii kuhusu nafasi ya mwanamume katika jamii.

1.7 Hitimisho

Sura hii mmejadiliwa mambo muhimu yanayohusu mada ya utafiti. Imeanza kwa kujadili usuli wa mada; ambamo pameelezwa Abakuria ni kina nani na wanaishi wapi. Aidha, umuhimu wa tohara miongoni mwa Abakuria umeelezwa. Mmejadiliwa pia motisha ya utafiti na mada ya utafiti. Sura hii vilevile, inafafanua; madhumuni ya utafiti,nadharia tete, umuhimu wa utafiti na upeo wa utafiti.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI

2.1 Utangulizi

Katika sura hii mmejadiliwa mapitio ya maandishi muhimu yanayohusiana na mada yetu ya utafiti na pia uhakiki wa nadharia ambazo tulizitumia katika utafiti wetu. Katika sehemu ya mapitio ya maandishi mmejadiliwa yale ambayo yameshughulikiwa na mwanya ambao utafiti wetu ulikusudia kuziba. Katika sehemu ya msingi wa nadharia mmejadiliwa misingi mwafaka ya nadharia tulizozitumia katika utafiti na uchanganuzi wa deta.

2.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Abakuria

Kuna wasomi mbalimbali ambao wameandika kuhusu jamii ya Abakuria, wengi wa waandishi hao wamebobea zaidi upande wa historia, utamaduni na fasihi ya Abakuria. Mengi ya maandishi yaliyopatikana yamelenga historia na maswala ya kianthropolojia. Hata hivyo katika baadhi ya kazi hizo, sura ya mwanaume hujitokeza hapa na pale.

2.2.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Utamaduni wa Abakuria

Kirsten na Svensson (1983) wanaeleza Abakuria, kama mojawapo ya jamii za Wabantu wanaoishi katika vilima vya Mara na uwanda wa Serengeti nchini Tanzania na Kenya. Wanaendelea kusema kwamba kwa muda mrefu Abakuria wamejihusisha na uchumi mseto wa ukulima na ufugaji. Wameshikilia kindakindaki utamaduni wao ambao ni sehemu ya maisha yao. Mifugo, hasa ng'ombe, huwa na dhima muhimu katika matambiko yao na uchumi wao. Kwa sababu hizi Abakuria huthamini sana ng'ombe, kiasi ambacho wako radhi kupigana wenyewe kwa wenyewe au hata na majirani wao kwa sababu ya mifugo hawa.

Kwa upande wa majukumu, Kirsten na Svensson Wanabainisha mgawanyo wa majukumu kiuana, hivi kwamba majukumu yenye kuhitaji nguvu nyingi na yanayochukuliwa kuwa na thamani kubwa yametengewa wanaume, ilhali wanawake hutekeleza majukumu madogomadogo yenye kuhitaji nguvu kadri. Mwanaume, ndiye humiliki ng'ombe na hutekeleza

majukumu yote muhimu yanayoandamana na ufugaji wa ng'ombe. Hivyo, thamani ya ng'ombe katika jamii ya Abakuria huenda sambamba na thamani ya mwanamume.

Katika upande wa ndoa, Kirsten na Svensson, wanabainisha uwezo na madaraka makubwa anayohodhi mwanamume. Kwa mfano, wanasema, wasichana walihesabiwa katika rika la vijana wa kiume waliotahiriwa nao hadi pale walipoolewa. Baada ya kuolewa msichana alijiunga na rika la mume wake. Kauli inayobainisha kuwa mwanamke ni sehemu ya milki ya mwanamume.

Kirsten na Svensson, katika, michoro mbalimbali ya picha ndani ya kitabu chao, wanabainisha mavazi na maleba ya wanaume, hali ambayo humsawiri mwanaume kama shujaa na shupavu, kwani katika baadhi ya picha mwanamume amejifunga kipande cha ngozi ya chui au simba, ana mkuki, sime na ngao, zana hizi ni za kivita hali ambayo hubainisha kuwa mwanaume sharti awe tayari katika kulinda na kupigania jamii yake. Aidha, wasomi hawa wanasisitiza umuhimu wa tohara katika jamii ya Abakuria, kwani ni ishara ya uwezo na uhalalisho wa ushujaa na ukali katika kutetea jamii yake. Vilevile ni baada ya tohara kijana wa kiume huruhusiwa kuingia katika kundi la watu wazima Tohara ilikuwa sharti muhimu katika kuoa au kuolewa.

Kutokana na kazi hii, inadhihirika wazi kuwa kaida, mila na desturi za Abakuria ni mchango mkubwa katika kujenga na kukuza uume. Aidha, hubainisha na kuratibu majukumu ya wanajamii katika awamu mbalimbali za maisha yao kwa misingi ya kijinsia. Kirsten na Svenson wanasema.:

> ...wajibu mkubwa wa mwanamume wa Abakuria ni kulinda jamii kutokana na maadui...mashambulio ya kupora ng'ombe kutoka kwa maadui wao lilichukuliwa swala la kawaida na muhimu. Vita na uvamizi huu ni matukio yanayodhihirisha ujasiri na ushujaa.(tafsiri yangu)

Ni wazi kuwa kazi hii imezingatia zaidi utamaduni, imani, mila na desturi, itikadi na mitazamo ya jamii ya Abakuria hali ambayo ni tofauti na utafiti wetu. Hata hivyo, kazi hii ni mwafaka katika hatua ya kubainisha historia na hali ya maisha ya jamii ya Abakuria kwa jumla. Vilevile, ni mchango katika kutathmini sura ya mwanaume inavyobainika katika nyiso za jando.

Max Weiss (1910) amesisitiza umuhimu wa utamaduni katika kuendeleza maisha ya wanajamii. Anasema mpangilio wa jamii huongozwa na utamaduni huu, na ni sehemu muhimu inayotawala mielekeo na matarajio ya jamii kwa kila mwanajamii.

Max, anabainisha awamu mbalimbali za kila mwanajamii na matarajio na mielekeo ya jamii kwa kila awamu mintarafu ya majukumu, mavazi na tabia. Haya yote huunda sura mahususi ya mwanamume na mwanamke katika jamii. Hivyo basi, kutokana na kazi hii, mila, desturi na kaida za jamii ni sehemu muhimu katika uundaji na uhifadhi wa sura ya mwanamume katika jamii za kiafrika.

Max, amezingatia sana maswala ya kitamaduni ya Abakuria yanavyotawala jumla ya maisha ya jamii hii. Utafiti wetu uliangaza nyiso za jando kama utanzu wa fasihi na jinsi unavyomsawiri mwanaume na swala zima la ujenzi wa uume. Hata hivyo, kazi ya Max ilikuwa mwafaka katika utafiti huu katika sehemu ya historia na jumla ya hali ya maisha ya Abakuria kumhusu mwanamume.

2.2.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Fasihi ya Abakuria

Chacha, L.(1997) ameshughulukia majigambo ya Abakuria. Ameeleza majigambo kama sanaa ya unenaji uliyo na utendaji ambayo kwayo mtu hujisifu na kutangaza sifa zake mbele ya hadhira. Aidha anaeleza kuwa majigambo ni sanaa ya ushairi ambayo hutumia maneno yenye mvuto ya kuibua hisia zinazowaathiri wasikilizaj na kuwafanya wahisi furaha au uchungu. Majigambo huhodhi sifa za mtu binafsi, ukoo, kabila, mnyama au kitu fulani. Tofauti baina ya nyiso na majigambo hujitokeza katika mkutadha wa matumizi ya fani hizi miongoni mwa Abakuria. Kwani nyiso hutumika katika kipindi cha tohara pekee, ilihali majigambo ni sanaa ambayo hutumiwa na mtu yeyote katika sherehe mbali mbali za jamii. Kazi hizi vile vile zinatofautiana katika matumizi ya nadharia. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi wa nadharia ya Uwezo uume ilihali Chacha aliongozwa na nadharia za Umuundo na Semiotiki. Nadharia hizi zilimruhusu kuhakiki miundo katika majigambo nayo semiotiki ikamwongoza kuchunguza maswala ya kijamii na ya kitamaduni. Licha ya tofauti hizi, kazi ya Chacha imechangia kwa namna mbalimbali kwa kuwa imerejelea jamii ambayo imeshughulikiwa katika utafiti huu.

Chacha,D.(1991) ameshughulikia vitendawili: maana na matumizi katika jamii ya abakuria. Katika utafiti wake amezingatia maana na matumizi ya vitendawili. Amebainisha kuwa vitendawili ni utanzu wa fasihi simulizi ya Abakuria ambavyo vina matumizi mapana katika misingi ya kitamaduni ya kimazingira kuliko kuchemsha bongo za watoto. Kazi hii ni tofauti na yetu, kwani utafiti wetu umezingatia nyiso za jando huku tukichanganua taswira za mwanamume zinazobainika humo. Kadhalika, nadharia zinazoongoza tafiti hizi ni tofauti.

Chacha ameongozwa na matazamo wa kiishara ilihali utafiti wetu umeongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi na nadharia ya Uwezo-uume. Kazi ya Mathew imechangia utafiti wetu kwa upande wa mambo kadha ya kitamaduni aliyoyabainisha katika utafiti wake, ili kuweka wazi mielekeo na matarajio ya kijamii kuwahusu wanaume.

Mwita, B.(2005) ameshughulikia *ichingero.* Ameeleza *ichingero* kama sanaa ya unenaji anayoitumia mwanaume kumsairi mwanamke kwa lengo la kumwendekeza ili akubali kumpenda.Anaendela kueleza kuwa *ichingero* kama sanaa ya lugha hutumia maneno yaliyoteuliwa na kupangwa kwa mnato na mtiririko wenye mantiki. Kadhalika, lugha ya *ichingero* imejaa tamathali za usemi ili msanii aweze kuwasilisha ujumbe anaodhamiria. Tofauti ya *ichingero* na nyiso hudhihirika katika mkutadha na madhumuni ya matumizi ya fani hizi miongoni mwa abakuria. *Ichingero* hutumiwa na wanaume peke yao kuwasawiri wanawake, kwa upande mwingine, nyiso hutumiwa katika kipindi cha tohara kubainisha mielekeo na matarajio ya jamii kuwahusu wanaume. Aidha, *ichingero* ni sanaa ya unenaji inayotumika katika muktadha fiche uliofungiwa katika mahusiano ya kijinsia. Vilevile, nadharia zilizotumiwa zimetofautiana. Utafiti wetu uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi na nadharia ya Uwezo-uume ilhali Mwita aliongozwa na nadharia ya Unisai Yakinifu Licha ya tofauti hizi, kazi ya Mwita imechangia kwa namna nyingi kwa kuwa imeangaza jamii ambayo imeshughulikiwa na mtafiti.

Svensson (1994) anaeleza methali kama muhtasari wa yale ambayo tajriba imewafunza wanajamii. Katika maelezo yake kuhusu fasihi, anasema fasihi huunda wajibu muhimu katika upitishaji wa thamani na maarifa ya jamii kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine. Fasihi, hufunza, hukanya na kushauri na kwa kufanya hivyo hubainisha yale yanayoitambulisha jamii kuhusu wanayoyathamini na wanayoyachukia. Svensson anatoa kauli kwamba, kusisitiza umuhimu wa utamaduni katika jamii huwapa wanajamii utambulisho juu ya thamani, imani

mielekeo na utawala wa jamii. Anaendelea kusema kwamba, methali sawa na tanzu zingine za fasihi ya jamii hupitisha thamani za jamii, imani, desturi na haki za kila mwanajamii.

Kazi hii ni tofauti na utafiti huu, kwani Svensson ameorodhesha baadhi ya methali ndani katika za Abakuria na kuzitafsiri kwa lugha ya Kingereza na amezungumzia umuhimu wa fasihi kwa jumla. Utafiti wetu ulilenga utanzu wa nyiso jando na kuzama kuchanganua jinsi utanzu huu unavyomsawiri mwanaume na hasa zaidi mchango wa utanzu huu katika kujenga na kukuza uwezo-uume.

Otube na Wengine (1989) wamechunguza kuhusu nyimbo na ngoma za kitamaduni katika jamii ya Abakuria na nafasi zao katika kuendeleza na kuhifadhi utamaduni. Utafiti wao umeegemea mtazamo wa kianthropolojia. Utafiti wetu ulienda mbele katika kudhihirisha taswira ya mwanamume katika nyiso za jando.

2.2.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Utawala na Historia ya Abakuria

Tobisson, E. (1986) ameeleza kwa kina siasa na mpangilio wa kiutawala wa jamii ya Abakuria. Katika kazi hii mwanamume ndiye kiongozi wa kaya na jamii, na maswala ya siasa humhusu mwanaume pekee. Aidha, Tobisson ameeleza kwa uwazi zaidi utambulisho wa kila mwanajamii wa Abakuria mintarafu ya rika na kizazi, katika maelezo yake inabainika bayana kuwa mwanamke ni milki ya mwanamume kwani utambulisho wa mwanamke hubainika kupitia kwa rika na kizazi cha mume wake. Kwa mujibu wa utangamano na mtagusano wa wanajamii, Tobisson amemchora mwanamume kama kiumbe mwenye uwezo na mamlaka juu ya raslimali muhimu za jamii, hivi kwamba ardhi na vyote vilivyomo ni milki ya mwanamume. Mwanamke hana nafasi ya kurithi ardhi kutoka kwa wazazi wake au mume wake. Kazi ya Tobisson imeegemea sana upande wa historia na sosholojia ingawa kauli zake ni mchango muhimu katika uchanganuzi wa data na uelewa wa utamaduni na mitazamo ya jamii ya Abakuria kumhusu mwanamume.

Abuso (1980) ameandika kuhusu historia ya Abakuria kati ya 1400-1914, amezingatia chimbuko lao, uhamaji wao, makazi yao, marika mbalimbali, utamaduni wao na mpangilio wa kisosholojia na kisiasa. Ni bayana kuwa hakugusia swala la nyiso za jando. Mchango wake kwa utafiti huu ulikuwa wa kihistoria na ulituwezesha kujua Abakuria ni kina nani na wanaishi wapi. Aidha amegusia baadhi ya maswala muhimu ya utamaduni wa Abakuria, tohara ya wavulana na wasichana ikiwemo.

2.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ya Utafiti

Ingawa usomi wa jinsia na uana umekuwa katika kasi kwa takribani miongo mitatu na nusu, umezingatia zaidi maswala ya kike. Sehemu ya uume katika maswala ya jinsia ni somo ambalo liko katika awamu ya mwanzo.

Katika kuchunguza vitabu na tafiti mbalimbali kuhusu taswira ya mwanaume katika nyiso za jando miongoni mwa jamii ya Abakuria, ilidhihirika ni machache yameandikwa. Hii ni kutokana na sababu kwamba mada hii haijashughulikiwa. Kazi tulizozitumia zilikuwa ni kwa minajili ya kuthibitisha pengo lililopo ambalo utafiti huu ulinuia kuziba na ikizidi kazi hizi zilitoa mchango kwa njia moja au nyingine katika kufanikisha utafiti huu.

Mackinon (1987) anabainisha uhalalisho wa uwezo na mamlaka ya juu anayoyamiliki mwanamume katika jamii. Anadokeza kuwa, kutokana na hali hii mwanaume huhodhi amri na nafasi pana ya utawala. Anaendelea kusema kwamba wanaume wana shauku kubwa ya kuoa wanawake wawili au zaidi na ikizidi tamaa hii humwelekeza mwanaume kuwa na wapenzi wengi nje ya ndoa. Aidha, Mackinnon anadokeza kwamba, ili mwanaume aweze kujitosheleza na kutosheleza familia yake sharti awe na nguvu za kimaumbile zaidi ya mwanamke. Ni bayana kuwa kazi hii ya Mackinnon haielezei chanzo na ukuzaji wa uwezo huu wa mwanamume, swala amabalo utafiti wetu ulilenga kulijibu kwa kina. Hata hivyo, kazi hii ilkuwa mchango mwafaka katika uchanganuzi wa data hasa juu ya hadhi anayopewa mwanaume na jinsi ambavyo jamii ya Abakuria kupitia kwa utanzu wa nyiso za jando hudhihirisha na kukuza sura hii ya mwanamume.

Mackinon anaendelea kusema, kuwa mwanamume katika jamii hujitokeza kama mtawala na mwenye mamlaka makubwa, ikizidi mwanamke ni milki ya mwanaume. Rai hii ilikuwa msingi katika sehemu ya uchanganuzi wa data hasa kutathmini majukumu, mielekeo na matarajio ya jamii juu ya utambulisho wa mwanaume katika jamii ya Abakuria.

Katika kazi yao Michele na Coltrane (2005) wanabainisha umuhimu wa historia na utamaduni wa jamii katika kujenga na kukuza uwezo-uume. Wanadokeza na ninakubaliana nao, kwamba jamii zote hujamiisha watoto kwa jinsi ambavyo wanavyoendelea kujifunza sheria na kaida za jamii yao ambazo huendeleza na kutawala tabia za kijumla za kila mwanajamii. Sheria na kaida hizi huwafanya wanajamii kutenda na kushiriki katika jamii kulingana na mahitaji yanayoandamana na jinsia yao . Michele na Coltrane Wanasema:

> ... ujamiishaji na mifanyiko tendani maishani ambayo huruhusu kila mwanajamii kuingia na kutoka katika makundi mahususi ya jamii ni zao la utamaduni wa jamii hiyo. Sehemu moja ya mifanyiko tendani hii huhusisha ujamiishaji wa kijinsia: yaani, ujifunzaji wa sheria na kaida andamizi na jinsia ya kike au ya kiume. Sheria na kaida hizi ndizo humfanya kila mwanajamii kutenda na kufuata mwenendo unaokubalika kulingana na jinsia yake(tafsiri hii ni yangu na zitakazofuata)

Kazi ya wasomi hawa inasisitiza kwamba, familia ni asasi muhimu katika uzalishaji na ukuzaji wa thamani za kijinsia. Ni katika familia ambapo wavulana humaizi fadhila za hadhi yao na jinsi ambavyo fadhila hizi humpa mwanaume uwezo na mamlaka makubwa katika jamii. Ni katika familia ambapo watoto wa kiume hujamiishwa katika kumiliki na kubainisha sifa zao za kiume.

Ingawa utafiti huu unagusia sura ya mwanaume katika jamii, umebobea sana katika utamaduni na swala la ujamiishaji wa wanajamii, vilevile wasomi hawa wamesisitiza umuhimu wa familia katika kujenga na kukuza utengano wa kijinsia mintarafu ya majukumu, tabia na mitazamo. Aidha, kazi hii inatofautiana na utafiti wetu, kwa misingi ya nadharia na hasa zaidi utafiti wetu ulizingatia utanzu wa fasihi simulizi ya jamii ya Abakuria. Hata hivyo, kazi ya wasomi kawa ilitufaa sana katika kuelezea mifumo ya kisiasa, kidini na kiuchumi ya jamii ya Abakuria na mchango wa utamaduni katika kujenga na kukuza sura ya mwanamume. Vilevile kazi hii ilikuwa mchango mwafaka katika sehemu ya uchanganuzi wa data..

Holter (2005) anadhihirisha uwezo na fadhila katika mfumo wazi wa utawala msonge wa kijinsia. Kategoria anazosisitiza katika mfumo huu ni wanaume na wanawake. Anadokeza kuwa uchanganuzi wa usawa au utofauti wa kijinsia uangazwe kwa misingi ya wajibu wa jamii katika kuhalalisha nafasi kubainisha na ya kila jinsia. Anaendelea kusema kwamba, jamii huwa na jukumu la kuwaweka wanajamii katika kategoria sawa au tofauti kutegemea jinsia. Mfumo huu hujengwa na: uchumi, utamaduni, saikolojia na mahitaji ya kijamii. Vipengele hivi ni mchango muhimu katika kumjamiisha mwanamume kama mkimu-familia; wajibu ambao ni wa kimsingi katika jamii.

Kauli za Holter zilikuwa mchango mwafaka katika utafiti huu hasa katika uchanganuzi wa data. Hii ni kwa sababu tulizitumia kama mwongozo wa kutathimini thamani na mantiki ya yaliyomo katika nyiso za jando na mchango wake katika kumpa mwanamume sura mahususi. Holter, vilevile anasisitiza utofauti wa kijinsia kuangazwa kwa misingi ya wajibu wa jamii kuhalalisha utofauti huu. Utafiti wetu ulienda ndani katika kubainisha sifa na majukumu ya kijinsia na jinsi majukumu haya huratibiwa na kuhalalishwa na jamii kupitia kwa utanzu wa nyiso za jando, kwa sababu fasihi ni zao la jamii.

Katika makala ya Rogers (2004) anamweleza mwanamume kama binadamu mwenye uwezo na mamlaka; naye mwanamke hujitokeza kama jinsia saidizi,.Rogers anasema;

> ...wanaume wanatawala jamii, hivi kwamba wanachokipenda, wanachotaka au wanachopenda kukiona kinatendeka... katika hali hii wanawake hupata haki haba. Wanaume hawako radhi kupunguza madaraka yao juu ya raslimali za jamii na katika mchakato wa uamuzi katika jamii.

Nao wanawake hujamiishwa kwa misingi ya utamaduni wa jamii husika katika kutekeleza majukumu ya kike.Rogers, anasisitiza umuhimu wa utamaduni kama sehemu muhimu ya utenganisho wa kijinsia. Kazi hii inatofautiana na utafiti wetu, kwa kuwa Rogers alilenga kubainisha nafasi ya mwanamume na jinsi anavyofikiria juu ya usawa wa kijinsia. Ilhali utafiti wetu uliangaza sura ya mwanaume katika jamii ya Abakuria na mchango wa nyiso za jando katika kubainisha sura hii. Hata hivyo, kazi hii ilikuwa muhimu katika utafiti huu; ilitusaidia kuchanganua iwapo mwanaume anadhihirika kama mwenye uwezo na mamlaka katika nyiso za jando.

De Keijzer (2004) anadokeza umuhimu wa utamaduni katika ujenzi na ukuzaji wa uume. Utamaduni huathiri jinsi ambavyo kila jinsia hujamiishwa. Anaendelea kusema:

> ... imani juu ya uwezo wa wanaume kuhusu mamlaka yao juu ya wanawake huhalalishwa na utamaduni... juu ya utumishi wa wanawake kwa wanaume, ni imani zinazojengwa na utamaduni wa jamii husika.

Utamaduni na milekeo ya jamii huhalalisha viitikio vya matumizi ya nguvu nyingi kama njia moja ya marekebisho ya tabia za kike. Kwa mfano, mwanaume hatakikani kuonyesha hisia za uoga na huzuni, kwani tabia hizi huchukuliwa kuwa za kike. Anaendelea kusema kwamba, pindi wavulana wanapobaleghe, wengi wao huanza kujifunza tabia zinazojenga na kukuza uume na utambulisho wao kama wanaume, ambazo huwaepusha katika kudhihirisha baadhi ya hisia na kuwahimiza kuonyesha hisia, kwa mfano za hasira na ukali. De Keijzer anasema:

> ...sura ya ubaba ya; ukali, mwenye nguvu, mgandamizaji na mwenye uchu kwa wanawake... ni mtindo uliorithishwa kwao, ni namna walivyofunzwa kuwa wanaume...

Ni wazi kuwa mwandishi amesisitiza umuhimu wa jamii na utamaduni wake katika kujenga utambulisho wa mwanaume, hali ambayo ni tofauti na utafiti wetu. Utafiti wetu ulizingatia nyiso za jando kama mojawapo ya tanzu za fasihi simulizi ya Abakuria na kuchanganua nafasi yake katika kujenga na kukuza uume na mchango wake katika kubainisha sura mwafaka ya mwanaume wa Abakuria. Hata hivyo kazi hii ya De Keijzer ilikuwa muhimu katika kutathmini taswira ya mwanamume inavyojitokeza katika nyiso za jando.

Katika kazi ya Matteru (1982) mwanamume amesawiriwa kama chanzo cha matatizo yanayomkumba mwanamke mintarafu ya mahusiano yao katika jamii. Ingawa kazi hii imeshughulikia fasihi simulizi, imeegemea sana katika kubainisha taswira ya mwanamke. Kazi hii inatofautiana na utafiti wetu kinadharia na katika malengo ya utafiti. Ukweli wa kazi hii hata hivyo, ulikuwa msingi katika kuchanganua sura ya mwanaume katika nyiso za jando.

Choti (1998) amebainisha kupitia data alizozikusanya kuwa katika leksia ya lugha ya Kikisii mwanamume amechorwa kama binadamu mwenye nguvu tofauti kabisa na mwanamke. Katika utafiti huu Choti amedhihirisha kuwa mwanamume huangazwa kwa mtazamo chanya, ilhali mwanamke huangazwa kwa mtazamo hasi. Choti amemrejelea mwanamke; kazi yake inatofautiana na hii yetu kinadharia. Hata hivyo, tulitumia kauli zake kama mojawapo ya vigezo vya kuthibitishwa iwapo nyiso za jando humsawiri mwanamume kama binadamu mwenye nguvu na mamlaka tofauti na mwanamke katika jamii ya Abakuria.

Wandera (1996) amethibitisha kuwa ushairi wa Waswahili wa kipindi hicho haukumtweza mwanamke wala kumkuza mwanamume. Bali ulitenganisha majukumu na nafasi ya kila mmoja kwa misingi ya vigezo vya: uana, maumbile, sheria za dini ya kiisilamu, mila,

siasa na mfumo wa kiuchumi. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa msingi kwamba umeangaza sura ya mwanamke. Hata hivyo, ulikuwa na mchango wa kutusaidia katika ukusanyaji wa deta. Maoni yake vilevile yalikuwa msingi wa uchanganuzi wa data.

Katika jarida la *Gender Health and Sustainable Development: A Latin American Perspective* (1994) inabainika wazi kuwa jamii ya Walatini na Wamarekani, wanaume walifanya kazi tofauti na wanawake. Kazi walizozifanya wanaume ni zile za sulubu, ukulima, ufugaji wa wanyama na uhandisi ilhali wanawake walikuwa wasaidizi tu, kuzaa, kupika, kuosha nguo miongoni mwa kazi zingine rahisi. Kauli hii ilitumika kama msingi wa kutathmini iwapo nyiso za jando miongoni mwa Abakuria zinaratibu majukumu ya kijamii kwa misingi ya uana.

Mazrui (1981) anabainisha jinsi ambavyo utamaduni umeratibu shughuli za kijamii kwa misingi ya uana. Swala la siasa lapaswa kuwa la mwanamume na mahala pa mwanamke ni jikoni na shughuli kubwa ni kuwalea na kuwatunza watoto. Rai hii ilikuwa kigezo cha kutathmini mchango wa utamaduni, kupitia kwa jinsi nyiso zinavyoratibu majukumu ya jamii mintarafu ya uana.

Richmond (1992) katika utafiti wake wa ujamiishaji awali wa majukumu ya kijinsia, amebainisha kuwa lugha ni kitengo muhimu cha jamii, ambacho ni mithili ya kioo katika kuutazama utamaduni wa jamii. Lugha hubainisha mipaka ya fikra na uwezo wa kuelezea hali fulani ya jamii. Katika tamaduni zingine lugha hubainisha tofauti za kijinsia mintarafu ya majukumu na mahusiano yao. Utafiti huu ni tofauti na wetu lakini kauli zake zilitusaidia katika uchanganuzi wa yaliyomo katika nyiso za jando ili kubainisha taswira ya mwanamume.

Muindi (1990) alichunguza usawiri wa wahusika makahaba katika riwaya za S.A Mohammed. Utafiti huu ulidhihirisha kuwa ukahaba ni swala la kiuchumi na mwanamke husawishika kuingia kwenye ukahaba kwa sababu nyenzo zote za uchumi wa jamii zinamilikiwa na mwanamume. Hivyo basi, mwanamume anabainika kuwa na uwezo mkubwa wa uchumi kuliko mwanamke. Ingawa utafiti huu ni tofauti na wetu, utatusaidia katika kuthamini iwapo mwanamume wa Abakuria amesawiriwa kama mwenye uwezo wa kiuchumi, huku mwanamke akijitokeza kama mhitaji.

Maandishi mengi tuliyoyapitia yalitupa mwongozo kuhusu njia mwafaka za kutumia katika ukusanyaji wa deta na vilevile kuhusu uchanganuzi wa nadharia mwafaka tulizozitumia. Isitoshe yalitusaidia kubainisha ni yapi yamefanywa na wengine ili kujua ni mkondo upi utafiti wetu ungefuata ili kuziba mwanya ulioachwa na watafiti wa awali.

2.4 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi na Nadharia ya Uwezo – uume. Viambajengo vya lugha hususan taswira na jazanda vilichanganuliwa na kuhakikiwa ili kuweka wazi itikadi, mitazamo na mielekeo ya kiume inayotawala mtagusano na utangamano wa wanajamii.

Nadharia ya Uwezo uume ilitupatia utambuzi muhimu juu ya umuhimu wa dhakari kama kielelezo cha mamlaka ya mwanamume juu ya mwanamke. Aidha, ni sehemu muhimu iliyojenga umaizi wetu katika kutambua jinsi ambavyo kiungo hiki cha uzazi hutumiwa na jinsia ya kiume katika kudhihirisha thamani za kimaumbile, kiishara na za kisaikolojia ambazo huambatanishwa nacho kama kifaa mwafaka cha mamlaka na uwezo katika jamii. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi tutajikita katika nafasi ya lugha katika kujenga na kuhahalisha mahusiano ya kiuwezo katika jamii mintarafu ya jinsia. Kulingana na Wodak (2001b:111):

> Uwezo ni juu ya mahusiano katika utofauti na hasa zaidi juu ya athari ya utofauti huu katika miundo ya jamii. Ulinganifu wa lugha na maswala mengine ya kijamii huhakikisha kuhusishwa kwa lugha na uwezo katika jamii kwa njia mbalimbali. Lugha ni kielelezo cha uwezo, hudhihirisha uhusiano huu palipo na ukinzani juu ya uwezo katika jamii. Uwezo hautokani na lugha bali lugha huweza kutumika kuthibitisha uwezo, kuchochea na kubadili mgawanyo wa uwezo kwa wakati mfupi au baada ya muda mrefu. Lugha hueleza kwa uwazi njia tofauti za uwezo katika mfumo wa utawala msonge katika jamii. Hivyo basi, Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi hubainisha kwa uwazi jinsi viambajengo vya lugha huunda na kudhihirisha ngazi za uwezo katika jamii. Uwezo huu haudhihirishwi kupitia kwa mfumo wa sarufi katika matini au usemi, lakini hata hivyo mamlaka ya mwanajamii katika nyakati maalum hudhihirika katika tanzu mbalimbali za matini.

2.4.1 Nadharia ya uchanganuzi hakiki wa usemi

Schiffrin (1987:1) anafafanua uchanganuzi usemi kama jaribio la kuchunguza mpangilio wa vipashio vya lugha ambavyo ni vikubwa kuliko sentensi na kirai. Anaendelea kusema kuwa uchanganuzi usemi hushughulika na matumizi ya lugha katika miktadha ya kijamii.

Brown na Yule (1993:1) wanasema uchanganuzi usemi ni uchanganuzi wa lugha katika uamilifu wake; hivyo basi uchanganuzi huu hauwezi kuwekewa mipaka ya kiisimu. Kutokana na kijelezi hiki, ni sharti ichunguzwe kwa misingi ya matumizi yake katika miktadha mbalimbali kutegemea watumiaji wake.

Nadharia hii ilibuniwa miaka ya sabini baada ya utambuzi wa majukumu ya lugha katika kuratibu uwezo na mamlaka miongoni mwa wanajamii.Kabla ya miaka ya sabini, tafiti nyingi za kiisimu zilijihusisha na swala la umilisi lugha, swala ambalo halikubainisha matumizi ya lugha. Katika kipindi hiki, uhusiano baina ya lugha na muktadha uliangazwa chini ya kitengo cha pragmatiki.

Kuanzia miaka ya tisini, Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi ilishika moto. Kress (1985: 94) alibainisha jinsi ambavyo nadharia hii ilikuwa ya kipekee ya kuchanganua lugha. Aliorodhesha maksio mahsusi ambayo yametokea kuwa msingi wa nadharia hii.

a) Lugha ni swala la kijamii
b) Makundi ya jamii, taasisi za jamii na kila mwanajamii huwa na maana halisi na thamani ambazo hubainishwa kupitia kwa lugha katika utaratibu mahsusi
c) Matini na usemi ni viambajengo mwafaka vya lugha katika mawasiliano.
d) Kuna uhusiano baina ya lugha ya kisayansi na lugha ya kijamii.

Kutokana na maksio haya inabainika bayana kuwa uamilifu wa lugha sio tu wa mawasiliano, bali lugha huhodhi itikadi, mielekeo na matarajio ya watumizi wake.

Fowler (1991) anaonyesha jinsi viambajengo vya lugha vinavyotokana na nadharia wastani za kiisimu za Chomsky (1965) ya sarufi na nadharia ya Halliday (1970) ya utaratibu wa uamilifu wa sarufi. Viambajengo hivi vinaweza kutumika kubainisha miundo ya kiisimu ya mamlaka katika usemi na matini. Fowler anaonyesha jinsi ambavyo utaratibu wa usemi unavyoweza kuasisi, kuendesha au kuhalalisha ngazi za mamlaka katika jamii.

Fairclough (1989, 1991) anabainisha mikakati maalum ya uchanganuzi wa lugha mintarafu ya mahusiano na uwezo, itikadi na mabadiliko ya jamii na utamaduni. Utafiti wake ulizingatia vyombo vya habari.

Wodak (1996) anaonyesha wasomi wa uchanganuzi usemi wenye asili tofauti jinsi wana mtazamo sawa kuhusu dhana ya mamlaka, itikadi na historia ya jamii. Anaunga mkono mapendekezo ya wasomi hawa kuwa uhusiano kati ya lugha na jamii ni changamano, anapendekeza utafiti wenye kuhusisha masomo mbalimbali.

Msingi wa nadharia hii ni kuwa lugha yenyewe haina uwezo wala mamlaka. Bali hupata uwezo huu kutokana na wanajamii wenye kumiliki uwezo katika jamii. Hii ndiyo sababu nadharia ya uchanganuzi hakiki wa usemi huchagua mtazamo wa wale wanaoteswa na kuchanganua kwa kina matumizi ya lugha ya wale wenye uwezo na mamlaka ambao wamewajibika katika kuendeleza hali ya kutokuwa na usawa katika jamii. Aidha, ndio wanaomiliki njia na nafasi ya kustawisha hali nzuri ya usawa katika jamii.

Wodak (1996) anashikilia kuwa lugha ni tendo la jamii na anasisitiza umuhimu wa muktadha wa matumizi ya lugha. Aidha, ni muhali usemi kuwa zao la mtu mmoja. Usemi huongozwa na tofauti za kimamlaka ambazo ni sehemu ya jamii.

Usemi na matini ni sehemu ya mapambano ya kubainisha tofauti katika itikadi, mamlaka na uwezo unaobainisha mvutano wa kiutawala baina ya jinsia ya kiume na ya kike. Sifa muhimu ya nadharia hii ni kule kujihusisha na uwezo/mamlaka kama kitovu cha maisha ya jamii.

Uwezo, itikadi, majukumu na mamlaka ni maswala yanayobainisha mahusiano na utofauti na hasa zaidi athari ya tofauti hizi katika mfumo wa jamii. Lugha husheheni uwezo katika itikadi, hubainisha uwezo na itikadi hizi na huwa kichocheo cha kudhihirisha na kutathmini mamlaka katika jamii.

Nadharia hii hujihusisha na jinsi ambavyo wanajamii hupata na kuendeleza uwezo na mamlaka katika jamii yao, hubainisha utendakazi wa itikadi katika taasisi za kijamii na vilevile huonyesha jinsi ambavyo usemi huundwa na kuongoza mielekeo na matarajio ya wanajamii.

Wodak na Van Dijk (2000) wanasema kuwa Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi huzingatia matatizo mbalimbali ya kijamii. Kwa kufanya hivyo, huchanganua mtazamo wa wale ambao hutwezwa na kuchanganua vipengele mbalimbali vya lugha vinavyotumika katika kuhalalisha ngazi za kiutawala, na kulinganisha na wale wanaohodhi uwezo, njia na nafasi ya kusuluhisha matatizo haya.

Nadharia hii hujihusisha na uchanganuzi wa miundo ya mahusiano ya wanajamii wenye mamlaka, waliotengwa na wenye kumiliki nyenzo za uzalishaji mali, na kuonyesha jinsi ambavyo miundo hii inavyojitokeza kupitia kwa lugha inayotumiwa. Hivyo, nadharia hii ilikuwa mwongozo thabiti wa kutuwezesha kuchanganua mpangalio wa kijamii na jinsi ambavyo jamii imeratibu ngazi za mamlaka na majukumu kiuana kupitia kwa lugha katika nyiso za jando. Kipengele hiki kilituwezesha kuchanganua iwapo mwanamume katika jamii ya Abakuria hujitokeza kama jinsia yenye mamlaka. Hii ni kwa sababu lugha ni njia ya kubainisha mamlaka

na nguvu za kijamii. Hutumika vile vile kuhalalisha utaratibu wa umilikaji wa uwezo mintarafu ya uana.

Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi ilituwezesha katika kubainisha muundo wa mahusiano ya kiuwezo katika nyiso za jando na kubainisha bayana itikadi zinazotawala mahusiano ya kijamii. Nadharia hii ni uti wa mgongo katika kubainisha wazi ruwaza ya mahusiano ya kiuwezo.

Uwezo wa usemi hujengeka kupitia kwa nafasi ambayo hupewa, kufasiri, kueleza na kuweka mipaka kwa kile ambacho husemwa na kutosemwa na ikizidi kile kinachoweza kutenda na ambacho hakina uwezo huo (Kress, 1985).

Uchanganuzi usemi hutambua umuhimu wa matumizi ya lugha katika miktadha ya jamii na hubainisha wazi utendakazi wa itikadi zinazowakilishwa kupitia kwa lugha (Fowler 1991:5). Kama mtazamo fafanuzi, nadharia hii hulenga sio tu kwa matumizi halisi ya lugha bali kama utaratibu wa utangamano wa kijamii kwa hali na muktadha mahususi. Aidha, ni taratibu zinazobainisha kategoria za kijamii kwa misingi ya mahusiano yao. Ni muhimu kutaja kuwa desturi za kijamii na mahusiano ya wanajamii huundwa kutokana na raghba ya mtazamo na dhana mahsusi mintarafu ya uhalisi wa kijamii (Deacon, Pickering na wengine 1999).

Nadharia hii imejengeka kwa dhana nne muhimu, uwezo/mamlaka, historia, muktadha na itikadi. Hivyo basi kila usemi katika lugha husika hubainisha historia na mielekeo ya jamii, hii ni kwa sababu usemi huwa na maana katika kipindi fulani cha kihistoria na katika muktadha mahsusi. Usemi huo huhalalishwa na itikadi za jamii hasa na kundi la jamii lenye kumiliki mamlaka katika jamii. Katika utafiti wetu tulitumia vigezo hivi katika kudhihirisha sura ya mwanamume inayojitokeza. Misingi ya nadharia hii ni mihimili ya kutosha katika kubainisha uhusiano uliopo kati ya matumizi ya lugha na muundo wa jamii, hasa zaidi kuhusu ngazi za kiuwezo. Nadharia hii itakuwa mwongozo mwafaka katika uchanganuzi wa nyiso za jando katika kutimiza malengo ya utafiti huu.

Nadharia hii ilituongoza katika uchanganuzi wa data, ili kubainisha nafasi ya lugha katika kujenga na kuhifadhi mahusiano ya kiuwezo baina ya wanajamii katika jamii ya Abakuria. Aidha, ilikuwa mwongozo wa kutathimini maana na thamani za kijamii ambazo hubainishwa kupitia kwa lugha ya nyiso. Ili kufanikisha azma hii, taashira na tamathali za lugha zilichanganuliwa katika kubainisha jinsi jamii imeratibu ngazi za mamlaka na majukumu kupitia kwa lugha. Kwa upande mwingine nadharia hii haizingatii nafasi ya utamaduni, mielekeo,

matarajio na itikadi za kijamii katika ujenzi wa Uwezo-uume. Hali hii ilizua uhitaji wa nadharia ya Uwezo-uume. Nadharia hii ilituwezesha kubainisha taswira ya mwanamume wa Abakuria kwa misingi ya utamaduni, mielekeo, matarajio na itikadi za jamii ya Abakuria.

2.4.2 Nadharia ya Uwezo-uume

Utafiti huu vilevile, utaongozwa na nadharia ya uwezo-uume, mtazamo huu hubainisha nguvu na mamlaka yanayomilikiwa na jinsia ya kiume, hasa kutokana na utamaduni wa jamii husika. Dhana 'mwanamume' ipo kwa misingi ya kibaolojia ilihali 'Uume' hutokana na mielekeo, imani na matarajio ya utamaduni wa jamii. Hivyo basi uume huzaliwa na kukuzwa na utamaduni, na huhalalishwa kwa njia, hali na nyakati tofauti za jamii nzima.

Imebainika kwamba sura ya mwanaume na mvulana katika jamii haitokani na ombwe tupu au wanavyojifikiria wanaume bali sura hizo hujengwa kutokana na matarajio ya kiitikadi na kitamaduni kuwahusu. Ni kutokana na matarajio haya ambapo baadhi ya sifa husisitizwa. Kwa mfano, stahamala, ubabe na ukatili katika kutenda bila kujali iwapo vitendo hivyo vitaleta maangamizi au vurugu katika jamii.

Uume hubainika bayana kwa misingi ya uhuru, wa kijinsia, ushari, ushindani na uwezo wa kutawala, kuamuru na kuzuia (Walsh, 1997). Katika jamii za kiafrika uume huhusishwa na uwezo wa mwanamume kuwa na mafanikio kukimu na kutosheleza mahitaji ya familia. Aidha, mwanamume hazaliwi na uume kama sehemu ya viungo vyake vya uzazi bali hujengwa na kukuzwa na utamaduni anamokulia.

2.4.3 Chimbuko la Nadharia ya Uwezo-uume

Asili ya nadharia hufungamanishwa na *dhakari* na wenye kuimiliki (wanaume). Wanachukuliwa kuwa na nguvu, wenye kuheshimiwa na kustahibiwa katika jamii. Binadamu anayezaliwa na kiungo hiki hujamiishwa katika jamii kama raslimali yenye manufaa makubwa kwa jamii. Hivyo basi siku zote mwenye dhakari hupewa hadhi ya juu na huchukuliwa kuwa bora zaidi ya wale ambao hawana kiungo hiki (wanawake) Izugbara (2005:13).

Izugbara (2005:13) anasema:

> Umbo la dhakari la ubenuzi na hali ya kutokuwa na haya ikishirikishwa na uwezo wa dhakari kuwa ngumu, kubwa, thabiti na yenye nguvu wakati wa

mchechemo ni dhihirisho kwa mawazo asili kuwa dhakari ina uwezo! ... shahawa ambayo inatoa kipindi cha tendo la ngono huonekana kama sumu ambayo humdhoofisha mwanamke... (tafsiri hii ni yangu na zitakazofuata).

Izugbara, anaendelea kusema kuwa dhakari imetawazwa na umuhimu wa uhai na ufu... matokeo muhimu huhuzishwa na amali ya dhakari na upenyezi wake katika kupoteza ubikra na kutia mimba, hali hii huitawaza dhakari uwezo juu ya uhai na ufu...

Itikadi za kitamaduni ambazo hubainisha aula, uwezo, nguvu, uhodari na uhayawani wa mwanaume, kielelezo chake cha mamlaka, utendakazi wa viungo vya uzazi, upenyezi wa dhakari, kuwa na uhusiano wa kingono na zaidi ya mwanamke mmoja nje ya ndoa, ushari wa kimapenzi, sauti nzito miongoni mwa sifa zingine, huchukuliwa kama sifa mwafaka zenye kumtambulisha mwanamume tofauti na wasiomiliki dhakari.

Izugbara (2005) anaendelea kusema kuwa dhakari hutumika kama chombo cha kumzusha hadhi mwanamke. Kwa sababu hii dhakari ni asili ya "uanaume" silaha ya kumwezesha mwanamume kuwa mshindi katika ushindani wa kijinsia. Maana yake na umuhimu wake huhalalishwa katika tendo la ngono na sifa zake muhimu zenye kuakisi matarajio ya jamii juu ya mwanamume. Aidha ni kiungo cha kibaolojia ambacho ni kielelezo muhimu cha thamani katika ujamiishaji wa wanaume katika jamii.

Katika kuzaliwa kwa mtoto, watu huangalia kwa makini kuwepo au kutokuwepo kwa dhakari. Swala ambalo hukolea katika fikra za kitamaduni za wanajamii kama dalili ya uwezo. Kuwepo kwa kiungo hiki cha mwili huwafanya wanajamii kuwaweka watoto wa kiume katika kategoria mahususi mintarafu ya mtazamo wa utamaduni wa jamii husika. Wale ambao hukosa kiungo hiki hujamiishwa kwa njia tofauti yenye kuafiki nafasi yao katika jamii (Izugbara 2005: 14).

Kuwepo au kutokuwepo kwa kiungo hiki cha kibaolojia huchukua nafasi muhimu ya utamaduni na mtazamo wa kijamii kuhusu matarajio juu ya hizi jinsia mbili. Wanasosholojia hukubaliana na msingi huu wa nadharia hii katika kumpa mwanaume uwezo anaoumiliki katika jamii.

Utambuzi wa uume na uke hujengwa katika miaka ya awali ya mtoto. Takribani umri wa miaka miwili watoto huanza kuelewa utambulisho wao wa kijinsia. Hivyo basi kadri watoto

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

hawa wanavyokua huanza kuepuka matendo na shughuli ambazo huaminiwa kutoafikiana na jinsia yao.

Mahusiano ya kiuwezo ya kijinsia yameacha hiba kwa ambavyo wanaume humiliki uwezo mkubwa katika raslimali za jamii, fadhila na katika kuamua juu ya masuala muhimu ya kijamii. Aidha mwanamume huwa na haki zaidi ya mwanamke katika nyumba na masuala mengine ya umma. Uume hukuzwa na kuendelezwa na utamaduni wa jamii na huwa sehemu ya asasi ya jamii hiyo. Hivyo basi, nadharia hii huchukulia utamaduni kama uti wa mgongo wa misingi yake. Wao hawazingatii maswala ya kibaolojia na kianthropolojia ambayo hushilikilia mtazamo kwamba tabia za kiume ni uhalisia wa maisha ya jamii. Tofauti za kibaolojia kati ya mume na mke hazitoshelezi kumfanya mwanamume kuwa na uwezo mkubwa, mkware, mpakaji, mwenye mamlaka yaliokithiri na muuaji. Bali utamaduni na mazingira anamokulia huwa na mchango mkubwa.

Richmond (1992) anasisitiza kuwa jamii ni taasisi muhimu ambayo hujenga na kuratibu majukumu na shughuli za kijamii kiuana. Swala la ujamiishaji huendelea kadri mwanajamii anavyokua kutoka utotoni hadi utu-uzima. Hivyo, kila jamii huwa na jinsi maalum ya kuanzisha na kuendeleza ujamiishaji kwa wanajamii wake. Marie, vilevile, anaangaza jinsi majukumu ya kiuana hufungamanishwa na tofauti za kibaolojia, uwezo na hadhi, anaendelea kusema kuwa majukumu ya kijinsia yamo ndani ya historia ya kitamaduni na hutiliwa mkazo na taasisi mbalimbali za jamii husika.

Nadharia ya uwezo uume hufafanua sifa mahsusi anazostahili kuwa nazo mwanamume (Kimmel 1997). Nadharia hii hujengeka mintarafu ya uwezo na mafanikio, uwezo wa kijinsia ambao huweza kufafanuliwa na kubainishwa kwa njia tofauti, ni kipengele muhimu cha mtazamo wa nguvu za jinsia ya kiume. Nadharia hii hudhihirisha jinsi ambavyo mwanamume hupanda ngazi, kiutawala, kufikia ukamilifu na kuendeleza nafasi yake katika jamii. Haya yote huhalalishwa kupitia kwa itikadi na utamaduni wa jamii.

Hanke (1998) anaonyesha jinsi ambavyo runinga huchangia kupitia kwa picha na simulizi katika kukuza uwezo-uume. Naye Fiske (1987) anaangaza masimulizi ya matukio hatari, ushari wa vitendo na mashindano sambamba na wanasesere wa kiume. Tafiti hizi zote zimebainisha jinsi ambavyo utamaduni na mazingira huwa vigezo muhimu katika kukuza uwezo-uume ambao hukolea katika fahamu za wanajamii. Hali hii huathiri kwa njia moja au nyingine mahusiano ya mwanamume na mwanamke katika jamii.

Maclenness (1998) alibainisha jinsi ambavyo masharti ya kihistoria na ya kitamaduni yanavyohalalisha miekekeo na mitazamo tofauti baina ya jinsia ya kike na ya kiume. Anaeleza kuwa uume hauwezi kubainishwa kama sifa ya mwanaume bali hutokana na itikadi na utamaduni wa jamii husika. Masharti mahsusi ya kihistoria yanayothibiti imani za mume na mke katika jamii na majukumu yao tofauti huendelezwa kupitia kwa imani za kijamii, matarajio na mielekeo yao.

Kwa mujibu wa utafiti wa Uchendu (2005) uume miongoni mwa vijana wa kiume huhusishwa na sifa za kimaumbile, kijamii na za kisaikolojia. Kimaumbile wavulana hutamani kuwa na sauti nzito, nywele fupi, njia ya kipekee ya kuvaa, kuwa huru, kifua pana na ishara za uso za kutisha miongoni mwa sifa zingine. Kisaikolojia wanaume hutamani kuogopwa, kuwa na mamlaka ya uamuzi, kuwalinda wanyonge, kuwa na msimamo thabiti, kuwa wenye amri, kuwa na hadhi ya juu katika jamii, mwenye akili na hekima ya kuthaminiwa, kuthubutu na kutoonyesha mhemko.

Ni kutokana na usuli huu ambapo nadharia hii hufafanua uelewa wa wavulana na wanaume juu ya jinsi wanavyopaswa kutenda ili kukubalika kama wanaume katika jamii. Mwanaume huhusishwa na Madaraka ya juu, uwezo thabiti, mshindani na mwenye uwezo wa kuhudumia wanawake wengi wa halali na wa nje ya ndoa (Frosh wa wengine 2004:76).

Kwa muhtsari nadharia hii imejikita katika mambo manne muhimu ambayo hutawala matarajio na mielekeo ya jamii kuhusu mwanamume, nayo ni: itikadi za jamii, uwezo, mamlaka, utamaduni na mazingira. Hivyo basi, nadharia hii ilikuwa mwongozo thabiti katika kutathmini na kuitolea kauli sura mwafaka ya mwanamume wa Abakuria kupitia kwa nyiso za jando. Nadharia hii hutambua umuhimu wa utamaduni, mielekeo na mitazamo ya kijamii katika kuhalalisha uwezo anaomiliki mwanamume katika jamii. Nadharia hii ilituongoza katika kudhihirisha taswira ya mwanamume wa Abakuria kwa misingi ya utamaduni, itikadi, mielekeo na matarajio ya jamii. Utanzu wa nyiso za jando umejaa taasubi za kiume ambazo hudhihirishwa na tamathali za usemi. Taasubi hizi zimejikita kwenye itikadi, mazingira, utamaduni, mielekeo na matarajio ya jamii kumhusu mwanamume.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inajadili mbinu za utafiti ambazo zilitumika katika ukusanyaji wa data, aidha, inabainisha njia mwafaka zilizotumika katika uchanganuzi wa data ili kujibu maswali ya utafiti. Hayo yote yalitekelezwa kwa misingi na mwongozo wa mada ya utafiti, madhumuni ya utafiti na misingi na ya nadharia tukizozitumia

Utafiti huu ulifanyika kwa awamu mbili, awamu ya kwanza ilihusisha ukusanyaji wa nyiso za jando hasa zile zinazamrejelea mwanamume. Awamu ya pili ilishusisha uchanganuzi wa data ili kubainisha taswira ya mwanaume inavyojengwa na kujitokeza katika nyiso za jando.

3.2 Eneo/Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ulifanyiwa katika wilaya ya kuria tarafa ya Ntimaru. Abakuria wamegawika katika takribani koo kumi na moja. Utafiti huu ulilenga nyiso za jando miongoni mwa ukoo wa Abairege, mojawapo ya koo za Abakuria. Abairege wanaishi katika tarafa ya Ntimaru nchini Kenya na tarafa ya Nyamwanga nchini Tanzania. Kwa mujibu wa utafiti huu ni muhimu kutaja kuwa jamii ya Abakuria ni ya kuumeni, hivi kwamba mwanamume hujitokeza kuwa mwenye uwezo takribani katika muswala yote ya kijamii.

3.3 Ukusanyaji wa Data

Kusudi kubwa katika awamu hii lilikuwa kukusanya nyiso za jando hasa zile zinazobainisha taswira ya mwanamume mintarafu ya matarajio, mielekeo, itikadi, mitazamo na majukumu yake katika jamii. Nyiso hizi ndizo data ya msingi ya utafiti huu. Vilevile, tulikusanya yale yote ambayo hutoa ujumbe wowote kuhusu sura ya mwanamume katika jamii ya Abakuria kupitia kwa mahojiano ya ana kwa ana na wasaili wetu tuliowateua kwa misingi ya umri na tajriba yao kuhusu nyiso za jando, historia, fasihi na utamaduni wa jamii ya Abakuria kwa jumla.

3.3.1 Njia za Ukusanyaji wa Data

Nyiso za jando miongoni mwa jamii ya Abakuria hazijatiwa kwenye maandishi zipo tu kwenye bongo za wanajamii na zingine zimerekodiwa kwenye kanda za redio.
Kwa mujibu wa ukweli huu tutatumia mbinu za mahojiano ya ana kwa ana, uchunguzi-shiriki na matumizi ya kanda na kinasa-sauti.

3.3.2 Matumizi ya Kanda/Kaseti na Kinasa-sauti

Baadhi ya nyiso zilipatikana kutoka kwa kanda/ kaseti ambazo tulizipata kutoka kwa baadhi ya wanajamii ambao wamezirekodi nyiso hizo. Awamu ya kwanza ilikuwa kuziweka nyiso hizo katika maadishi katika lugha ya kikuria, hili liliwezekana kwa sababu mtafiti ana uelewa mpana wa lugha hii kwani ndiyo lugha yake ya kwanza. Hatimaye nyiso hizo zilitafsiriwa kwa kiswahili kwa kutumia tafsiri huru(tafsiri ya neno kwa neno) na tafsiri maana. Kwa kuzingatia mada ya utafiti na madhumuni ya utafiti tuliratibu nyiso hizo kwa ambavyo tuliorodhesha nyiso zile zinazolenga kujibu maswali yetu ya utafiti chini ya mwongozo wa misingi ya nadharia zetu za utafiti.

3.3.3 Mahojiano ya Ana kwa ana

Mtafiti alitumia jumla ya wasailiwa kumi na watano wenyeji asili na wazungumzaji wa lugha ya kikuria wenye umri kati ya miaka kumi na tano na tisini. Wasailiwa hawa waliwekwa katika makundi mawili kutegemea umri. Kundi la kwanza lilijumlisha wasailiwa wa umri kati ya miaka 28 na 90, kundi hili lilikuwa mwafaka kutusaidia kupata; historia, utamaduni, mielekeo na mitazamo ya jamii ya Abakuria kumhusu mwanamume. Kundi la pili lilijumlisha vijana wa kiume wa kati ya miaka 15 na 18, hawa ni wale waliotahiriwa miaka ya 2004 na 2005. Kundi hili lilikuwa na kumbukumbu mwafaka kuhusu nyiso za jando. Aidha, wote walikuwa wanafunzi wa shule ya upili, hivyo basi, walikuwa na uwezo wa kuziandika nyiso walizozikumbuka kwa lugha ya kikuria. Hata hivyo,makundi haya yote yalikuwa na uelewa na tajriba mwafaka kuhusu nyiso za jando ambazo zinamrejelea mwanamume.

Data nyingine tulioikusaya kwa kutumia mbinu ya mahojiano na mijadala huru ya ana kwa ana na baadhi ya wasaili wetu wa kundi la kwanza ilihusu maelezo ya jumla juu ya historia simulizi ya Abakuria, shughuli zao za kimaisha, tohara na umuhimu wake, maoni, mitazamo, itikadi, mielekeo, mila na desturi zao na imani za jamii kumhusu mwanaume. Data hii ni

malighafi mwafaka katika utungaji wa nyiso za jando na umuhimu wake ulibainika bayana katika uchanganuzi wa deta.

3.3.4 Uchunguzi-shiriki

Tarehe 19/12/2005,mtafiti alishiriki sherehe za tohara katika kijiji cha Gitungi iliyofanyiwa katika boma la Mogosi Mang'ara. Aidha, tarehe 21/12/2005 mtafiti alishiriki sherehe nyingine katika kijiji cha Rewankwe katika boma la Marwa Waikanga. Katika sherehe hizi mtafiti aliweza kurekodi baadhi ya nyiso kwa kutumia kinasa-sauti, hatimaye alizinakili kwa maandishi katika lugha ya kikuria na baadaye kustafsiri kwa Kiswahili. Hivyo basi, kwa sababu utafiti huu ulifanywa katika kipindi ambacho Abairege walikuwa na sherehe za tohara, mbinu ya uchunguzi-shiriki ilitumiwa katika ukusanyaji wa nyiso za jando, mbinu hii ilikuwa mwafaka katika kubainisha muktadha mahususi wa matumizi ya nyiso za jando. Hii iliwezekana kwa sababu mtafiti ni mojawapo ya wanajamii ambaye amewahi kuhudhuria na kushiriki sherehe hizi za tohara na jando, hivyo basi, ana uelewe mwafaka juu ya nyiso za jando na sherehe za tohara kwa jumla. Uelewa wake ulikuwa mchango mkubwa katika matumizi ya mbinu hii ya uchunguzi- shiriki.

3.4 Uchanganuzi wa Data

Jumla ya nyiso isitini zilikusanywa na kutiwa kwenye maandishi kwa lugha ya Kikuria na tafsiri yake kwa lugha ya Kiswahili. Tulitumia tafsiri ya neno kwa neno(tafsiri huru) na tafsiri maana. Katika tafsiri ya neno kwa neno tulizingatia muundo wa lugha asilia wa neno kwa neno. Tafsiri maana ilitumiwa pale ambapo tafsiri huru ilishindwa kubainisha maana kamili.

Kwa mujibu wa malengo ya utafit huu na muda, ilikuwa muhimu kuteua nyiso zipatazo ishirini na nne kwa minajili ya uchanganuzi ili kubainisha taswira ya mwanamume wa Abakuria. Kutokana na jumla ya nyiso tulizozikusanya inabainika kuwa nyiso zina 'ubeti' mmoja wenye mistari miwili hadi kumi na miwili. Nyiso hizi huwa hazina kibwagizo wala mada kuu. Nyiso hizi huundwa kwa uteuzi wa maneno yaliyo na mnato na kupangwa kwa jinsi ambavyo hubainisha mapigo maalum ya kuwezesha kuimbika kwake.

Urejeleo wa uchanganuzi wetu ulikuwa mwanamume. Katika nyiso tulizozichanganua mwanamume alirejelewa kama; 'taata'(baba), 'sokoro'(babu), 'mame'(mjomba), 'abamura/abakare'(vijana wa kiume/mashujaa) na mtahiriwa.

Katika uchanganuzi wa data, tulijikita katika viambajengo vya lugha iliyotumiwa katika nyiso tulizoziteua kwa minajili ya uchanganuzi katika muktadha maalum wa jando. Tulizingatia na kuhakiki taashira na tamathali za usemi zilizotumiwa katika nyiso hizo kumsawiri mwanamume na kumweka mahali pake katika jamii, kutegemea misingi ya itikadi za Abakuria. Katika kiwango hiki Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi ilikuwa mwongozo wa kutathimini jinsi lugha katika nyiso za jando hujenga na kuhalalisha uwezo na mamlaka ya mwanamume katika jamii ya Abakuria ndani ya muktadha wa tohara. Ili kubainisha taswira ya mwanaume katika nyiso tulijikita katika kuhakiki thamani na mantiki ya yaliyomo katika nyiso tulizoziteua kwa minajili ya uchanganuzi. Azma ilikuwa, kubainisha uwezo na itikadi za jamii ya Abakuria katika kuratibu ngazi za kiuwezo na mamlaka ya mwanamume kupitia kwa lugha katika nyiso. Tulizingatia tashibihi, istiara, jazanda na taswira kama mojawapo ya tamathali za lugha jinsi zilivyobainisha makisio ya utafiti wetu, tuliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi. Tulihuzisha tamathali hizi na maana za kisemantiki na maelezo yalilenga madhumuni ya utafiti.

Aidha, katika uchanganuzi huu, tulizingatia umuhimu wa utamaduni, mielekeo na mitazamo ya jamii ya Abakuria katika kujenga na kuhalalisha uwezo anaomiliki mwanamume. Msisitizo hapa ulikuwa ujenzi wa uume. Nadharia ya Uwezo-uume ilituongoza katika uchanganuzi wa nyiso hizi ili kutimiza azma hii. Nadharia hii ilituwezesha kutathmini ujenzi wa itikadi, Uwezo-uume, mitazamo na mikakati ya kumsawiri mwanaume. Kutokana na tamathali za lugha katka nyiso za jando ambazo hubainisha matarajio ya kiitikadi katika kusisitiza sifa za kiume kwa mfano; ubabe, ushari na ukatili.

Uhakiki na uchanganuzi wa nyiso uliendelezwa kwa kuzingatia dhamira, maudhui na fani chini ya madhumuni ya utafiti na misingi ya Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi na ile ya Uwezo-uume. Kwa mujibu wa nadharia hizi sehemu zifuatazo ziliangazwa katika kufanikisha utafiti huu.

- Ujenzi wa itikadi na uwezo uume.
- Taashira na tamathali za usemi
- Thamani ya mantiki na yaliyomo katika nyiso za jando.
- Sifa na majukumu ya mwanamume.
- Mitazamo na mikakati ya kumsawiri mwanamume.
- Urejeleo – mwanamume.

Matokeo ya uchanganuzi huu yalitumika katika kutoa muhtasari wa jarabati za matokeo ya utafiti huu.

3.5 Hitimisho

Sura hii imebainisha mbinu za utafiti zilizotumiwa katika kukusanya data, kutafsiri, kufasili na kuichananua. Uchanganuzi wa data uliongozwa na maneno ya utafiti na nadharia za utafiti.

SURA YA NNE

ASILI, HISTORIA NA UTAMADUNI WA ABAKURIA

4.1 Utangulizi

Katika sura hii tumejadili asili na historia ya Abakuria na mahali wanakoishi hivi leo. Mkondo wa historia-simulizi umetumiwa. Kama jamii bainifu ina fasihi yake inayotuwaliwa na jadi na kaida za kijamii ambazo zinabainisha mahusiano ya wanajamii kwa misingi ya uana na umri. Hivyo basi katika sura hii mmejadiliwa jadi na kaida za jamii kumhusu kila mwanajamii katika awamu mbalimbali za maisha yake; hii ni kwa sababu kila awamu ina matarajio, majukumu na haki zake. Aidha, katika sura hii mmejadiliwa mifumo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kidini inavyojitokeza katika jamii ya Abakuria na jinsi mifumo hii inavyobainisha mahusiano ya wanajamii katika maisha yao ya kila siku. Jambo linalodhihirika ni kwamba historia, utamaduni na ada mbalimbali za kijamii ni maswala ambayo yana uhusiano mkubwa na chimbuko la baadhi ya mahitaji, matarajio, mila na desturi za jamii. Itikadi na mielekeo na jinsi haya yote huongoza mahusiano ya wanajamii na hasa zaidi jinsi ambavyo kila jinsia inavyopaswa kuishi katika jamii katika kutekeleza majukumu yanayohusiana na jinsia yao; yote haya yamejadiliwa katika sura hii.

> Historia na utamaduni wa jamii mahususi ni nguzo mwafaka ya kuwezesha uelezaji wa tanzu mbalimbali za fasihi simulizi na jamii husika. Maswala haya ni muhimu kwa sababu yanachangia katika kuzalisha na kuendeleza falsafa na mitazamo mbalimbali ya jamii fulani, kwa sababu hii, utanzu wa fasihi simulizi (ambao ni zao la jamii) husaidia katika kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii (Okindo A. 1995: 48)

4.2 Historia – simulizi ya Uzao wa Abakuria kutoka kwa "Monto"

Kutokana na simulizi nyingi zinavyoeleza usuli wa jamii ya Abakuria, inajitokeza bayana kuwa Abakuria ni uzao wa familia ya *Monto* ambaye ni mzazi wa Wabantu wote. Kwa kuzingatia jamii zinazounda kabila la Abakuria ambao ni wabantu wenye asili ya "Monto" uzao wao ulipatikana kama ifuatavyo (kwa mujibu wa mzee Matiko, 2006).

4.2.1 Uzao wa Abakuria

Monto alimzaa Range pamoja na wengine. Naye Range akamzaa Mugaiwa na wengine. Magaiwa ndiye aliyemzaa Mkuria ambaye aliwazaa vijana watano, Nyanchage, Wangwe, Mongoso, Nano na Mendi. Nyanchage aliwazaa; Mtimbaru, Mosi na Mosonga; hawa ndio jamii ya Abakuria wanaojiita Pundamilia, ambao hadi leo wapo kwenye makundi Matatu: Abanyabasi, Abatimbaru na Ababwasi (Abuso 1980: 145). Abanyabasi hupatikana pande zote mbili za Kenya na Tanzania ilhali Watimbaru na Ababwasi wapo Tanzania pekee.

Wangwe aliwazaa; Moracha, Mwirege, Keroba, Mugumbe na Gisiri. Hawa ndio jamii ya Wakuria wanajulikana kama "Engwe"; yaani mnyama chui, ingawa mara nyingi hujiita 'Kemoramba ya gesaka' (shujaa wa mwituni). Baada ya miaka mingi, kadri koo zilivyoendelea kupanuka, ukoo wa Moracha ulibadilika na kuitwa "Abanyamongo" ikiwa na maana ya "wenye akiba ya chakula". Pia ukoo wa Mugumbe ulibadilisha jina na wakajiita "Abarenchoka" kutokana na kuishi kwenye eneo lililoaminika kuwa na nyoka wengi. Abuso anaainisha koo tatu za jamii hii ya chui, nazo ni; Abagumbe, Abairege na Abanyamongo. Abairege ambao ndiyo jumuiya ya utafiti huu, hadi leo hujitambulisha kwa urejeleo wa mnyama chui. Utambulisho huu hujikita katika imani za ushujaa na ushari wao katika kuwashambulia maadui wao. Hali hii ni ithibati ya kimsingi jinsi ambavyo historia ya Abakuria imechangia katika kujenga na kukuza Uwezo-uume.

Mongoso alimzaa Mukira ambaye alikuwa mtoto wake wa pekee, na yeye ndiye asili ya jamii ya Abakuria wajulikanao kama Abakiira. Mongoso ni jina lenye maana ya Tembo dume; maana ya Nyangoso ni Tembo jike na ndio maana ukoo wa Abakiira hurejelewa kwa jina la mnyama Inchugu (Tembo) au Nyabironge lenye maana sawa na Tembo (Mzee Matiko, 2006).

Nano aliwazaa Mokenye, Musweta na Mosembete. Hawa ndio jamii ya Abakuria inayoitwa Inano yenye maana ya mnyama "Nyani". Kutokana na hawa, jamii ndogo ndogo ziliibuka kama; Abakine, Abarieri, Abamera na Abahancha ambao kwa sasa wanaishi mwambao wa ziwa Viktoria kati ya mto Mara na Migori.

Mendi naye alimzaa Munchari pekee na ndiye asili ya jamii ya Abanchari. Mendi ni jina la mnyama mdogo jamii ya panya ambaye huishi mahali penye nyasi; Abakuria humwita "Irigeki". Abuso anarejelea jamii hii ya Abanchari kwa kuihusisha na mnyama kiboko. Urejeleo huu unatokana na hali ya jamii hii kuishi kando ya ziwa Viktoria na kandokando ya mto Mara.

Huo ndio mwainisho wa namna Abakuria walivyozaana kutoka kwa Monto, ambaye anasimuliwa kuwa ni Mzazi wa kabila zote za Wabantu. Inasimuliwa na kuaminika kuwa Wakuria ni wengi sana zaidi ya inavyojulikana . Hali hii ilitokana na kuzagaa kwa mara kwa mara na uhamaji uliotokana na msagao huo. Mbali na kutenganishwa na uhamaji, Abakuria wengi wamemezwa na kupotelea kwenye makabila mengine baada ya lugha na utamaduni wao kumezwa na makabila hayo. Kwa mfano, inasimuliwa kuwa kijana wa Wangwe aliyeitwa Gisiri aliamua kuondoka na ng'ombe wake na kwenda kuishi katika jamii ya Wamasai. Akaoa hukohuko binti wa Kimasai na kuunda jamii kubwa ijulikanayo kama Osiri ambayo lugha na tamaduni zote zina ukuruba wa jamii ya Abakuria wa sasa.

Mbali na hawa, Abakuria wengi wametekwa na kabila la Wajaluo kwa lugha, mila na desturi zao. Kwa mfano, upande wa Tanzania wilayani Tarime, mwambao wa ziwa kuanzia Utegi, kuna vijiji ambavyo ni vya Waluo, lakini inaaminika kuwa vijiji halisi vya Waluo ni vine tu. Kwa upande wa Kenya inaaminika na jamii ya Abakuria kwamba Waluo wa Gosi ni wa asili ya Abakuria ukoo wa Wairege.

4.3 Historia-simulizi ya Uhamaji na Utengano wa Abakuria.

Abuso (1980) anadokeza kuwa mwaka 900 B.K., ndio jamii za Wabantu zilianza kuondoka kutoka Misri kwa kufuata mto Naili. Walipofika eneo ambalo kunakutana Naili Nyeupe (White Nile) na Samawati (Blue Nile) Wabantu wakatengana makundi mawili. Wapo waliofuata milima ya Ethiopia na wengine wakaendelea na Mto Naili na kutokea Uganda. Jamii za Abakuria zilikuwemo kwenye kundi hili. Baada ya kufika Uganda wakafuata hadi misitu ya Kongo. Baada ya kusafiri kwa miaka mingi walifika Afrika Kusini. Katika kipindi hicho, Wabantu wengine walitawanyika sehemu mbalimbali za Afrika Magharibi, Kati na Mashariki; mfano, Wabaganda, Wahaya, Wasukuma miongoni mwa makabila mengine.

Abakuria, baada ya kutoka Ethiopia, pamoja na Wabantu wenzao walifika Mlima Elgon na wakaendelea kuhama mpaka Mlima Kenya. Miongoni mwa Wabantu walioghura nao ni; Wakikuyu, Waluhya, Wakamba, Wachagga, Wameru, Wasambaa, Wapare, Wanyiramba (kwa mujibu wa Kirutu, 2006).

Uhamaji na utengano ulizingatia maagizo ya manabii wao, ambao inasimuliwa kuwa walikuwa wanaume. Aidha, kuendelea kuishi pamoja au kuhamia eneo moja kulijenga na kukuza undugu wa karibu baina ya jamii. Kwa mujibu wa hali hii, Wabantu walioishi Mlima Kenya ni

pamoja na, Abakuria, Wakikuyu na Wachagga. Abakuria waliishi kwenye chanzo cha chemichemi ya mto Ruiro, kwa sasa eneo hili linajulikana kama Ruiru. Kwa Kikuria jina Ruiro lina maana ya mkusanyiko wa watu wengi wenye asili moja (kwa mujibu wa Masambe, 2006).

Baadaye Abakuria na Wachagga walihama na kuwaacha Wakikuyu sehemu za Mlima Kenya. Wachagga walielekea kusini mwa Mlima Kenya hadi kufikia Mlima Kilimanjaro ambapo walijiamirisha hadi leo. Abakuria nao walielekea kusini magharibi mwa Mlima Kenya mpaka kufikia kwenye vilima vidogo vya Taita ambapo walipata chanzo cha Mto Mara. Walianza kuishi na kuhama kwa kufuata Mto Mara kwa upande wa kulia. Walifuata mto huu wakiwa kundi kubwa kwa kupitia eneo linalojulikana kwa sasa kama Mbuga ya Maasai Mara (Kenya) na Serengeti (Tanzania). Waliendelea hadi eneo linalojulikana kama 'Nyagasense' (penye mchanga mwingi), ambapo mto ulikuwa umepanuka vya kutosha na kurundika mchanga na hivyo kupunguza kasi ya maji na kina kupungua (Kirutu, 2006).

Aidha, kwa maelezo yake Moronya (2006) ni katika eneo hili *Nyagasense* ndipo koo sita za Abakuria ziliamua kuvuka mto Mara na kuwa ng'ambo ya pili. Hizo koo kwa sasa zinajulikana kama; Waikizu (*Abaigisu),* Wazanaki (*Abachanake),* Wangurueme (*Abangurueme*), Waikoma *(Abaikoma*), Wanata (*Abanata)* na Waisenye (*Abaisenye).* Koo hizi zilitokana na wazee waliojulikana kwa majina; Nyakyege aliyewazaa Wazanaki na Waikizu; Mekoma, aliyewazaa Waikoma na Waisenye; na Monata aliyewazaa Wanata na Wangurueme. Hawa wote sita ndio chanzo cha majina ya koo hizi.

Kila koo imejaribu kujitenga na kuwa kabila linalojitegemea ingawa lugha, mila na desturi zinafanana. Ni muhimu kutaja kuwa Abakuria huamini kuwa Mkuria wa kwanza kuona ziwa Viktoria ni Nyakyege, matokeo yake ni usemi *Inyancha ni ya Nyakyege* (Ziwa ni la Nyakyege). Imani hii hukuza na kuhalalisha itikadi kwamba mwanaume ni mwenye akili na hekima ya juu kuliko mwanamke mintarafu ya kasi ya utambuzi wa mambo na vitu mbalimbali katika mazingira yake.

Kwa mujibu wa Nchagwa (2006), kundi lililobakia upande wa kulia mwa Mto Mara lilianza kuishi kuelekea kaskazini mwa eneo la Nyagasense hivyo basi wakaacha kufuata mwelekeo wa mtiririko wa Mto Mara. Waliishi katika bonde la kaskazini mwa mto mpaka kwenye safu za milima inayotenganisha uwanda wa chini na wa juu. Huo uwanda wa chini ulijulikana kama "Chochoro" lakini baada ya utawala mrefu na mzuri wa kiongozi Kiribo

Nyabachaita, uwanda huo ulibadilishwa jina na kuitwa kiribo mpaka hivi leo. Huyo Kiribo alitokana na ukoo ambao hadi sasa unajulikana kama 'Wakisii' .

Baadaye walivuka vilima wakaja uwanda wa juu, palipojulikana kwa jina la "Gibahwe" (Nyambeho mbariri) yaani eneo la baridi kali na udongo mwekundu. Eneo hili lilianzia vilimani hadi kuishia kwenye mwanzo wa udongo wa kichanga. Hii mipaka inatokea magharibi kuelekea mashariki, ni maeneo yaliyo mashariki mwa ziwa viktoria, kati ya Mto Mara na Mto Migori. Eneo hili lote limegawika katika sehemu tatu; Chochoro (Kiribo), Gibahwe (Chonoche) na Giringani (Muyuyi). Majina yaliyo kwenye Mabano ndiyo yanayotumika kwa urejeleo wa Maeneo haya hadi sasa. Asili ya majina haya ni watawala waliovuma sana kwa ujasiri wao katika kutetea, kulinda na kuongoza jamii ya Abakuria (Masambe, 2006). Ni muhimu kutaja kuwa viongozi hawa wote walikuwa wanaume, hali ambayo huhalalisha imani kwamba uongozi wa familia na jamii ni kazi ya jinsia ya kiume. Hivyo basi tangu enzi hizo mwanaume alistahili kuwa jasiri ambaye alitunukiwa jukumu kubwa la kulinda, kutetea na kuongoza jamii yake. Aidha, historia ni Malighafi ya kimsingi kwa nyiso za jando hivi kwamba baadhi ya nyiso tulizozirejelea katika kazi hii zinabainisha maeneo na mazingira ambayo yamerejelewa hapo juu. Hivyo basi, historia huwa na mchango mahususi katika utamaduni na fasihi ya jamii.

Baadaye, waliendelea zaidi kaskazini na kuingia eneo lililojulikana kama 'Giringani' wakiwa chini ya mtawala aliyeitwa Muyuyi Nyabihore (kwa mujibu wa Kirutu, 2006). Walipofika Kehancha, ambayo kwa sasa hivi ni makao makuu ya wilaya ya Kuria, walipata utajiri mkubwa wa chakula na mifugo hasa ng'ombe. Uzao uliongezeka sana na maisha yao yakawa bora mno; kutokana na ustawi huu, waliimba wimbo *Keragento kehancha* ukiwa na maana (kila kitu kimekubali*)*. Hii ndio asili ya jina Kehancha. Eneo hili la Kehancha hadi Mto Migori lilibadilika jina kutoka *Giringani* hadi *Muyuyi* jina la kiongozi wa Abakuria kipindi hicho.

Kwenye maeneo haya, kati ya Mto Mara na Mto Migori, walikuta makabila manne yakiishi humo. Ambayo ni, Wanyairamba, Watatiro, Wabobwe na Wasing'eng'i. Kutokana na nguvu na ujasiri wa wanaume wao, waliwafukuza Wanyiramba kuelekea kusini hadi Singida (Tanzania). Nao Watatiro walielekea sehemu za Narok, lakini Wabobwe na Wasing'eng'i walitekwa na kumezwa na kuwa kundi la Abakuria liitwalo Abagichere (Matiko, 2006).

Waliendelea kusonga na kuelekea kaskazini mpaka kwenye vilima viitwavyo Kabianga. Walipofika hapo, kiangazi kilitokea, wakawa na uongozi mbaya, mifugo wakadhoofika na wengi

wakafa. Mifugo wengine wakaibiwa na Wamaasai. Kutokana na lindi hilo la shida, njaa ikawaua wengi na maisha yao yakawa ya shida kubwa. Hapo ndipo palikuwa nyumbani kwao (ka) lakini kila kitu kilikataa (bianga) kinyume na Kehancha. Hivyo wakaanza kulalamika kwa kusema *kabianga,* wakimaanisha 'nyumbani vimekataa'. Hadi waleo kuna vilima vya Kabianga .

Kwa mujibu wa Kirutu (2006), jamii ya "Ogusuhi" ilivumilia shida hizi, lakini jamii zingine ziliamua kurudi Kehancha. Waliobaki Kabianga hadi leo wanajulikana kama Wakisii. Baada ya kufika Kehancha tena waliendelea na kuelekea magharibi mwa eneo la Muyuyi wakaishi kandokando ya mto Migori upande wa kushoto mpaka walipofika ziwani, hawakuvuka mto tena. Kule pwani ya ziwa walipaita *Gendia*, jina lenye maana ya tembeza juu ya maji. Baadaye walianza kuhama kuelekea upande wa kusini mwa hilo eneo huku wakiambaa na pwani ya ziwa. Waliendelea hadi wakafika Shirati (Chirate) ambayo ina maana ya "kelele za kushangilia kwa furaha". Inaaminika kuwa eneo hilo la Shirati ndipo walipofanyia sherehe zao za jubilii (*Egekerero*) (Nchagwa, 2006).

Eneo hilo la Shirati, ndipo waliopoachwa Wasoba, ambao idadi yao kubwa imetekwa na Wajaluo, mintarafu ya lugha, mila na desturi. Wengine waliendelea kwa kupitia kisima cha Kemwita wakielekea eneo la mashariki mwa Mlima Rorya. Waliendelea na huo mwambao wa Chonoche kupitia Mlima Tarime mpaka eneo la Nyansincha. Baada ya hapo walivuka na kuingia eneo la Muyuyi mpaka Misimei sehemu iliyoko Umasaini. Walipitia sehemu iliyojulikana Gutura. Kwa sababu ya vita na Wamasai, walilazimika kurudi tena kupitia Getasengeri Goroswe wakapita Ng'atabarigo eneo ambalo kwa sasa linajulikana kama Ng'ata Barigoi, walipita Togota na kurudi tena Gatura.

Ni katika eneo hili, kwa mujibu wa kumbukumbu za mzee Moronya , siku moja nabii wa Abakuria aliamuru Abakuria kutengana; aliwaamsha asubuhi na mapema kitendo ambacho kwa Abakuria ni *ugutura*. Hivyo, kwa kumbukumbu ya tukio hilo eneo hilo hadi leo linaitwa Gutura. Hili ni eneo lililoko Muyuyi mashariki mwa Kehancha. Utengano huu ulikuwa kama ifuatavyo: Abairege walienda kuishi Getasengeri, Abanyamongo (Abaracha) walienda Gairoro. Abanyabasi wakaenda Matare, Abanchari walielekea Nyakwiriategera, Abagumbe wakaenda Chinato, Abakiira wakaenda Gatende, Abasweta wakaenda Bungurere, Abasembete walienda Kangariani, Abakenye walienda Nyamwaga (Nyamogora) Abakeroba walienda Rosana (Ng'aramwa) na Abatimbaru walienda Binage (Mzee Matiko 2006). Ni muhimu kutaja kuwa huu ndio ulikuwa

msambao mkubwa uliotokea ndani ya koo za Abakuria. Katika koo hizi, Abairege walikuwa Mashariki kwa wote na Watimbaru ndio waliokuwa Magharibi kwa wote.

Waliobaki eneo la Muyuyi ni Abairege, Abanyamongo, Abanchari, Abanyabasi, Abakira na Abagumbe. Walioenda Chonoche kwa kuazia Mashariki ni, Abasembete, Abasweta, Abakenye, Abakeroba na Abatimbaru. Katika koo hizi ni Abatimbaru peke yao ambao hawakuhama kutoka lile eneo lao la Binage. Abakeroba walihama jumla na kwenda Musoma, ingawa hadi sasa lugha, mila na desturi zao zina ukuruba na jamii zingine za Abakuria (Matiko, 2006).

Hivi sasa maeneo ya Kiribo, Chonoche na Muyuyi ambayo yako kati ya Mito Mara na Migori yamekaliwa na jamii ya Abakuria. Ingawa kwa miaka ya hamsini, koo mbalimbali zilianza kuhama na kuvuka Mto Mara na kwenda kuishi wilayani Serengeti. Kwa sasa Abakuria wanapatikana ng'ambo zote za Mto Mara. Kwa upande wa Magharibi Abakuria wamepakana na ziwa Viktoria na kabila la Wachita kule Musoma wamepakana na Bunda. Kusini wamepakana na kabila la Wasukuma na Mbuga ya Serengeti. Upande wa Mashariki kuna mbuga ya Masai Mara na jamii ya Wamasai na kaskazini kuna Wamasai, Wakisii na Wajaluo.

4.4 Jadi ya Abakuria

Kwa mujibu wa Akivaga na Odaga (1982:116)

> Jadi ni dhana ambayo inajumlisha tabia za watu wa jamii fulani. Tabia hizi mara nyingi huzingatia mila na miiko ya jamii. Isitoshe, tabia na matendo ya watu huongozwa na maadili mbalimbali ya kijamii. Kwa hivyo fasihi simulizi ni msimbo ambao, kupitia kwayo maadili ya mafunzo ya kijamii huhifadhiwa na kupitishwa (tafsiri yangu)

Kwa hivyo, fasihi simulizi ni nyenzo mwafaka ambayo hudhihirisha na kuendeleza, itikadi, imani, mitazamo, mielekeo na matarajio ya jamii kumhusu kila mwanajamii. Fasihi simulizi hubainisha tabia na matendo yanayokubalika katika jamii. Matendo na tabia fulani huendelezwa na kila mwanajamii katika kukidhi mahitaji ya asasi mbalimbali za jamii. Kwa mfano, tabia za kishujaa, ukakamavu, uhodari na utetezi wa jamii ni sehemu muhimu ya utambulisho na uhifadhi

wa uume. Imani hii iliendelezwa na jamii kupitia tanzu mbalimbali za fasihi simulizi ya Abakuria ikiwemo utanzu wa nyiso za jando.

Katika sehemu hii, tutajikita katika kudhihirisha bayana jadi za kimsingi ambazo huthaminiwa na jamii ya Abakuria na kwa jinsi ambavyo hubainika katika awamu mbalimbali za maisha ya wanajamii, kutoka kuzaliwa hadi hatima ya maisha yake ulimwenguni. Katika maisha ya Mkuria, kuna sherehe mahsusi ambazo huandamana na kila awamu ya maisha yake; kuna sherehe andamizi za kuzaliwa kwa mtoto, anapotahiriwa, anapoolewa au kuoa na anapofariki.

Katika kila awamu, tumejaribu kubainisha jinsi ambavyo zinachangia kukuza, kuendeleza na kuhifadhi uume na sura mahususi ya mwanaume. Awamu hizi kwa njia moja au nyingine hubainisha mielekeo, mitazamo na matarajio ya jamii kumhusu mwanaume. Kwa kufanya hivyo tumejikita kwa kudhihirisha imani za kitamaduni na jinsi ambavyo zinachukuliwa kama uti wa mgongo wa kutawala hatua mbalimbali za maisha ya mwanaume katika jamii ya Abakuria.

4.4.1 Awamu ya Kuzaliwa na Malezi

Uwezo wa kuzaa miongoni mwa jamii ya Abakuria ulithaminiwa na kutunukiwa heshima kubwa, kwani ulikuwa ni hakikisho la kuendeleza jamii, kizazi baada ya kingine. Ukosefu wa uwezo huu ulichukuliwa kama laana, swala ambalo liliwapatia wanajamii wasiwasi mwingi. Mwanamke ambaye hakutunukiwa uwezo huu aliitwa "Omogomba" na kwa kiasi kikubwa alidharauliwa sana na jamii. Hali hii ilimlazimu mwanaume kuoa mwanamke mwingine. Mwanamke huyu wa pili angekosa kuzaa, ilithibitika kuwa mwanamume ndiye aliyekuwa na kasoro. Mwanaume wa aina hii ailiitwa 'inture". Hali hii iliibua haja ya mwanaume kwenda kwa mpiga ramli "Omoraguri" ili ajue chanzo cha kasoro hiyo. Iliposhindikana kabisa, ndugu wa mume au binamu yake aliteuliwa kushiriki kingono na mkewe ili kumzalia watoto. Iwapo ilibainika bayana kuwa mwanamke ndiye aliyekuwa na kasoro, alilazimika kuoa mke mwenza baada ya miaka fulani. Ndoa ya aina hii ilijulikana kama "inyumba mboke".

Hali ambapo mwanamke alikosa kupata mtoto wa kiume, ilimlazimu mwanaume kuoa mwanamke mwingine. Vilevile ilimlazimu mwanamke kuoa mwanamke mwenzie, kwa kutumia mahari ya mmoja wa binti wake. Hili ilitokana na thamani kubwa aliyotunukiwa mtoto wa kiume katika jamii.

Kuwa na watoto wengi katika familia; wasichana kwa wavulana, kulikuwa sifa kubwa kwa mwanamume. Alitunukiwa heshima na taadhima kubwa kutoka kwa jamii. Nyiso ni kielelezo cha hali hii.

Ikihita getaata ne kenene
Kerarenta bairo na bageni
na bako ba ng'ombe

lango la baba ni kubwa
linaleta shemeji na wageni
na shemeji wa ngombe

Nyiso hii huashiria wasichana kuolewa na vijana kuoa na kupanua nasaba ya jamii kwa jumla. Miongoni mwa jamii ya Abakuria mwanamke mja-mzito hakuficha hali yake, kwani hali hii ilibainisha uwezo wa mume na mke katika kupata mtoto. Tokeo hili lilimfanya mwanamume kuheshimiwa kwa kudhihirisha uwezo wake wa uzazi. Katika hali hii mwanamke alilishwa vizuri na kuepushwa kufanya kazi ngumu, alitunzwa mithili ya yai.

Isitoshe, ujauzito katika ndoa ya waliooana karibuni ni swala lililoleta furaha kwa familia ya bwana na bibi. Ilikuwa ishara mwafaka ya kuimarisha uhusiano baina ya familia ya mume na mke na udumishaji wa nasaba ya mume, pia ujauzito ulithibitisha uwezo wa uzazi wa mume na uwezo wa utungisho wa mwanamke. Katika nyiso za jando thamani ya uwezo huu ilielezwa kama ifuatavyo:

Tiga ngore baaba umwene ibisa
Newe biare gwita komagiha
Araikara araibonda mona obota
Bokogera seto na burugo nantera moroni.

Namsifu mama aliyenizaa
Ndiye aliyehisi uchungu wa uzazi
Uchungu ukamfanya kujikunja mithili
Ya upinde, karibu na maviga,kama

Upinde wa kwendea vita na uporaji wa
Ng'ombe katika nchi za maadui

Mwanamke alipokaribia kujifungua, wakunga waliitwa kwa minajili ya kutekeleza wajibu wao, alipojifungua salama, shangwe na vigelegele, vilisikika kutoka kwa nyumba alimojifungulia. Shangwe na vigelegele hivi vilitegemea jinsia ya mtoto. Iwapo alikuwa mtoto wa kiume vigelegele vilikuwa vingi na vilitolewa kwa sauti ya juu, huku wakisema "ni itimo na nguba"! (ni mkuki na ngao, zana ambazo ziliashiria jinsia ya kiume). Iwapo ni mtoto wa kike vigelegele vilikuwa vichache na kwa sauti ya chini huku wakisema "Mosaire go nkwe" (ni kitita cha kuni) ishara ya jinsia ya kike. Ni bayana kuwa hali hii ni ithibati mwafaka ya thamani ya mtoto wa kiume. Zana za mkuki na ngao zilitumika kubainisha sura na wajibu wa mwanaume katika jamii.

Katika jamii ya Abakuria mwanamke aliyezaa wana wa kike bila mtoto wa kiume alidharauliwa. Kila mara alirejelewa kama "Monya basagane" (mwenye wasichana). Jambo hili lilimlazimu mume kuoa mwanamke mwingine. Ili kuhakikisha amepata mtoto wa kiume, ambaye angekuwa mrithi wake. Inaaminika kwa jamii ya Abakuria kuwa mwanamke hawezi kurithi mali ya baba yake. Kwa sababu hii mwanaume huchukuliwa kama jinsia muhimu sana katika uendelezaji wa uhai wa jamii. Anasawiriwa kuwa mwenye uwezo na mamlaka zaidi kuliko mwanamke takribani katika maswala yote nyeti ya jamii. Kwa mfano urithi, ulinzi, kutosheleza mahitaji ya kifamilia na hakikisho la kuendeleza jamii kiuzazi.

4.3.2 Sherehe za Kumpatia Mtoto Jina

Miongoni mwa jamii ya Abakuria, majina yalitofautiana kiuana. Mtoto wa kike alipewa jina baada ya siku nne, ilhali mtoto wa kiume alipewa jina baada ya siku tano. Tofauti hii ni ishara ya thamani kwa mtoto wa kiume. Jamii ya Abakuria ina majina sita kwa kifungua mimba, matatu ya kike (Boke, Gati na Robi) na matatu ya kiume (Mwita, Marwa na Chacha). Kwa mtoto wa pili na kuendelea kuna mifumo ya kuzingatiwa, kwa mfano majina ya wanajamii waliotangulia na ambao wamekufa yalitumiwa, mashujaa, matukio ya kukumbukwa, mahali alipozaliwa mtoto na majira. Kwa mfano, mtoto aliyezaliwa njiani aliitwa; 'Nyagochera' iwapo ni msichana na 'Machera' ikiwa ni mvulana.

Malezi

Mtoto katika jamii ya Abakuria alikuwa ni wa jamii nzima; ndiposa kuna methali ya Abakuria;

Temoona aana mweene hai

Mtoto hana mwenyewe

Ilikuwa ni wajibu wa jamii nzima kumlea na kumkuza mtoto; alipoonekana kufanya kosa, kila mwanajamii alikuwa na wajibu wa kumrudi na kumwelekeza ipasavyo. Kusudi kubwa lilikuwa kuwakuza watoto wenye heshima ndani na nje ya jamii yao. Hivyo basi, mafunzo kwa watoto yalitekelezwa na jamii nzima. Mafunzo haya yalihusu mwenendo wa watoto, majukumu, matarajio, itikadi miongoni mwa mengine. Haya yote yalitekelezwa kiuana. Wanawake walikuwa na wajibu wa kuwafunza watoto wa kike na wanaume kuwafunza watoto wa kiume. Hali hii ilizua sura tofauti ya kijinsia kadri watoto walivyoendelea kukua. Watoto wa kiume, kwa mfano, walifunzwa majukumu ya kiume, mielekeo na matarajio ya jamii kuwahusu na nafasi yao katika jamii. Kwa kiasi kikubwa, ni katika kipindi hiki ambapo ujenzi wa uume na sura halisi ya mwanamume hujitokeza. Watoto wa kiume walijitahidi kuepuka tabia na majukumu ya kike. Walilazimika kujaribu kwa vyovyote vile kuiga yanayowapasa kutoka kwa jinsia ya kiume. Kwa mfano, wavulana walifunzwa kilimo, uhunzi, ufugaji, ufumaji, ujenzi, ulinzi na umuhimu wa ushujaa, kujitegemea na uhodari. Haya yote yalisisitizwa katika utekelezaji wa majukumu yao katika jamii. Alipokaribia umri wa kutahiriwa, alijenga nyumba (isiiga) yake wakati huu, kwa usaidizi wa vijana wa rika lake na vijana wengine ambao wametahiriwa chini ya uongozi wa wazee wa familia. Alipelekewa chakula kwenye nyumba yake na alikuwa huru kutoka na kurudi nyumbani wakati wowote. Hali hii ni ithibati ya kutosha kuwa kijana wa kiume hujamiishwa kuwa huru, kujitegemea na kuhudimiwa na jinsia ya kike, akiwa katika umri mdogo. Aidha, katika umri huu mvulana hubainisha uwezo na mamlaka yake katika jamii, ili kudhihirisha kuwa amekomaa vya kutosha kutahiriwa.

Katika kipindi hiki familia na jamii huchukua sehemu muhimu katika kujenga mtazamo wa kilimwengu na uelewa wa matendo ya mtoto katika jamii. Pindi wavulana wanapobaleghe, wengi wao huwa wamejifunza kwa kina jinsi ya kukuza na kuhifadhi tabia zao za kiume na utambulisho wao katika jamii. Hali hii huwafanya kujitahidi kwa vyovyote kutoonyesha mhemuko na kuwahimiza kudhihirisha hasira, ushari, ushujaa katika kutekeleza majukumu ya kiume pindi watakapotahiriwa, mafunzo haya huwatarayarisha kikamilifu katika kuingia kundi la "Abamura" (mashujaa wajamii).

Kere ngosoka na abamura
nebo bagitere rogakong'a
nkanyora rroika kurwa igoro
roracha waito kubihita, hara
tokoraria ichintang'ana
hamwe na ichimori.

Ninacho heshimu ni mashujaa
ndio walioziba ua imara
ambao ulikuwa umeanguka
na kuacha mwanya katika lango
la zizi letu, wanapolala ng'ombe
wetu

Nyiso hii hubainisha thamani ya mtoto wa kiume katika kutekeleza wajibu muhimu wa ulinzi katika jamii. Hii ni kwa sababu, katika jamii ya Abakuria watoto wa kiume huthaminiwa zaidi, kwani wao ndio watetezi na walinzi wa jamii.

4.4.3 Awamu ya Tohara: "Esaro"

Miongoni mwa jamii ya Abakuria wavulana na wasichana walipashwa tohara wakiwa kati ya umri wa miaka kumi na moja na kumi na saba. Hata hivyo, umri huu hubadilika kutegemea uwezo wa kichumi na wa kisosholojia wa jamii ya mtahiriwa. Kwa mfano, msichana kutoka familia maskini alipashwa tohara akiwa na umri mdogo, kumuweka tayari kuolewa ili apatie familia yake mahari. Kwa upande mwingine, familia ambayo ilikuwa na mvulana pekee "Omosorori" alipashwa tohara akiwa na umri mdogo, kwa ajili ya kuoa kwa kutumia mahari ya dada zake wakubwa kwake. Hali hii ilimlazimu mvulana wa aina hii kuoa wanawake wengi, kwa kusudi la kupata wavulana wengi. Kwa jinsi hii, jamii ilihakikisha kwamba kizazi chake hakitafifia wala kutoweka.

Kabla ya siku ya kutahiriwa, wavulana ambao wanajitayarisha kutahiriwa "abarisia" walipewa mafunzo na wazee, ambayo yalihusu historia na umuhimu wa ushujaa na utetezi wa jamii. Mafunzo haya yalisisitiza ujasiri kama kipimo mahususi cha uume. Kipindi hiki, vilevile, kilitumika kuwatayarisha wavulana hawa kisaikolojia kuhimili ukali wa kisu kwa ushupavu wao

wote, kwa sababu inaaminika kuwa kupepesa jicho wakati wa kutahiriwa ni ishara ya kulia *ugukura* ambapo matokeo yake yalikuwa ni kutengwa na kuchekwa na jamii nzima (Masambe,2006)

Asubuhi na mapema, siku ya kutahiriwa, mvulana huyu alisindikizwa kwenda kutahiriwa na vijana wengine wa kiume ambao walikuwa wametahiriwa "Abamura". Hapa ndipo mvulana huyu alighani nyiso za sifa kwa vijana hawa waliompeleka, kusudi likiwa kuwatia hamasa. Nyiso hizi ziliashiria ujasiri wake na kwamba yuko tayari kujiunga na kundi la waliotahiriwa "Abamura" (Mutundi 2006).

Abamura bawaito monga nkoba
mete mogosara na binyege
na nkomo cha biara

vijana wetu wa kiume ni mithili ya radi
hupasua mapandikizi ya miti kwa
mikono na makucha ya vidole.

Kijana huyu alivikwa maleba yaliyojumlisha kofia ya ngozi ya chui au simba yenye manyoya ya kunguru, alivikwa shuka, huku amebeba sime na mkuki. Hii ilikuwa ishara ya shujaa wa jamii ya Abakuria. Aidha, ilibainisha hatua muhimu ya kuonyesha kujitarayarisha kwa mvulana huyu katika kujiunga na kundi kubwa la "Abamura" katika kulinda, kutetea na kutekeleza wajibu wa mwanaume katika jamii.

Baada ya kufika mahala pa tohara, watahiriwa walijipanga kwa mstari, vijana waliowapeleka wakisimama mbele na nyuma yao na kuendelea kuwapa motisha ya kisaikolojia ili kuhimili uchungu wa kisu kwa ushujaa bila kutetereka kwa hali yoyote. "Omosari" (ng'ariba) alianza kuwatahiri "abarisia" mmoja baada ya mwingine kwa kukata gofu la dhakari.

Baada ya kutahiriwa kijana huyu alisindikizwa nyumbani na vijana waliompeleka na kupokelewa na wanawake ambao walimwimbia nyimbo za sifa, huku akiendelea kughani nyiso, ambazo yaliyomo yalidhirisha ushujaa wake na wa vijana waliompeleka. Pia hakuepuka kupigia hali ya kutotahiriwa "uburisia" kwa heri na kubainisha uhodari wake katika kuingia katika kundi la wanaume mashujaa wa jamii yake. Alitembea polepole kuelekea nyumbani huku akipongezwa

kwa nyimbo na zawadi. Waliompeleka walikimbia kwa furaha kubwa na kwa ushupavu huku wamejifunga maleba ya kishujaa.

Baada ya kutahiriwa, vijana wa kiume walitiwa jandoni kwa muda takribani mwezi mzima. Katika kipindi hiki, vijana hawa walipata mafunzo kutokana na wazee walioteuliwa na jamii. Mafunzo haya yalijumlisha majukumu ya jinsia ya kiume, mbinu za vita, matumizi ya zana za vita, mambo yanayohusu unyumba. Mafunzo haya yalibainisha upeo wa juu wa ujenzi wa uume, kwani ni baada ya kipindi hiki ambapo kijana wa kiume alikuwa yuko tayari kushiriki na kutekeleza wajibu wake na kutetea nafasi yake kama mwanaume katika jamii. Aidha, walifunzwa kukuza na kutetea hadhi yao katika jamii na umuhimu wa ushirika wao. Hatima ya kipindi hiki ni sherehe ya kutoka jandoni "Omoroko". Hii ilikuwa ni sherehe ya siku moja ambayo inaweza kumithilishwa na sherehe ya kufuzu kwa wanazuoni katika chuo kikuu. Sherehe hii ilifanywa baada ya wote waliotahiriwa kupona, na kupewa jina la utambulisho wa rika lao. Ni baada ya sherehe hii ambapo kijana wa kiume alikuwa radhi kuoa na kutekeleza wajibu wake wa kiume katika jamii.

Mabadiliko ni sehemu muhimu ya ukuaji wa binadamu. Hatua ambazo mwanaume hupitia kutoka utotoni hadi utu-uzima miongoni mwa jamii ya Abakuria hubainishwa bayana kupitia kwa tohara, kwani tendo hili hudhihirisha wazi tofauti ya mwanaume na mwanamke. Vilevile hubainisha ukamilifu wa mwanaume na uume katika jamii. Katika jamii ya Abakuria kitendo cha kutahiri kimekolea na hupewa umuhimu mkubwa. Kinatekelezwa na wanaume wa umri mkubwa. Kinahusisha kiwango kikubwa cha uchungu wa kimwili na kuteseka kihisia. Hali hii huwa fundisho muhimu katika kukoleza ushari na uwezo kwa vijana wa kiume. Wanaume huamini kwa pamoja kuwa tohara ni kitendo kisichoepukika na hubainika kama hakikisho la mabadiliko ya kumfikisha mwanaume katika hadhi ya kijamii inayokubalika (Mutundi, 2006).

Baada ya tohara na sherehe za kutoka jandoni, kijana huyu huwa yuko tayari kuoa. Pia huwa tayari kujifunza umuhimu wa ushirikiano katika jamii hasa katika kulinda jamii, na kujumuika na wanaume wenzake katika kutetea na kuendeleza jamii. Kwa mujibu wa matayarisho yake ya kuoa, alitambua umuhimu wa ng'ombe kama sehemu muhimu ya mahari. Mwanaume aliyeoa kwa kutumia mahari yake alitunukiwa sifa na heshima kubwa. Alibainisha juhudi zake ambazo zilichukuliwa kama kigezo muhimu cha kubainisha kujitosheleza kwake katika kuikuza na kuikimu familia yake. Kwa kufanya hivi alijitambulisha kama mwanaume mwenye uwezo, mamlaka na wakujitegemea katika jamii.

4.4.4 Awamu ya Ndoa

Ndoa ni hatua muhimu sana katika jamii ya Abakuria. Ni swala ambalo lilikuwa lazima, kwani ndoa ilichukuliwa kama hakikisho la uendelezaji wa kizazi na jamii kwa ujumla. Msichana na mvulana aliyefariki kabla ya kuoa au kuolewa alizikwa mbali na boma. Kifo cha aina hii kilichukuliwa kama kimetokana na laana fulani. Kwa sababu hii, baada ya tohara, mvulana alipaswa kujitahidi iwasekanavyo ili kupata jiko.

Kwa mujibu wa mila na desturi za jamii ya Abakuria kijana wa kiume hupewa nafasi katika kujichagulia binti anayedhamiria kumwoa. Wasichana hawana hiari hii. Kwa upande mwingine, wazazi wa mvulana waliweza kumpendekezea mwanao wao binti wa kuoa. Hali hii vilevile haikuwepo kwa upande wa msichana. Kwa hivyo, ni bayana kuwa msichana hakupewa nafasi ya kujichagulia mume wa kumwoa.

Baada ya utambuzi huu, mshenga kutoka kwa upande wa mvulana alitumwa kupeleka ujumbe wa posa "Obokwe" kwa msichana aliyeteuliwa. Familia hizi mbili zilipokubaliana ziliingia katika hatua ya majadiliano ya mahari. Ni muhimu kutaja kuwa hatua ya posa na majadiliano ya mahari zilitekelezwa na wanaume, kwani uhusika wa wanawake ulikuwa wa kutoa maoni na wala si wa kukata shauri. Aidha, miongoni mwa jamii ya Abakuria mwanamke husawiriwa kama binadamu asiyehifadhi siri na mara nyingi hukasirika haraka. Hali hii ilimpa mwanamume nafasi pana katika majadiliano na maamuzi juu ya maswala muhimu katika jamii.

Baada ya maafikiano ya idadi ya mahari, familia hizi mbili zilikubaliana siku ya kuchukua mahari kutoka kwao mvulana *"Ekemaho"*. Ni muhimu kutaja, kuwa miongoni mwa jamii ya Abakuria, ng'ombe ndio sehemu kuu ya mahari. Kwa sababu hii, ng'ombe huthaminiwa sana katika jamii ya Abakuria, kiasi kwamba mwanaume aliyeoa kwa kutumia ng'ombe wake bila kupewa msaada wowote aliheshimiwa na kupigiwa mifano katika jamii.

Siku ya "ekemaho" ilipowadia, babake msichana, ndugu zake, vijana wake na marafiki waliandamana kwenda kwa mvulana kwa minajili ya kuchukua mahari. Hawakuandamana na mwanamke. Hali hii ni ithibati ya mamlaka aliyonayo ambayo hubainisha uhusika mkubwa na mwanaume katika maswala muhimu ya jamii. Wanawake walihusika katika shughuli za kupika na kuwatayarishia wageni na wenyeji chakula. Makundi haya mawili ya wanaume yalijadiliana na kuafikiana juu ya tarehe ya harusi bila wanawake kuhusishwa. Hali hii inabainisha nafasi pana ya wanaume katika kufikia uamuzi wa maswala ya kijamii.

Ilipofika siku ya sherehe ya harusi, bwana harusi aliandamana na wasimamizi wake, marafiki na jamaa wake, kwenda kwa bi arusi. Walipofika walilakiwa kwa nderemo na vifijo na bi arusi na wasimamizi wake. Hatimaye, walielekezwa kwenye nyumba iliyokuwa imetayarishwa na kuandaliwa kwa ajili yao. Walipewa vyakula, vinywaji na viburudisho vya aina mbalimbali. Hatimaye, wazazi na jamaa wa bibi harusi walijumuika na kundi la bwana harusi katika kipindi cha hotuba. Hotuba hizi zilihusisha wosia kwa bibi na bwana harusi katika kutimiza wajibu wao katika ndoa.Hii in pamoja na matarajio ya jamii kuwahusu, kama mume na mke. Hotuba hizi zilimpatia mwanaume nguvu, uwezo na mamlaka kama 'kichwa' katika familia na kuhalalisha nafasi ya mwanamke kama msaidizi wake katika ndoa. Aidha, majukumu ya mwanamke na mwanaume katika ndoa yalibainishwa bayana; na kusisitizwa, hali ambayo ilibainisha tofauti kubwa za kijinsia.

Baada ya kipindi cha hotuba, bwana arusi na wasimamizi wake waliondoka, na hatimaye bibi harusi, na wasimamizi wake walifuata huku wakisindikizwa na jamaa na marafiki kuelekea kwa bwana harusi. Sherehe ya harusi iliendelea kwa bw. arusi hadi siku iliyofuata. Baada ya sherehe za harusi, bwana harusi alimjulisha bibi harusi kwa jamaa wake ili kumtambulisha kama mmoja wao katika familia. Mama mkwe alimfunza mkaza mwanawe majukumu ya kinyumba, hasa zaidi jinsi ya kujenga na kuendeleza ndoa yenye mafanikio. Mwanaume naye aliingia kwenye kundi la watu wazima. Alikuwa radhi kujiunga na baraza la wazee. Hivyo basi alikuwa amepiga hatua muhimu ya kijamii ya kumwezesha kutoa maoni, uamuzi na mwelekeo katika maswala muhimu ya kijamii.

Katika maisha ya ndoa, mwanaume alikuwa na wajibu wa kiitikadi wa kuwa nguzo ya familia yake na kuitosheleza kwa hali yoyote. Mwanamke alikuwa msaidizi tu, mamlaka na uwezo katika ndoa ni viambajengo muhimu vilivyomtambulisha mwanaume katika familia na jamii kwa jumla.

4.4.5 Ada za Mazishi/Matanga

Miongoni mwa jamii ya Abakuria, kifo kilikuwa ni mwisho wa safari ya maisha ya binadamu ulimwenguni na mwanzo wa maisha baada ya kifo, ahera. Huko ahera marehemu hakuwa binadamu tena bali pepo. Kifo kilileta simanzi na huzuni kwa jamii kwani kilisababisha pengo lililobaki katika kumbukumbu za wanajamii daima dawamu.

Kwa sababu ya imani ya maisha baada ya kifo, jamii ya Abakuria huwaita watoto wanaozaliwa majina ya waliokufa. Majina ya wanaume ambao waliishi bila mchango wowote katika jamii, waoga, waliokuwa na akili punguani na ambao walikufa bila kuoa majina yao yalitumbukia kwenye kaburi la sahau. Hali hii ilikuwa tofauti kabisa na mwanaume ambaye alisheheni sifa za kutajika na kukumbukwa, kila mwanajamii alikuwa na kila sababu ya kuita mtoto wake wa kiume majina ya wanaume wa aina hiyo. Hii ni kwa sababu ya imani kuwa kulikuwa na uhusiano mkubwa wa jina na urithi wa tabia za mwenye jina aliyetangulia kuishi.

Sherehe za matanga na mazishi ziliratibiwa mintarafu ya uana. Ni wanaume walioo walioruhusiwa kuchimba kaburi (*imbehera/indwi*). Mwanaume alizikwa katikati mwa zizi upande wa kulia ilihali mwanamke alizikwa upande wa kushoto. Mwanaume alilalia mkono wa kulia akiwa kwenye jeneza ilihali mwanamke alilalia mkono wa kushoto. Dhana ya mkono wa kulia ni ishara ya nguvu na uwezo wa mwanaume katika jamii ya Abakuria, sifa ambayo huandamana nayo hata ahera. Katika hatua ya kurusha mchanga kaka mkubwa wa aliyefariki alitangulia. Pale ambapo hakuwa na kaka mkubwa mwanaume wa rika yake kutoka kwa ukoo wake alitekeleza wajibu huu. Hatimaye jamaa na marafiki walifuata (Masambe,2006)

Baada ya mazishi, matambiko kadhaa hufanywa kuanzia jioni ile. Wakati wa kipindi cha matanga, jamaa wa aliyefariki hawakuruhusiwa kutoka nje ya boma lao, kusafiri au vijana wa kiume kwenda vitani. Muda wa kipindi cha matanga ulitegemea uana; ikiwa ni mwanaume aliyefariki, kipindi hiki kilichukua siku tano ilihali mwanamke ni siku nne. Hatima ya matanga, ni sherehe ya kunyolewa nywele kwa jamaa ya aliyefariki (*ukwirabi),* baada ya sherehe hii jamaa wa marehemu walikuwa huru kushiriki shughuli zao za kawaida na waliruhusiwa kutoka nje na kujumuika na wengine.

Ni muhimu kutaja kuwa mazishi miongoni mwa Abakuria hutegemea uana na umri wa marehemu. Watoto huzikwa nje ya zizi la ng'ombe. Ilihali kuna mahali maalum kwa watu wazima ndani ya zizi la ng'ombe (bori).

Katika kitengo hiki, tumeshughulikia awamu mbalimbali za maisha ya kila mwanajamii na kuziambatanisha na sherehe andamizi. Ni bayana kuwa kila awamu inatawaliwa na miiko mahususi na ina umuhimu wake. Hii ni kwa sababu kila awamu ni kiungo muhimu cha ukuzaji wa wanajamii. Hoja zinazodhihirika katika awamu hizi zinampa mwanaume nguvu, uwezo na mamlaka zaidi ya mwanamke. Kwa mfano, mtoto wa kiume anapozaliwa hupokewa kwa furaha

na vifijo zaidi kuliko yule wa kike. Aidha, ni bayana kuwa, thamani kwa mwanamume huanzia siku anapozaliwa hadi anapokata roho.

4.5 Mifumo ya Kijamii, Kisiasa, Kidini na Kiuchumi ya Abakuria

Nyiso tulizozikusanya huunda urejeleo wa utamaduni, siasa, uchumi , dini na maisha ya Abakuria kwa jumla. Aidha, zinabainisha majukumu ya kila mwanajamii katika kukidhi mahitaji ya jamii ya Abakuria. Kwa hivyo, uelewa wa jamii, utamaduni, mpangilio wa kisiasa na shughuli za kiuchumi za Abakuria ulitumika kama jiwe la msingi katika umaizi na uchanganuzi wa nyiso tulizozikusanya. Umuhimu wa sehemu hii ni kutokana na ukweli kwamba, fasihi ni sanaa inayotumia maneno katika kuyaeleza na kuyahakiki maisha na mazingira ya jamii; ni zao la jamii, huchota maudhui yake katika harakati za maisha huku ikicheua vionjo na vya watu wa jamii hiyo katika muhula maalum. Hivyo basi nyiso za jando miongoni mwa jamii ya Abakuria ni utanzu wa fasihi yao ambao umo ndani ya mipaka ya jamii na ndani yake ni jumla ya maisha yao.

4.5.1 Hali ya Maisha na Muundo wa Jamii ya Abakuria

Kulingana na Chacha (1999) ulimwengu wa jamii ya Abakuria umejengeka kutokana na vitengo panA kuanzia kwa familia ya wazazi wawili na watoto wao, ndoa ya wake wengi hadi mbari nzima ya Abakuria. Kitamaduni Abakuria huishi kwenye makazi ya nyumba zaidi ya mbili ambazo zimezungukwa na shamba. Nyumba hizi hujengwa kwa mzunguko ambao una zizi la ng'ombe katikati. Katika hali nyingi, baba, vijana wake wa kiume na wajukuu huunda familia moja. Chakula cha familia nzima hupikwa katika chungu kimoja. Wanaume hupakuliwa chakula kwanza, kisha watoto na mwishowe wanawake. Hali hii hudhihirisha wazi nafasi ya mwanaume katika kitengo kidogo cha jamii (familia). Kwani, kwa mujibu wa utamaduni wa Abakuria mwanamke huwa wa mwisho kukaa chini na kula.

Kwa upande mwingine, kijana wa kiume ambaye ameoa kwa muda ana uhuru wa kuhama kutoka kwa boma la babake na kujenga mji wake. Utengano wa aina hii huitwa *Okohoka.* Hali hii humfanya kijana huyu kuwa huru na kujitegemea katika kutosheleza mahitaji yake na ya familia yake. Hii ni ithibati mahususi ya kupanuka kwa jamii, hali ambayo hupokelewa kwa njia chanya na jamii.

Abakuria hufungamanishwa na uhusiano wa kanuni mbili, walizozitambua na kuzithamini, jadi moja na kuishi katika himaya moja. Kanuni hizi hazikuwasaidia tu katika kuwapa mtazamo mmoja wa kijamii na kisiasa bali kuumba mtazamo wao wa kilimwengu. Imani kwa kanuni hizi ni malighafi mwafaka ya ujenzi wa tamaduni, itikadi, mielekeo na matarajio ya Abakuria.(Tobisson ,1980.69)

Kila mbari iligawika katika vitengo vilivyojulikana kama (ibisaku). Ndani yake ni watu waliotambulishwa na uhusiano wa kiukoo. Chini ya kitengo hiki ni (amagiha) ambacho watu wake walikuwa na uhusiano wa karibu sana kuliko wale wa (ibisaku). Chini zaidi ni kitengo cha (eka) ambacho kilikuwa cha msingi, kitengo hiki kilijumulisha baba na vijana wake wa kiume. Katika vitengo hivi vyote uongozi, mamlaka na madaraka yalipewa mwanaume, hali ambayo huhalalishwa na mpangilio huu wa jamii. Aidha, mwanaume hujitokeza kama mwenye nguvu na uwezo mkubwa kuliko mwanamke. Uhusika wake ni muhimu na huthaminiwa zaidi katika jamii (Chacha, 1999).

Sifa bainifu za utamaduni wa Abakuria ni (Amakora) mpangilio wa jamii kwa mfumo wa vizazi na wa rika (ichisaiga). Mfumo wa vizazi hujumuisha mfumo wa ruwaza wa mahusiano ya wanajamii na hubainisha hadhi ya kila mwanajamii. Kuna vizazi vinane ambavyo vimegawika katika jozi mbili zenye vizazi vinne kwa kila moja. Vizazi hivi in sambamba na kila kizazi huja baada ya kingine hadi kukamilika kwa duara. Duara la vizazi vya Abakuria huchukuwa miaka 100 hadi 112 (Tobisson,1986:114 na Mwita 2005:67-69). Jozi hizi in *Monyasae* na *Monyachuma*. Monyasae ilijumulisha; Abasae, Abanyamburiti, Abagamunyeri na Abamaina, ilihali Monyachuma ilijumisha, Abamairabe, Abagini, Abanyangi na Abachuma. Watoto wa mwanaume katika kizazi fulani walistahili jina la kizazi kilichofuata. Urejeleo wa mifumo hii ya kizazi ulikuwa kwa wanaume, hivi kwamba wanawake walifuata jina la kizazi cha mume wake. Hivyo basi utambulisho na hadhi ya mwanamke ilijengwa mintarafu ya mume wake, hali ambayo inabainisha kuwa mwanamke alikuwa milki ya mwanaume katika jamii hii ya Abakuria (Abuso 1980;98).

Viongozi na wanachama wa mabaraza ya jamii walikuwa ni wa kutoka kizazi kikubwa katika jamii. Wao ndio waliotoa ushauri na uamuzi kuhusu maswala mbalimbali katika jamii. Ni bayana kuwa katika jamii ya Abakuria, kila mwanajamii anatambua jina la kizazi chake . Hali hii husaidia kila mwanajamii kujua njia bora ya kuhusiana na wengine. Mahusiano baina ya wanajamii katika sherehe mbalimbali yaliongozwa na mfumo huu. Hivyo, ruwaza za vizazi ni

vitengo muhimu vilivyotawala takribani kila hali, tabia, na vitendo ndani ya jamii. Muundo na mwelekeo huu umejengwa kutokana na urithi wa kihistoria na uhalisia wa kijamii ambao ni ithibati mwafaka katika ujenzi wa ngazi za kijinsia zinazohalalisha uwezo na mamlaka ya jinsia ya kiume.

Mfumo mwingine wa mpangilio wa jamii ya Abakuria ni ule wa hirimu, (ichisaiga). Waliotahiriwa katika kipindi kimoja walipewa jina maalum la rika lao. Urejeleo wa mwanamke ulizingatia rika ya mume wake, kwani kwa Abakuria, *te mokari ana saiga* (mwanamke hana rika). Majina ya rika ni sehemu muhimu katika utamaduni wa Abakuria hasa zaidi katika kuonyesha utaratibu wao maalum wa kupanga miaka na matukio. Kila rika lilipewa jina kutokana na tukio maalum lililotokea katika kipindi au kabla ya tohara. Kwa hivyo, ni kumbukumbu mwafaka katika kujenga historia ya matukio mahususi katika jamii.

Mifumo hii miwili ilitumiwa na jamii ya Abakuria katika kuimarisha umoja wao na kuwapa mwelekeo mahususi juu ya mahusiano yao. Aidha, ni muhimu kutaja kuwa mifumo hii miwili ilimrejelea zaidi mwanaume kuliko mwanamke, kwani jinsia ya kike inajitokeza kama jinsia tegemezi yenye kumilikiwa na jinsia ya kiume. Matokeo ya mifumo hii miwili ni kuhalalisha uwezo, nguvu na mamlaka ya mwanaume, hali ambayo ni ithibati mwafaka ya ujenzi wa uume katika jamii ya Abakuria.

4.5.2 Siasa na Utawala

Jamii ya Abakuria imegawika katika mbari ndogo kama kitengo maalum cha utawala. Mbari ilijengwa kutokana na kundi la wanajamii wa mlango mmoja wenye uhusiano wa karibu wa kifamilia. Mbari hizi zilijulikana kama "ibiaro" ambazo zilikuwa ni vitengo vikuu vya kisiasa na kiutawala. Aidha mbari zilikuwa vitengo maalum vya ulinzi na nguvu za kijeshi. Katika kila mji nyumba zilijengwa kwa jinsi ambavyo ziliimarisha ulinzi. Wanaume walitakikana kushiriki vikamilifu katika siasa, utawala na ulinzi wa mbari na jamii kwa jumla.

Katika karne ya 19 Bukuria ilikuwa imegawika katika majimbo (ibiaro). Haya yalikuwa maeneo yaliyojengeka kutokana na viwakilishi vya ishara za wanyama fulani. Wanajamii waliojitambulisha na ishara ya mnyama fulani waliishi katika jimbo mahususi. Ni muhimu kutaja kuwa kata za siku hizi za Bukuria zimejengwa mintarafu ya majimbo haya. Kila jimbo lina baraza la kiutawala 'irritongo'. Majadiliano yote yanayohusu maendeleo yao yalijadiliwa na baraza hili. Baraza hili liliundwa na idadi mahususi ya wanaume kutoka kwa kila mbari

(Tobisson 1980). Wanawake hawakushirikishwa katika baraza hili. Hivyo basi; ni wazi kuwa mwanaume hupewa nafasi pana ya kisiasa na kiutawala katika jamii, kwa sababu hii, mwanaume miongoni mwa jamii ya Abakuria ni mtawala ambaye hustahili kuongoza jamii takribani katika maswala yote yanayohusu maendeleo na uhai wa jamii.

Aidha, katika mpangilio wa kisiasa wa Abakuria kuna halmashauri ya siri (Abagaka ba ikimira) ambayo hujengwa kutokana na wazee wenye haiba mintarafu ya umri wao mkubwa na tajriba yao kuhusu maisha. Halmashauri hii hushirikisha wanaume wa umri takribani kati ya miaka ishirini na thelathini kama hakikisho la uendelezi wa halmashauri hii. Wanachama wa halmashauri hii ni wasimamizi na wadhibiti wa nidhamu. Vilevile, wana mamlaka ya kuamuru vikwazo na adhabu kwa yoyote yule ambaye kwa njia moja au nyingine anahatarisha usalama wa jamii kwa vitendo au kwa tabia. Wanachama wa halmashauri hii ni wanaume pekee.

4.5.3 Maafikiano na Uamuzi Katika Jamii

Wanawake hawakuhusishwa katika baraza lolote la jamii ambalo lilihusika katika kuleta maafikiano dhidi ya maswala mbalimbali ndani ya jamii. Aidha sehemu kubwa ya uamuzi katika familia na jamii kwa jumla ilitekelezwa na wanaume. Hali hii huchangia pakubwa katika kumpa mwanaume nguvu, uwezo na mamlaka makubwa miongoni mwa jamii ya Abakuria. Katika mikutano ya mabaraza ya jamii wanawake wanahudhuria kusikiliza tu na wala si kuongea kwani utamaduni wa jamii ya Abakuria haumruhusu mwanamke kuzungumza mbele ya wanaume; hii ni kwa sababu rai zao hupuuzwa sana na wanaume. Katika matukio mengi mwanamke anaposimama kuongea, wanaume huguta kwa kusema;

> *'Eh! Te mosaacha a hano agasumacha'*
> Eh! hakuna mwanaume hapa wa kuzungumza"

Hali hii imewafanya wanaume katika vijiji vingi kukubaliana kwamba hamna sababu yoyote ya wanawake kuhudhuria mikutano ya mabaraza ya kijiji, hasa wanapojadili kuhusu maswala nyeti ya kijamii kijijini. Wanaume mara nyingi husema wanawake wana kazi zingine za kufanya nyumbani, mfano kupika na kuwalea watoto. Aidha huaminika kuwa wanawake hawana uwezo wa kutunza siri.

Uhusika mpana wa wanaume katika mikutano hii, ni kielelezo mwafaka cha ujenzi wa uume katika jamii ya Abakuria. Aidha ni ithibati muhimu ya jinsi ambavyo hoja na maamuzi ya mwanaume huthaminiwa zaidi katika jamii. Hali hii huibua matarajio na mielekeo tofauti ya jamii kumhusu mwanamume na mwanamke.

Serikali na utawala wa Abakuria, imejengwa kwa mhimili imara wa utamaduni thabiti, unoaruhusu majadiliano kuhusu maswala mbalimbali hadharani. Kuanzia maswala madogomadogo yanayohusiana na ugomvi wa kifamilia hadi shida na mashaka ya jamii nzima. Mara kwa mara, mikutano ya kijamii huandaliwa kuanzia kwa mbari hadi jamii nzima. Maoni ya umma katika mikutano hii ni uamuzi wa mwisho wa kundi dogo la wanaume waadhama wenye hulka maalum, mfano wasemaji wa mbari, nabii na viongozi wa vita wenye maarifa na tajriba katika uwanda wa sheria na maswala mbalimbali ya kijamii. Hadhira katika mikutano ya aina hii haikuruhusiwa kuongea wala kutoa maoni yoyote katika mikutano ya kutatua kesi zinazohusu mashauri ya kisheria. Hivyo basi, ni dhahiri shahiri kuwa wanaume wanajitokeza kama viongozi, watawala na wenye madaraka makuu katika uhalisia wa kijamii. Mawazo na uamuzi wao hupokelewa na jamii bila pingamizi, hivi kwamba tajriba na matarajio yao ni viambajengo muhimu vya nguvu na uwezo wao katika jamii ya Abakuria.

Kila mbari ilikuwa na kiongozi wake (omogambi). Huyu alikuwa mwanaume mwenye umri mkubwa ambaye aliongoza mikutano ya kijamii, kisiasa na ya kidini. Alipewa mamlaka na jamii ya kuamua juu ya maswala mbalimbali ya kijamii aidha alishirikishwa katika baraza la wazee (inchama)

4.5.4 Dini na Imani Andamizi

Abakuria walikuwa na Mungu wao waliomrejelea kwa majina mbalimbali, kwa mfano; *Rioba, Enokwe, Gekoni, Getemi, Mosacha Obiaro, Keng'ori na Nyamohanga* (Abuso 1980: 159). Huyu Mungu wao aliaminika kuwa kila mahala, mkarimu na aliyejaa wema. Aliwakilishwa na "Rioba" jua ingawa hakuwa jua halisi. Rioba humaanisha jua, ambaye ni muumbaji wa kila kitu, ambaye ana wajibu wa kubariki watu wake, kwa kuwakirimia wanaume uwezo wa uzazi, mvua kwa mazao na mifugo. Wakuria waliamini kuwa Mungu hakuwa tayari kwa njia yoyote kuwadhuru watu wake.

Chini yake kulikuwa na mawakali wawili muhimu ambao waliabudiwa mara kwa mara kama daraja kati ya Abakuria na Mungu wao. Walijulikana kama *Abakoro* (mizimu) na *ibihwe* (mizimu habithi/pepo wabaya). Matakwa yoyote madogo ya Abakuria kwa Mungu wao yalipitishwa kupitia kwa *Omokoro(*mwanzilishi wa mbari). Kafara nazo kwa Rioba zilipitia kwa *Omokoro.* Sherehe za kutoa kafara kwa Rioba ziliongozwa na wanaume; wanawake walikuwa wapishi tu. Hii ni ithibati mwafaka ya kuonyesha nafasi muhimu ya mwanaume katika maswala ya imani za kidini, ambayo ni daraja kati ya jamii na miungu ya jamii. Waliaminika kuwa na hekima ya kutambua uhitaji wa kafara, walikuwa mstari wa mbele katika matayarisho na utekelezaji wa sherehe nzima. Mtu mwenye cheo kikubwa katika sherehe za utoaji wa kafara alijulikana kama *Omoraguri.* Huyu alikuwa mwanaume na kuhani mkuu. Ndiye aliyekubali kafara kutoka kwa jamii na kuwashauri juu ya waliyopaswa kutekeleza katika kipindi cha magonjwa au balaa yoyote kwa jamii.

Kwa sababu ya uhitaji wa umoja na uelewano katika jamii, kuna sheria za kidini ambazo kila mwanajamii anapaswa kuzitii. Sheria hizi hazikuhitaji uwepo wa koti. Hizi zilikuwa kanuni za kidini ambazo zilipaswa kushurutisha utiifu. Uvunjaji wake uliaminika kuleta balaa kwa mkosaji na familia yake. Mwanaume kama nguzo na kiongozi katika familia alipaswa kuhakikisha kuwa mke wake na watoto wake wanatii miiko na imani za kijamii. Nafasi hii ya mwanaume ya utekelezaji wa wajibu huu ni ya kiitikadi ambayo inabainisha imani, mielekeo na matarajio ya utamaduni wa jamii katika kumpa mwanaume nguvu, uwezo na mamlaka ya juu katika shughuli muhimu za kijamii.

4.5.5 Shughuli za Kiuchumi za Abakuria

Shughuli za kiuchumi za Abakuria zinashirikisha ukulima na ufugaji. Wao ni mfano mwafaka wa kundi la watu ambao hadi sasa wanashikilia mtindo mseto wa uzalishaji mali. Zamani kidogo,kulikuwa na koo ambazo zilijihuzisha na uwindaji katika uchumaji wao wa riziki. Hawa walikuwa wakiwinda wanyama pori katika pori ya Serengeti na Maasai-mara. Kutokana na kampeni za uhifadhi wa wanyama pori, wawindaji wameachwa bila njia nyingine ya kujipatia riziki, hali ambayo imewalazimu kushiriki ukulima na ufugaji. Vikozi vya askari vimewekwa katika mbuga hizi ili kuhakikisha kuwa hakuna uwindaji haramu. Utanzu wa nyiso za jando miongoni mwa Abakuria umetumiwa kikamilifu katika kuwakanya mashujaa wa Abakuria juu ya uwindaji haramu:

Abamura bawaito muyi ng'ora
Ichitinyi chaya aharai
Abagemu mbabaita nichinkong'u
Mutige abasino kunyanyi

Vijana wetu wa kiume mwende polepole
Wanyama wa pori wameenda mbali
Walinzi watawaua kwa silaha kali
Muwaache wajane kwa shida kubwa

Hali ya kuwaacha wajane kwa shida ni ithibati mwafaka ya kubainisha wajibu wa mwanaume kama mkimu familia. Uwindaji ni shughuli ya kiume, ambayo huhitaji ujasiri, na kujitolea kwa mwanaume katika kutosheleza familia yake kwa hali yoyote ile.

4.5.5.1 Ufugaji wa Ng'ombe

Abuso (1980) anasema; utamaduni wa Abakuria ni zao la mchanganyiko wa tamaduni tofauti, kwa mfano tamaduni za Wamasai, Wakisii, Wakalenjini na Wajaluo. Athari kutoka kwa Wabantu ambao shughuli yao muhimu ni ukulima na vilevile athari ya wanailotiki ambao ni wafugaji ndizo zimewafanya Abakuria kuwa wafugaji na wakulima. Mchanganyiko huu wa utamaduni ulianzia enzi ya vizazi vya awali vya Abakuria. Wakazi wa kale katika eneo la Bukuria walijishughulisha na ukulima na ufugaji, hali ambayo iliwafanya kuhama kutoka eneo moja hadi lingine. Ni kutokana na hali hii ambapo Abakuria wamekuwa na mwelekeo wa uzalishaji mali mseto kuanzia zama hizo hadi leo. Aidha hali hii imewapa mwelekeo mahsusi wa maisha yao ya kiuchumi, kisiasa, kitamaduni na kijamii. Kwa kilimo Abakuria wanafananishwa na Wakisii na Wajaluo ilihali kwa ufugaji wa mifugo waliiga mengi kutoka kwa Wamasai, Wazanaki na Wanguruimi (Chacha 1999)

Kama Wamasai, vijana wa kiume wa Abakuria hususurika katika eneo pana lililo wazi na mifugo yao kwa kutafuta malisho mazuri na miamba ya chumvi kwa ajili ya mifugo wao. Kutokana na uvamizi wa mara kwa mara kutoka kwa majirani wao, hasa Wamasai, Wanguruimi na Wakalenjin, kundi la vijana hawa hujihami kwa mikuki, pinde na mishale ya sumu wakiwa tayari kukabili ushambulizi wowote kutoka kwa maadui wao. Wakiwa katika hali hiyo, huandamana na mifugo yao ili kupatiana ulinzi kamili dhidi ya washambulizi kutoka kwa jamii

jirani. Ilihitaji uangalifu wa wanaume na kujihami na zana mbalimbali za kivita katika kulinda mifugo, familia na jamii kwa jumla dhidi ya ushambulizi kutoka kwa maadui wao usiku na mchana. Hali hii hujenga matajario ya jamii kumhusu kila mwanaume na mwelekeo wa jamii ya Abakuria huhalalisha vitendo vya ushari na unyang'ganyi wa kimabavu.

Kwa kudhukuru idadi ya kadhia ambamo taswira ya ng'ombe hubainika katika nyiso za jando, ni bayana kuwa ufugaji wa ngombe huchukua nafasi ya kati katika maisha ya Abakuria. Ni kweli kwamba, ni kutokana na uchungaji na ulinzi wa ng'ombe ambao hukuza na kuleta uhasama na vita baina ya Abakuria na Wamasai. Jamii hizi zote hushikilia imani sawa juu ya umilikaji wa ng'ombe, hasa kutokana na sababu za kihistoria, kiitikadi na za mazingira ya uhamaji wao.

Ng'ombe huauni Wakuria kwa maziwa, nyama, ngozi na ndiyo sehemu kubwa ya mahari. Maksai hutumiwa katika kutekeleza kazi ngumu kama kulima na kusaidia, kubeba mizigo. Kutokana na manufaa haya, kila familia ya Abakuria hujaribu kwa njia zozote kuwa na kundi kubwa la ng'ombe, kwani ni ishara ya utajiri na hadhi ya juu. Hivyo basi, ni kutokana na ukweli huu wa muktadha wa kijamii, ambapo ng'ombe ni mifugo wa kutegemewa na umuhimu wake hubainika katika sherehe mbalimbali za Abakuria. Kwa mfano, tohara (esaro), arusi (enyangi), kafara (ibimwenso) miongoni mwa zingine. Pale ambapo ng'ombe hawarejeliwi moja kwa moja, hutajwa kwa mhemko mkubwa kupitia kwa tamathali nyingi za usemi katika baadhi ya nyiso. Kwa mfano, utamaduni wa Abakuria ulihalalisha uvamisi na kupora ng'ombe kutoka kwa Wamasai; aidha, uvamizi huu ulitumiwa kama sharti kwa vijana wa kiume katika kuonyesha ushujaa wao katika jamii. Shujaa wa Abakuria alibainisha ujasiri na ushari wake kushambulia na kupora ng'ombe kutoka kwa maadui wao. Hii ilikuwa njia mojawapo ya vijana wa kiume kujipatia mahari. Hali hii inabainika bayana kupitia kwa nyiso ifuatayo:

Abakare bawaito ibohera
tui guchisora Rongararo
hara chikorara icha ababisa
chabo kiburuha na nyamahara
chaibora amatena amatebega
chitore Bwirege kobamura
chiche kubakinia abake bano

mashujaa wetu jitayarisheni
twende kuwafuata ng'ombe Rongararo
pale wanapolala ng'ombe wa maadui
hudhurungi na wenye mabaku
wanaozaa ng'ombe mahuluti na wanene
waje Bwirege kwa mashujaa
wawakuze watoto wetu wachanga

Kutokana na thamani kubwa ya ng'ombe kwa Abakuria, utamaduni wao huhalalisha vitendo vya uvamizi na kuwapora maadui wao ng'ombe. Hii ni kwa sababu itikadi na imani za Abakuria, huwafanya mashujaa wa Abakuria kuamini siku zote kuwa jamii yao ndiyo ina haki ya kumiliki ng'ombe. Imani hii vilevile ipo katika jamii ya Wamaasai.

Miongoni mwa jamiii ya Abakuria, ng'ombe ni mali ya mwanaume na ni ishara mwafaka ya utajiri na hadhi yake katika jamii. Aidha ng'ombe miongoni mwa Abakuria ni kibadilishio wastani na hutumiwa kama akiba ya thamani. Ng'ombe huchukua nafasi kubwa ya mahari. Hivyo, ndiyo malipo mwafaka ya mwanamke katika jamii. Malipo ya mahari kwa msichana kutoka jamii maskini, ni ishara ya kumtoa babake kutoka kwa lindi la umaskini. Kwa hivyo, ni bayana kuwa mwanaume huwa na wajibu mkubwa na muhimu sana katika ufugaji wa ng'ombe (kuchunga, kuchinja na kutayaraish ngozi, kujenga na kudumisha zizi la ng'ombe. Kukamua na kuhakikisha usafi wa zizi ni majukumu ya kike. Watoto wadogo huchunga na kulinda ndama.

Pamoja na ufugaji wa ng'ombe, Wakuria vilevile wanafuga, mbuzi, kondoo na kuku. Mbuzi na kondoo walikuwa miliki ya mwanamume ilihali kuku ni mali ya mwanamke na watoto. Hali hii hubainisha kiasi cha mamlaka na uwezo wa mwanamke akilinganishwa na mwanamume.

4.5.5.2 Ukulima

Abakuria walijihuzisha na ukulima wa mahindi, mihogo, mtama, wimbi na mboga za kienyeji. Kazi za kilimo ambazo zilichukuliwa kuhitaji nguvu nyingi zilihuzishwa na wanaume; mfano kukata miti kung'oa viziki, na kufyeka nyasi. Hali ambayo humsawiri mwanaume kama mwenye uwezo na nguvu zaidi ya mwanamke. Kulima kwa kutumia mikono ni kazi ya wote

wawili (mwanamume na mwanamke). Upanzi, kupalilia, kuvuna na kusafirisha mazao kutoka shambani hadi nyumbani ni kazi za kike (Tobisson 1980;84).

Fikra zinazohusu majukumu ya kike na ya kiume katika uzalishaji mali ni kutokana na misingi ya imani zinazozingatia tofauti za kiuwezo hasa kutokana na tofauti za kimaumbile kati ya mwanamume na mwanamke, aidha, tofauti za nguvu katika kutekeleza baadhi ya majukumu. Hali hii humfanya mwanaume kuwa na mamlaka zaidi ya mwanamke katika umilikaji wa raslimali za kimsingi za jamii. Uwezo mkubwa wa mwanamume katika uzalishaji mali hutokana na ugawaji wa majukumu, hivi kwamba ufugaji wa wanyama mfano ng'ombe, mbuzi na kondoo ni majukumu ya kiume. Kutokana na thamani kubwa ya ng'ombe na mifugo kwa jumla miongoni mwa jamii ya Abakuria, mwanaume hujitokeza kuwa na hadhi kubwa kuliko mwanamke.

Miongoni mwa Abakuria kuna Kisasili kinachoeleza asili ya mwainisho huu wa uwili mintarafu ya majukumu ya ufugaji na ukulima. Visasili vingi husimulia kuwa awali mwanamke ndiye aliyemiliki ng'ombe hadi pale aliponyang'anywa haki hii na wanaume kutokana na ujanja wa wanaume. Hii ndiyo sababu hadi leo wanaume huhusika katika kutekeleza baadhi ya majukumu ya kilimo. Matokeo ya maelezo kutokana na visasili hivi ni kwamba wanawake walikosa nguvu muhimu ambazo ni za kimsingi ndiyo maana ikawa rahisi kupinduliwa na wanaume (Chacha,1999).

4.5.5.3 Biashara

Biashara kama sehemu moja ya uchumi wa Abakuria ilitekelezwa kwa umoja na utangamano. Mtindo wa ubadilishano wa bidhaa ulitumika, hivi kwamba mwenye kiasi fulani cha wimbi angebadilishana na mwenye kiasi sawa na chake cha mihogo. Biashara ya faida kubwa ilikuwa ya wanaume ilihali wanawake walishughulika na bidhaa za mapato madogo na zenye kuharibika haraka, kwa mfano mboga. Ilikuwa ni kawaida mwanaume kubadilisha ng'ombe kwa zana za kivita au nafaka kwa ajili ya kulisha na kukimu familia yake. Masoko vilevile yalitenganishwa kwa misingi ya kijinsia mintarafu ya eneo, kiwango na wakati. Wanawake walijihusisha na bidhaa za faida ndogo, kiwango kidogo katika masoko yaliyo karibu na nyumbani. Wanaume walijihusisha na biashara za mali nyingi na mazao yenye faida kubwa. Walipelekea bidhaa zao katika masoko makubwa ya kimikoa kwa mfano Tagota na

Kilgoris(Mkoa wa Ponde la Ufa). Hivyo basi, ni bayana kuwa shughuli za kibiashara za wanaume ni pana, anuwai na zenye faida kubwa kuliko biashara ya wanawake.

Ni kutokana na hali hii ambapo mwanaume wa Abakuria humiliki uwezo mkubwa wa kiuchumi zaidi ya mwanamke. Uwezo ambao humpa nguvu na nafasi ya kutawala, kuwa na mamlaka na kuwa kitovu cha uamuzi katika familia na kwa jamii. Aidha uwezo huu humwezesha kuwa nguzo katika kukimu familia yake.

4.6 Hali ya Jamii ya Abakuria, Leo

Jambo linalodhihirika katika jamii ya Abakuria ni kwamba kuna mabadiliko mengi ambayo yametokea hadi hivi leo. Baadhi ya mabadliko haya ni yale ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Mabadiliko haya yamechochewa na athari za elimu na dini za kimagharibi. Athari za majirani pia. Mfumo wa ndoa na tohara umebadilika sana, kwa upande wa tohara watoto sasa hutahiriwa wakiwa na umri kati ya miaka 7 na 9. mtindo unaotumiwa ni ule wa kuwapeleka hospitalini na hawawekwi jandoni. Aidha, uposaji na ndoa unebadilika pia,.ndoa nyingi za siku hizi hufuata misingi ya kidini.

Nyiso za jando kama tanzu zingine za fasihi ya Abakuria hazikupeuka usasa huu, kwani kuna baadhi ya matumizi ya maneno katika nyiso yanayobainisha athari ya maendeleo haya ya kilimwengu, mathalan, kalamu, mwavuli, seng'enge na bunduki (katika sura ya tano).

4.7 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili kwa kina historia simulizi ya jamii ya Abakuria na mchango wake katika kumpa mwanamume sura mahususi. Aidha tumejadili matarajio, miiko, mielekeo, mila na desturi ambazo huandamana na kila awamu ya maisha ya mwanamume tangu kuzaliwa kwake hadi kifo chake. Matokeo yake ni kwamba katika awamu hizi zote, mwanamume husawiriwa kwa njia chanya, hivi kwamba utamaduni na matarajio ya jamii humpa mwanaume thamani kubwa katika jamii. Katika mchakato mzima wa kukua kwa mwanamume, jamii humjamiisha kwa jinsi ambavyo anaishi katika jamii kutetea na kuhifadhi hadhi yake kama mwanamume, hutekeleza majukumu ya kiume na kuepuka yale ya kike. Thamani na hadhi hii ni sehemu muhimu ya mwanamume kutoka anapozaliwa hadi kifo chake. Vilevile, katika sura hii tumejadili

mifumo ya kijamii, kisiasa, kidini na ya kiuchumi katika jamii ya Abakuria.Imebainika kwamba mwanamume hujitokeza kama binadamu mwenye uwezo na nguvu, mwenye mamlaka ambaye uamuzi wake huthaminiwa sana. Aidha, mwanaume humiliki takribani nyenzo zote za uzalishaji mali, hali ambayo humfanya kuwa mkimu-familia na mwenye uwezo wa kutosheleza familia na jamii yake kwa mahitaji ya lazima na ya ziada. Aidha, inabainika kuwa mwanamke ni sehemu ya milki ya mwanaume. Kwa upande wa majukumu, mwanamume hutengewa majukumu ya sulubu, yanayohitaji nguvu nyingi. Kwa upande wa siasa na utawala, mwanaume hutunukiwa nafasi muhimu ya kuongoza na kutawala, hali ambayo humsawiri kama kichwa au nguzo ya familia na jamii kwa jumla. Hali hii hutokana na imani kwamba mwanamume huhodhi akili na hekima ya juu kuliko mwanamke.

SURA YA TANO

MWANAMUME KATIKA NYISO ZA JANDO

5.1 Utangulizi

Katika sura hii tunachanganua deta tukizingatia madhumuni ya utafiti wetu chini ya mwongozo wa misingi ya nadharia za utafiti tulizozichanganua. Lengo letu lilikuwa kujadili sura ya mwanaume inavyojitokeza katika nyiso za jando. Aidha, tumeeleza kwa uwazi jinsi viambajengo vya lugha "taswira" katika nyiso za jando vinavyomsawiri mwanaume. Kutokana na sura ya nne ni wazi kwamba utamaduni ni mchango mkubwa katika kujenga, kukuza na kuhalalisha mielekeo, itikadi na matarajio ya jamii kuhusu mahusiano ya jinsia ya kike na ya kiume. Vpengele vitakavyozingatiwa katika uchanganuzi huu ni: maumbile, saikolojia, uchumi na utamaduni wa kijamii. Kwa mujibu wa Magayu (1977) anasema

Fasihi ni kielelezo cha hali halisi ya maisha. Kama kioo, mara nyingi huwa inamulika sehemu fulani ya maisha ya mtu binafsi na kundi la watu na uhusiano wao na mazingira yao.

Nyiso za jando ni mojawapo ya tanzu muhimu za fasihi simulizi miongoni mwa jamii ya Abakuria. Umuhimu wake ni bayana mintarafu ya thamana ya tohara ya vijana wa kiume katika jamii ya Abakuria. Sherehe za tohara hupewa umuhimu wa haja, kwani ndizo hubaini mwisho wa utoto na mwanzo wa utu-uzima. Hivyo basi, nyiso za jando kama kipengele muhimu katika sherehe hizi hubainisha utamaduni, itikadi, mitazamo na mielekeo ya jamii, kuwahusu vijana ambao wanajitayarisha kutahiriwa, wakati wa shughuli ya tohara na baada ya kutahiriwa. Kama wasemavyo Warren na Wallek (1949:94).

> ...lakini zaidi ya hayo, fasihi huwakilisha maisha; na maisha kwa kiwango kikubwa ni uyakinifu wa kijamii. Hakika kwa kawaida fasihi imeibuka kwa uhusiano mkubwa sana na asasi mahususi za kijamii (tafsiri yetu).

Nyiso za jando ni zao la historia, mazingira, utamaduni na jumla ya maisha ya jamii ya Abakuria na shughuli zao. Ni sehemu mojawapo ya utamaduni wao. Aidha, ni muhimu kutaja kuwa utamaduni wa jamii husika huchangia falsafa ya jamii, mielekeo na mtazamo wa maisha.

Malighafi ya nyiso za jando miongoni mwa jamii ya Abakuria ni; mazingira yao maalum, historia yao, mambo ya asili, wanyama, mimea, itikadi, mitazamo ya jamii na matarajio yao kuhusu kila mwanajamii. Hali hii hulazimu hadhira kuwa na uelewa wa vitu hivi ili kufasiri maana mwafaka ya nyiso hizo. Kwa hivyo, zinapotumika nje ya mazingira yake, thamani yake hupungua kwa kiasi kikubwa na maana yake huweza hata kupotea.

5.2 Taswira za Kisaikolojia

Taswira hizi hutokana na fikra za wanaume na jamii kwa ujumla juu ya nafasi ya mwanaume katika jamii. Fikra hizi hujenga imani kwamba mwanaume huwa na nguvu na uwezo wa kuamuru, kutawala, kuongoza, kulinda na hasa zaidi ana akili na hekima ya juu katika kutekeleza majukumu yake katika jamii. Imani hizi ni kipengele muhimu kinachotumika katika ugawaji wa majukumu katika jamii. Ni dhahiri kuwa mwanaume ametengewa kazi zinazohitaji nguvu nyingi, na pia akapewa jukumu la kuiongoza na kuikimu familia yake. Mwanamke naye amepewa jukumu la kuitunza familia, kulea na kuwafunza watoto.

5.2.1 Taswira ya Jiwe

Mwanaume husawiriwa kama jiwe wakati wa tohara, hivi kwamba sharti awe mgumu mfano wa jiwe, ajihami na kuwa imara wakati anapotahiriwa. Asionyeshe hisia za uchungu wala maumivu wakati anapopashwa tohara. Hii ni kwa sababu, kuonyesha hisia hizi ni dalili ya kulia au uoga. Ni mwiko kwa kijana wa kiume kulia au kuonyesha dalili zozote za kulia wakati anapotahiriwa. anapaswa kusimama wima bila kutingizika, bila kuonyesha ishara yoyote ya kuhisi maumivu kwa uso au macho. Swala hili liliwapa dukuduku wale waliompeleka kutahiriwa, wazazi wake na jamii kwa jumla. Kulia kulibainisha uoga, kitendo ambacho ni kinyume cha matarajio ya jamii kuhusu mwanaume. Aidha, ni kitendo ambacho matokeo yake ni fedheha kwa familia yake na kwa jamii nzima. Ilibidi baba mzazi wa mvulana huyo kutozwa faini ya ng'ombe au idadi fulani ya mbuzi ijapo angelia. Kwa sababu ya wasiwasi huu kila kijana wa kiume huhitajika kutoa hakikisho kuwa atasimama imara kutetea ushujaa wake na kuonyesha kuwa yuko tayari kuhimili uchungu au maumivu yoyote yale. Kwa kufanya hivyo, hujifananisha na jiwe ambalo halina hisi zozote.

Baaba wanyiboye ikara ogome
Nkagena waiboye akahiku
Agasachasacha

Mamangu kaa utulie
Ulikazaa kajiwe ambako kamekomaa
Mwanaume kamili na imara

Taswira hii ya jiwe hubainisha sifa za ushujaa, ushapavu, uvumilivu na uimara ambazo mwanaume hustahili kuwa nazo kama sehemu muhimu ya kudumisha nguvu ya kiume. Aidha hisia za, maumivu, uoga, furaha na uchungu ni za kike na mwanaume sharti ajiepushe nazo kwa hali yoyote kwa minajili ya kudumisha utambulisho wake kama mwanamume. Udogo wa jiwe katika nyiso hii ni ishara ya ugumu wa kuvunja kajiwe kadogo katika vipande vidogo zaidi.

5.2.2 Taswira ya Kuni na Ua

Miongoni mwa jamii ya Abakuria kijana ambaye hajatahiriwa huitwa "umurisia" ilihali aliyetahiriwa huitwa "umumura". Umurisia husawiriwa kama "kuni" ilihali umumura husawiriwa kama "ua imara". Katika hali halisi, faida ya kuni ipo tu kwa kuwasha moto; hivyo basi, faida yake huwa haba na huweza kuteketezwa na kuwa jivu na kusahaulika kabisa. Ilihali "ua" huwa na thamani kubwa kuliko "kuni" kwani ni ishara ya ulinzi thabiti, hubainisha mpaka na hufanya mji kuwa wa kupendeza. Thamani kwa kijana wa kiume ambaye hajatahiriwa ilikuwa ya chini kuliko yule ambaye ametahiriwa. Taswira ya "kuni" hubainisha sifa zifuatazo: iso na uhai, iso na thamani, iso na umuhimu miongoni mwa sifa zingine. Mvulana ambaye hajatahiriwa haruhusiwi kuoa, kushiriki tendo la ngono, kuwa na mji, kumiliki shamba au hata kupewa nafasi kuzungumza mbele ya watu wazima, kwani mawazo yake huchukuliwa kuwa ya kitoto. Ilihali kijana wa kiume aliyetahiriwa huwa ameingia kwenye kundi kubwa la wanaume na manufaa yake katika jamii ni bayana. Baada ya kutahiriwa kijana wa kiume huwa yuko huru kuoa na kuanzisha familia yake, kwani ndoa ni asasi muhimu ambayo ni hakikisho la kuendelea kwa jamii kiuzazi. Aidha taswira ya ua imara huashiria kuwepo kwa wanaume mashujaa katika familia au katika jamii.

Taata waya orantoka iga amatabore
Nauni ndagotebia iga ningitire
Mona obori boo ubuya bono

Baba umekuwa ukinilinganisha na kuni
Nami nakwambia mimi ni ua imara
Kama hili zizi lako zuri

Uimara wa ua unamithilishwa na zizi la ng'ombe. Katika jamii ya Abakuria. Zizi la ng'ombe lilijengwa kwa miti imara, migumu na isiyooza hivihivi. Mwanya haukuachwa ila tu uwazi wa mlango wa kupitia ng'ombe na mifugo wengine. . Taswira hii huashiria nafasi ya mwanaume katika jamii kama mlinzi wa familia yake na wa jamii nzima, kama vile zizi lilivyo imara na bila mwanya. Mwanaume wa Abakuria hutakikana kuwa shupavu na mwenye kujiamini kwa hali yoyote ile katika kulinda jamii bila uoga wowote ule. Na asiache nafasi yoyote ile kwa jamii kuvamiwa na maadui au shida yoyote ambayo inaweza kuzuiliwa na uwezo na nafasi yake kama mwanaume katika jamii.

5.2.3 Taswira ya Mjumbe

Mwanaume husawiriwa kama mjumbe wa jamii, ambaye sharti awe tayari na kwa hali yoyote kutekeleza wajibu huu kwa manufaa ya familia yake na jamii kwa jumla. Baada ya kutahiriwa, kijana wa kiume huwa amepiga hatua; baada ya jando, hujiunga na kundi la wanaume katika jamii. Hivyo basi kwa hiari au lazima ya jamii sharti athibitishe uume wake kupitia kwa uhusika wake katika matendo ya kishujaa na kutekeleza majukumu yake ya kiume katika jamii.

Taata wanyibaye noramehe
Kigire ngotebi noramehe
Nontoma kubiaro nindahike
Ndete nyagatoke na ikoroso
Totokere bori gategate
Chitagacha kwibwa chihete ho
Boke tohanene kuya moyo
Tui turakura ichikurate
Mona monto akwa.

Baba mzazi utatajirika
Kwani ujaponituma himaya za mbali nitafika,
Nilete talasimu tuifukie zizini katikati
Tuzuie ng'ombe wetu wasije wakaibwa
Asubuhi yake tufuate nyayo kwenda mbali
Huku tukipiga mayowe, kana kwamba tumefikwa na msiba

Ng'ombe ni mifugo ambayo huthamiwa sana katika jamii ya Abakuria. Mwanaume kama mlinzi huwa yuko radhi kutekeleza lolote katika kuhifadhi ng'ombe wake na kuwalinda dhidi ya wezi hasa kutoka jamii ya Wamasai na baadhi ya jamii za Wakalenjini. Katika kufanya hivyo mwanaume hutumia nguvu na ushujaa wake bila kuacha nyuma matumizi ya hirizi inapobidi. Matumizi ya hirizi hubainisha dhana ya mwanaume kujaribu kwa udi na uvumba katika kuhifadhi uwezo na mamlaka katika jamii. Hivi kwamba pale ambapo anashindwa hana budi kutumia njia zingine kwa mfano matumizi ya hirizi.

Pale ambapo jamii ilikuwa na uhitaji wa maarifa fulani, ni mwanaume aliyetumwa sehemu iliyofikiriwa kuwa na maarifa hayo. Ustahimilivu, ukakamavu na ushujaa zilikuwa sifa muhimu kwa mjumbe aliyestahili kutumwa sifa ambazo bila shaka zilikuwa za mwanamume. Aidha ilimbidi mjumbe kusafiri bila kujali hatari iliyo mbele yake na umbali wa sehemu alikotumwa. Kwani miongoni mwa jamii ya Abakuria inaaminika kwamba hakuna kisichowezekana kwa mwanaume. Imani hii hujengeka kutokana na jina la urejeleo wa mwanaume katika jamii ya Abakuria:

'omosacha'----------(mwanaume)

Jina 'omosacha'hutokana na neno 'sacha' lenye maana ya kujaribu. Kutokana na jina hili mwanaume wa Abakuria huzaliwa na kujamiishwa na imani ya kutokubali kushindwa katika hali iwayo yote. Sharti ajaribu kwa nguvu zake zote

Abairege baito tegeera
*montoma kurioba nenda*hike
niyi ntache umweri no-okogoro
na akarato kane karameni
ndete mahene gokebara
keno ke Bwirege

Wairege wetu nisikilize
Hata mkinituma angani nitafika
nikanyage mbalamwezi kwa mguu
huku kiatu changu kikimeremeta
nilete ukweli ulimwenguni
hasa hapa kwetu Bwirege

Katika jamii ya Abakuria, ni sharti mwanaume kuwa radhi kujiamini na kujitolea kutekeleza lolote kwa manufaa ya jamii. Mwanaume, kama mjumbe wa jamii, huwa tayari wakati wowote kutumwa na jamii kokote ilimradi anachokiendea ni cha manufaa kwa jamii, hufanya hivyo bila uoga wowote. Inaaminika katika jamii hii kuwa, baada ya kutahiriwa kijana wa kiume huwa ameingia katika kundi la wanaume, ambalo huipatia jamii kipau-mbele kabla ya kujifikiria binafsi. Aidha, mwanaume husawiriwa kama binadamu ambaye hujihami katika kukabiliana na hali yoyote katika kukuza na kuendeleza uwezo wake wa kiume katika kudumisha nafasi yake katika jamii, kutegemewa na kutosheleza jamii kwa mujibu wa mahitaji yao. Katika kufanya hivyo, mwanaume hujitokeza kuwa na uwezo mkubwa katika jamii, Hivyo basi usemi wake huwa na uzito kuliko wa mwanamke.

5.2.4 Taswira ya Mchikichi

Mwanaume husawiriwa kama mlinzi wa jamii, ambaye sharti ajihami kwa hali yoyote ile katika kulinda jamii kwa hatari yoyote. Ni wajibu wa kila mwanaume kuwa tayari na imara katika kukabiliana na uvamizi wowote kwa jamii ama wa binadamu (maadui) au wanyama hatari mfano simba, chui, nyati miongoni mwa wengine.

Abamura bawaito bang'anake
Bang'ana agakendo akangotera
Kamera Romara gate gate
Kararenda wandwe na wangubo
na ibi kurang'ati

Vijana wetu wa kiume ni mfano
wa Mchikichi/Mtende ambao umemea
mto Mara katikati
ukilinda simba, kiboko na mbweha.

Mwanaume amepewa sura ya mchikichi/mtende, mti ambao huwa na miiba yenye sumu na humea kandokando ya mto. Ufananisho huu ni dhihirisho kuwa kila mwanaume wa jamii sharti ajihami na silaha zake (sime, mkuki na ngao) ambazo zimefananishwa na miiba, katika kulinda jamii. Hali ya mtende kumea katikati ya mto Mara ndani ya maji ni hali ambayo imetiliwa chuku. Dhana ambayo inabainisha awe licha ya maadui wengi wa jamii au hali yoyote iwayo ngumu, mwanaume sharti kuwa imara katika kutetea na kulinda jamii. Taswira hii humweka mwanaume katikati ya jamii kama mchikichi ndani ya mto Mara, hali ambayo inamlazimu mwanaume kujihami na kuwa imara kushinda vishindo vya hali yoyote katika kutetea na kulinda jamii. Ufananisho huu ni ithibati mwafaka kwamba, mwanaume katika jamii ya Abakuria huwa na uwezo na mamlaka zaidi ya mwanamke. Uimara na ushujaa wake ni sifa ambazo humwezesha kudumisha uwezo na nafasi muhimu katika jamii.

5.2.5 Taswira ya Seng'enge

Seng'enge ni waya ambayo hutumika katika ujenzi wa ua, waya hii huwa na visumari vyenye ncha kali mfano wa miiba. Kwa kawaida, ua ambao umejengwa kwa seng'enge huaminika kuwa imara na ni hakikisho la ulinzi wa kutosha. Katika jamii ya Abakuria, mwanaume husawiriwa kama seng'enge. Ufananisho huu humpa mwanaume sura ya mlinzi wa jamii. Kwa sababu ya ugumu na visumari katika seng'enge, humaanisha nguvu na uwezo anazostahili kuwa nao mwanaume katika jamii ilihali visumari vyake ni kielelezo cha ushujaa,

ushupavu na hali ya kuwa tayari katika kukabiliana na hatari yoyote bila kutetereka katika kulinda wasiojiweza; kwa mfano watoto, wanawake na wakongwe.

Taata wanyiboye wang'ana
Orroseng'enge rro kerero
Mokare ataroke akoroheta
Agusima mbarera

Baba mzazi nakulinganisha na ua uliojengwa kwa
Seng'enge ya siku hizi
Usiowezwa kuvukwa na shujaa yeyote yule.

Mojawapo ya majukumu muhimu ya mwanamume miongoni mwa jamii ya Abakuria ni kuihami jamii. Historia simulizi inabainisha kwamba kumekuweko na uvamizi wa mara kwa mara kutoka kwa majirani wanaopakana na Abakuria. Wakati mwingine, uvamizi huu unaweza kutokea baina ya koo mbalimbali za Abakuria. Baadhi ya sababu ni upanuzi wa maeneo kwa ajili ya malisho ya mifugo, wizi wa mifugo, upanuzi wa mipaka ya aridhi kwa ajili ya kulima au uchokozi tu. Pindi uvamizi wa aina hii unapotokea, wanaume hutarajiwa kujihami kwa ushujaa katika kukabiliana na maadui hawa.

Mwanaume katika familia huwa na wajibu wa kijamii na wa kiitikadi kuhakikisha ulinzi wa kutosha katika mji wake na kwa jamii nzima. Kwa hivyo mzazi aliye na wavulana wengi huwa na hakikisho la ua imara na kuwa kizingiti cha kutosha kwa aina yoyote ile ya uvamizi. Kwa hivyo, baada ya kutahiriwa, mvulana huhitajika kuzidisha na kubainisha ushujaa na ukakamavu wake katika kulinda jamii.

5.2.6 Taswira ya Kipaza-sauti

Mwanaume katika jamii ya Abakuria hupewa sura ya kipaza sauti cha kutoa tahadhari dhidi ya hali yoyote ile ambayo inaweza kuzua shida au maangamizi katika jamii. Hivyo basi mwanaume husawiriwa kama binadamu mwerevu ambaye ana uwezo wa kutambua ishara yoyote ambayo inaweza kusababisha hasara, laana, uvamizi na maafa katika jamii. Uwezo huu humfanya mwanaume kushikilia nafasi muhimu katika jamii katika kutoa maamuzi ya kuaminika juu ya

maswala mbalimbali katika jamii. Hali ambayo bila shaka humfanya kujitokeza kama mwenye kumiliki mamlaka ya kiitikadi na ya kijamii kwa jinsia ya kike na jamii kwa jumla.

Abairege baito ndabatakia
Abaikwabe barwera komaguku
Baambaye ibibeti komareko
Bagora ichawaito ncharu
Totagaitwa na ubwiro.

Wairege wetu nawatahadharisha
Wamasai wametokezea milimani
Huku wametundika mikoba ya pesa begani
Wamenunua ng'ombe wetu wengi
Tusije tukaangamia kwa unyafuzi.

Unyafuzi ni ugonjwa unaotokana na ukosefu wa protini mwilini. Wamasai kununua ng'ombe wengi kutoka kwa Abakuria, ni ishara ya kutosha ya njama ya Wamasai ya kuzidisha idadi yao ya ng'ombe hali ambayo bila shaka ingewafanya Wakuria kuwa na ng'ombe wachache na kusababisha ukosefu wa maziwa na nyama ambayo ni sehemu kubwa ya vyakula vya aina ya protini. Ilikuwa ni wajibu wa mwanaume kutambua hali kama hii na kutoa tahadhari moja kwa moja, kuepusha jamii kujuta baadaye.

Shughuli ya uwindaji miongoni mwa jamii ya Abakuria ilitekelezwa na wanaume kwa kuzingatia ushupavu, ushujaa na ustahimilivu wao. Wakuria wamepakana na mbuga mbili za wanyama, Masai Mara kwa upande wa Kenya na Serengeti kwa upande wa Tanzania. Katika mbuga za wanyama kulikuwemo wanyama hatari mfano simba, chui, nyati, vifaru n.k. Vilevile, kulikuwepo askari walinzi ambao walikuwa na bunduki za kila aina. Hata hivyo wawindaji hawakuonyesha woga wowote.Nyiso ifuatayo ni kielelezo cha hatari walizokabiliana nazo wawindaji.

Abakare bawaito muyi ng'ora
Ichitinyi chaya aharrai
Abagemu mbabaita ni-ichikong'u
Mutige abasino kunyanyi

Mashujaa wetu mwende pole
Wanyama wa pori wameenda mbali
Walinzi watawaua kwa silaha kali
Muwaache wajane kwa shida

Katika hali kama hii, mwanaume hujitokeza kama kipenga cha kutahadharisha hasa kwa sababu ya werevu wa kugundua mambo kwa mujibu wa ishara fulani. Katika jamii ya Abakuria, mwanamke humtegemea mwanaume kiasi ambacho baada ya mwanaume kufa,mwanamke huzama kwenye lindi la shida. Mwanaume huwa na nafasi muhimu kama mtoshelezaji wa familia yake, uwepo kwake katika familia ni kinga ya kutosha kwa shida katika familia hasa zile ambazo ziko chini ya uwezo wake.

Mwanaume katika jamii ya Abakuria vilevile hufananishwa na baragumu. Kifaa hiki hutengenezwa kutokana na pembe ya kifaru au ya ng'ombe. Kwa kawaida baragumu hii ilipulizwa na mwanaume mwenye nguvu na ujuzi. Kusikika kwa sauti hii kulikuwa ishara ya kutokea swala la dharura. Aidha, ilitumika kutahadharisha jamii juu ya hatari fulani au kuhamazisha umma juu ya jambo fulani. Katika kipindi cha tohara, baragumu hii ilitumika kutambulisha pahala ambapo tohora itafanyiwa. Baragumu hii ilipulizwa na kutoa sauti za aina tofautitofauti ambazo zilieleweka kwa wanajamii. Kila sauti ikisimamia ujumbe fulani.

Taata wanyiboye wang'anake
Wang'ana irrirongwe rrya abasubi
rera rekogamba baikomana
amasubi amang'aini gacha hamwe

Baba nakulinganisha na baragumu maalum
ya wazee wa kimila/jadi
inayatumika kuwakusanya
wazee wenye hekima kuja pamoja.

Ufananisho wa baragumu na mwanaume ni dhihirisho la nafasi ya kipekee anayopewa mwanaume katika jamii kuhamasisha wanajamii na kutahadharisha jamii panapotokea jambo la dharura. Hali hii humpa mwanaume uwezo mkubwa wenye kumfanya kumiliki mamlaka

makubwa katika familia yake na jamii kwa jumla. Miongoni mwa jamii ya Abakuria, kuna kundi la wazee wanaojulikana kama "Abagaka ba ikimira" (wazee wa kimila/jadi). Wazee hawa huchukuliwa kuwa na hekima na busara na huaminika kuwa na 'nguvu za ajabu' ambazo huwawezesha kutenda vitendo vya ajabu kwa mfano, kusimamisha mvua, kuua, kutabiri n.k. Imani hizi huwafanya kutunukiwa heshima kubwa na wanajamii, kiasi ambacho uamuzi wao huwa kama sheria. Hukutana mara kwa mara katika kujadili mambo muhimu yanayoihusu jamii; kwa mfano, ni kundi hili ambalo huamua juu ya kuwepo au kutokuwepo kwa tohara katika kipindi fulani. Wazee hawa huwa na nafasi kubwa kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kipindi cha tohara, hasa kwa kuhakikisha kuwa kuna usalama na amani katika jamii na kwa watahiriwa na hasa zaidi huwa kinga halisi ambayo hubainisha nafasi pana na ya muhimu ambayo ni milki ya mwanaume miongoni mwa Abakuria. Hivyo basi, ni wazi kwamba mwanaume anachukuliwa kuwa na uwezo na nguvu za ajabu za kutatua masuala fulani katika jamii. Kuwepo kwake katika jamii ni hakikisho la kuwepo kwa mlinzi wa jamii. Hali hii hubainisha majukumu finyu ya mwanamke miongoni mwa jamii ya Abakuria kwani anaishi kumtegemea mwanamke siku zote.

5.2.7. Taswira ya Mtetezi

Katika kutetea nafasi yao katika jamii, mwanaume alipaswa kuwa tayari kwa hali yoyote, ili kubainisha ujasiri wake. Ushupavu wa wanaume katika jamii ni tisho na kinga dhidi ya maadui. Ili kutekeleza tendo la uvamizi wa kimabavu, iliwalazimu maadui kujipanga na kujitayarisha vilivyo bila kusahau kuwa mbele yao ni ukuta wa mashujaa ambao kwa hali yoyote wamejihami kuitetea jamii yao kwa nguvu na ushujaa.

Gikuburia waito giche ng'ora
giche keraburia ko-bamura
abangiri bawabo

Anayepanga uvamizi kwetu, aje polepole
Aulizie kwanza, huku akijua wapo
mashujaa, watetezi wa kwao.

Mwanaume husawiriwa kama mtetezi wa jamii anayeionea fahari na huwa radhi kwa uhai au kifo kuitetea. Hali hii humfanya mwanaume kujivunia kwao na kuwa tayari kwa hali yoyote katika kuhakikisha usalama na amani katika familia yake na jamii kwa jumla.

5.3 Taswira za Kimaumbile

Hizi ni taswira ambazo hubainishwa na vivumishi vya maumbile ya mwanaume. Taswira hizi hujengwa na kukuzwa kutokana na vivumishi angama vya mwili wa mwanaume ambavyo kwa misingi ya kibaolojia humtofautisha mwanaume na mwanamke kwa mfano sauti nzito, unene na nywele fupi. Sifa hizi hutiliwa nguvu na itikadi, utamaduni, imani na desturi, mielekeo na matarajio ya jamii kumhusu mwanaume. Hali hii huwa mchango wa kimsingi katika kumpa mwanaume sura mahususi.

5.3.1 Taswira ya Kalamu, Rungu na Upanga

Tohara ya vijana wa kiume huhusisha kukatwa kwa govi la dhakari, kitendo ambacho husawiriwa kama kuchongwa kwa kalamu au kunolewa kwa upanga. Baada ya kutahiriwa, wanawake huwaimbia watahiriwa nyimbo za sifa, hasa kusifu ushujaa, ushupavu na uvumilivu wa mtahiriwa. Nyimbo hizi husheheni taswira za kalamu, upanga na rungu mintarafu ya matarajio ya jamii kwa watahiriwa.

Rerro nchongewe ikaramu
Eno itagusira wino

leo nimechongewa kalamu
isiyoisha wino

Taswira ya "kalamu" huashiria tendo la kutolewa govi, ambalo ni ishara ya kuchongwa kwa kalamu aina ya penseli, kwani kabla ya kuchongwa haiwezi kutumika kwa minajili ya kuandika. Taswira ya kutoisha wino, ni ufananisho wa kuendelea kwa jamii kiuzazi. Baada ya kijana wa kiume kutahiriwa, alikuwa huru kuoa na kuanzisha familia yake kuhakikisha mwendelezo wa jamii ya Abakuria.

Rero ntiriribwe umuhio
Ogogwitaniria ababisa

leo nimenolewa upanga
wa kupigania na maadui

Taswira ya "upanga" hurejelea kukatwa kwa govi, tendo ambalo linafananishwa na kunolewa kwa upanga. Upanga uliashiria silaha, hivi kwamba baada ya tohara na kutoka jandoni, kijana wa kiume alijiunga na kundi la wanaume wa Abakuria, katika kulinda jamii. Hivyo basi, upanga uliashiria ulinzi wa jamii. Hivi ni kwa sababu miongoni mwa jamii ya Abakuria mwanaume ni mtetezi na mlinzi wa jamii. Hivyo ni sharti ajitolee kwa nguvu na ushupavu wake katika kuwatetea watoto, wanyonge, wakongwe na wanawake katika jamii. Wajibu huu huhalalishwa na methali ya Abakuria isemayo;

"Omosacha ni inguba"
"Mwanaume ni ngao"

Aidha, kitendo cha kutahiriwa kwa vijana wa kiume kilisawiriwa kama kuchongwa kwa "Rungu" ambayo ni aina ya silaha. Hivyo basi, urejeleo wa "rungu" na "upanga" ambazo ni silaha za vita, ni dhihirisho wazi kuwa wajibu wa wanaume ni kujihami na kubainisha ushujaa wao katika kuchunga na kulinda iktisadi ya jamii. Katika jamii ya Abakuria mifugo; mfano, ng'ombe, mbuzi na kondoo hupewa thamana kubwa, kiasi ambacho kila mwanaume alistahili kuwa mfugaji. Kuna imani katika jamii ya Abakuria kuwa, anayestahili kuwa na mifugo ni mwanaume mkakamavu, shupavu na mwenye kujitolea kukabiliana na hali yoyote ile hata iliyo hatari sana.

5.3.2 Taswira ya Nyati na Tufani

Naya ndaboronga mona eng'era
rrero nkuhusiande ki'omokama
gono go Muyuyi

nimekuwa nikiunguruma kama nyati
lakini kwa sasa ninavuma kama
tufani itokeayo Muyuyi

Ufananisho huu ni wa kuonyesha sifa mbalimbali za mwanaume, hasa vivumishi angama vya mwili wa mwanaume (sauti nzito, unene, nywele fupi). Mungurumo wa nyati na kuvuma kwa tufani hubainisha sauti nzito, aliyo nayo mwanaume. Kabla ya tohara, sauti ya kijana wa kiume inalinganishwa na mungurumo wa nyati lakini baada ya tohara sauti yake inafananishwa na kuvuma kwa tufani hali ambayo inabainisha kuwa kijana huyo amevuka kutoka hatua ya utotoni na kujiunga na kundi la wanaume. Matumizi ya sauti hizi ni kielelezo cha nafasi ya mwanaume katika jamii hasa kuhusiana na maamuzi kuhusu maswala nyeti ya jamii. Nyati ni mnyama mkubwa miongoni mwa wanyama wa porini, sifa ambayo inafananishwa na umbile la mwanaume, hasa unene. Aidha, nyati ni mnyama mwenye nguvu takribani zaidi ya wanyama wengi porini. Ufananisho huu hudhirisha umuhimu wa mwanaume kuwa na nguvu katika jamii akilinganishwa na mwanamke. Hivyo basi mwanaume husawiriwa kama binadamu mwenye uwezo na mamlaka katika jamii na unene wa maumbile yake ni uhalalisho wa nguvu jinsi ya kiume.

Kutokana na maelezo ya Kirutu (2006) Muyuyi ni eneo kati ya mpakani mwa Wakuria na Wamasai. Inaaminika kuwa upepo uliotokea eneo hilo ulikuwa mkali sana mfano wa tufani, wenye uwezo wa kuangusha na kupeperusha vitu vizito kwa mfano paa la nyumba na miti mikubwa. Uwezo huu wa tufani ni sifa ambayo mwanaume hustahili kuwa nayo katika jamii ili kutekeleza majukumu yake na kuhifadhi nafasi yake katika jamii.

Jinsia ya kiume miongoni mwa jamii ya Abakuria husawiriwa kama jinsia yenye uwezo wa ajabu. Hivi kwamba mwanaume anaweza kutekeleza kile ambacho kwa muda mrefu kimeaminika kushindikana. Kila kijana wa kiume hujamiishwa tokea utotoni na imani ya kutokubali kushindwa au kuogopa kutekeleza wajibu wake kwa kuzingatia kushindwa kwa waliomtangulia.

5.3.3 Taswira ya Chaka la Retinde

Mwanaume husawiriwa kama chaka lenye mapandikizi ya miti ya aina mbalimbali ambamo kuna wanyama hatari mfano simba, chui, ndovu, vifaru, nyoka miongoni mwa hatari

zingine ndani ya chaka la aina hii. Sehemu ya aina hii huwa ya kuogopwa na kuogofya. Anayeingia kwa chaka la aina hii huingia kwa tahadhari kubwa. Mwanamume mzazi hupewa sura ya chaka ilihali vijana wake wa kiume ni ufananisho wa hatari iliyomo kwenye chaka hilo.

Taata wanyiboye wang'anake
Wang'ana Retinde nyamegogo
Rekorara ichindwe na inchinsabi
na ichinguruneti

Baba mzazi nakulingaisha na chaka
la Retinde, lenye mapandikizi ya miti,
wanamoishi simba na majoka hatari
pamoja na wanyama wengine wakubwa
wa kuogofya

Chaka la Retinde lipo ufukoni au ukingo mwa mto Mara, ndani yake kuna wanyama wakali, majoka wenye sumu na hatari zingine zinazoandamana na chaka la aina hiyo. Ukubwa wa chaka hili na ukubwa wa miti ndani yake ni dhihirisho la sifa mojawapo inayompa mwanaume nguvu za kimaumbile. Taswira ya chaka hili ni ufananisho wa mzee ambaye katika familia yake mna vijana wa kiume waliojihami, mashujaa wa kuogopwa. Hii inamaanisha ukitekeleza uvamizi wa aina yoyote katika mji wa aina hii, sharti akiwa adui uwe umejiandaa vilivyo. Ilikuwa ni nadra mji wa aina hii kuvamiwa. Kwa ajili hii, mwenye mji (mzee) alitunukiwa sifa na heshima kubwa; kila mara alipigiwa mifano kwa mashujaa chipukizi. Taswira hii hudhihirisha thamani ya ushujaa miongoni mwa Abakuria, hali ambayo humchora mwanaume kama mlinzi wa jamii dhidi ya hatari ya aina yoyote ile. Mwanaume kama kichwa cha familia alikuwa na wajibu wa kijamii kuhakikisha kuwa watoto wake wa kiume wamejamiishwa kwa misingi ya kutokuwa na sifa ya uoga na kudhihirisha siku zote ujasiri.

5.3.4 Taswira ya Kifaru

Mwanaume miongoni mwa Abakuria hufananishwa na kifaru. Ufananisho huu hujengwa mintarafu ya sifa za huyu mnyama za ukali, hasira na uwezo wake. Mwanaume katika jamii ya Abakuria anarakiwa kuwa na sifa hizi. Sifa hizi huifanya jinsia ya kiume kuwa na mamlaka zaidi katika jamii kuliko wanawake. Aidha, ni za kimsingi katika ujenzi na ukuzaji wa nguvu-jinsi kiume katika mchakato mzima wa ujamiishaji wa mwanaume. Matokeo yake ni uhalalisho wa nafasi pana anayopewa mwanaume katika jamii. Hali hii humpa mwanaume sura ya mwenye madaraka ya kumwezesha kutawala na kumiliki nyenzo zote za uzalishaji mali.

Abakare bawaito mong'anake
Mong'ana akabwaro kagesaka
Kara kagusika amaroboko
gara gibing'eng'i

mashujaa wetu ni mithili ya kifaru
azibaye vivuko vya mto
vya kuelekea kwenye majabali ya chumvi

Majabali ya chumvi hupewa thamani kubwa miongoni mwa Abakuria kama lishe kwa mifugo. Kivumishi cha ukali wa kifaru ni tisho kwa adui wengine, sifa ambayo mwanaume anatakiwa kuwa nayo katika kuhifadhi nafasi yake ya kijamii na kiitikadi kama mwanaume wa kutegemewa na jamii. Jabali la chumvi ni taswira ambayo hubainisha raslimali za thamani kwa jamii. Miongoni mwa jamii ya Abakuria ng'ombe ni mifugo ambao huthaminiwa sana; hivyo basi, kuna uhitaji wa ulinzi thabiti. Kwa sababu hii, mwanamume kama kifaru sharti awe tayari kuziba vivuko au nafasi yoyote ile ambayo adui anaweza kuitumia katika kuwanyang'anya wanajamii raslimali hii muhimu. Wajibu huu humpa mwanamume hadhi muhimu ya kumwezesha kuwa mtawala na mwenye uwezo katika maamuzi muhimu kuhusu maswala mbalimbali ya jamii. Hali hii humsawiri mwanaume kama jinsia ya kutegemewa.

5.3.5 Taswira ya Radi

Kulingana na uwezo na nguvu anazostahili kuwa nazo mwanaume kwa mujibu wa mila, desturi, na itikadi za jamii ya Abakuria, mwanaume husawiriwa kama radi, sura ambayo huafiki uwezo wa ajabu alionao mwanaume katika jamii ya Abakuria. Nguvu zake ni mithili ya nguvu za radi. Hali hii huhalalisha hadhi na thamani anayopewa mwanaume mintarafu ya uwezo na nguvu zake katika kutekeleza majukumu muhimu ambayo ni mengi na mazito kuliko ya mwanamke.

Abamura bawaito monga nkoba
Mete mogosara na binyege
na nkomo cha biara

wanaume wa kwetu ni mithili ya radi
hupasua miti vipande vipande kwa kutumia
mikono na makucha ya vidole

Kwa kawaida pigo la radi linaweza kupasua pandikizi la mti vipande vidogovidogo. Ufananisho wa mwanaume na radi huakisi nguvu anazotakiwa kuwa nazo katika jamii kumwezesha kukabiliana na hali zote. Katika jamii ya Abakuria, mwanaume mwenye nguvu na shujaa ni raslimali ya jamii. Katika mchakato wa ujamiishaji, watoto wa kiume hujamiishwa kuwa wakali, wenye mori, na wenye uwezo wa kutawala. Sura hii humfanya mwanaume wa Abakuria kuwa na amri juu ya familia yake na kwa jamii nzima. Kwa jinsi hii, anakuwa na mamlaka ya kisiasa na maamuzi kuhusu mambo muhimu yanayoihusu jamii. Hivyo basi, mwanamume hutwaa mamlaka na nafasi nzuri katika jamii ikilinganishwa na ya mwanamke hususan katika maswala ya kiuchumi, kijamii na ya kijinsia. Kwa mfano, kutokana na uwezo na nguvu zake, anajihuzisha na kazi au biashara yenye mapato ya juu na huchukuliwa kama nguzo nyumbani mintarafu ya nafasi na majukumu yake muhimu katika familia.

5.4. Taswira za Kiuchumi

Hizi ni taswira ambazo huhalalisha nafasi ya mwanaume ya kuwa na uwezo wa kiuchumi ambao humwezesha kutosheleza na kuikimu familia yake. Kutokana na nguvu zake za kiuchumi,

huwa na nafasi kubwa kuliko ya mwanamke katika kumiliki na kutawala takribani nyenzo zote za uchumi katika kiwango cha familia na cha kijamii. Hali hii hujengwa na kukuzwa na utamaduni wa jamii mintarafu ya matarajio, itikadi, na mielekeo mahsusi ya jamii. Aidha, taswira hizi hubainisha mwanaume kama mwenye uwezo wa kuauni familia yake kwa chakula na malazi.

5.4.1 Taswira ya Mto Mara

Mwanamume husawiriwa kama mkimu-familia; mahitaji takribani yote ya familia humtegemea. Kwa hivyo ni wajibu wa kijamii na wa kiitikadi mwanaume kujitahidi kwa hali na mali katika kukimu familia yake, swala ambalo humfanya kuwa mwenye mamlaka na wajibu kama mkuu wa kaya. Mwanaume yeyote wa Abakuria anapoulizwa kuhusu hadhi yake katika jamii, takribani wanaume wote tuliowahoji walisema kwamba wamezaliwa na kujamiishwa kama wenye madaraka na hadhi ya juu katika familia na jamii kwa jumla. Ni muhimu kutaja kuwa wanawake hulinganishwa na watoto ambao ni sharti waelekezwe na wanaume. Kwa mustakabali huu mwanaume ni simba (endwe) ilihali mwanamke ni kondoo (iring'ondi) mintarafu ya sifa za wanyama hawa.

Sokoro waito no omonene
Wang'ana Romara niyo enene
Niyo itakahoye ekogatoka
Chikunywa agasense

Babu wetu ni mkuu
Ni mithili ya mto Mara, ndio mkubwa
Haujawahi kukauka
Hadi mifugo wanywe mchanga.

Mto Mara upo katika mkoa wa mara nchini Tanzania, unapitia katika ardhi ya Abakuria wa Tanzania. Katika historia ya Abakuria, Mto huu haujawahi kukauka hata wakati wa kiangazi . Maji ni uhai kwa binadamu, wanyama na mimea. Katika nyiso hii, mwanamume (babu) anafananishwa na mto Mara ambao tangu jadi hadi leo haujawahi kukauka hata siku moja.

Aidha, maji ni mahitaji la kimsingi kwa mifugo kama yalivyo kwa binadamu. Ufananisho huu hubainisha nafasi ya mwanaume katika kutosheleza jamii yake kwa mahitaji yote. Mwanamume ana wajibu katika familia kuhakikisha kuwa familia yake inapata mahitaji ya kimsingi; mfano chakula, mavazi na makao. Familia ambayo hukumbwa na njaa lawana humwendea mwanaume. Tukio hili lilimfanya mwanaume wa aina hii kuchukuliwa kama bwege, asiye na faida katika jamii.

5.4.2 Taswira ya Mwavuli (Irigamero/umwigamero)

Mwavuli ni kifaa cha kisasa ambacho humkinga binadamu kutokana na mvua au jua kali. Matumizi ya Mwavuli katika nyiso hii ni ithibati ya athari ya usasa takribani katika asasi zote za jamii. Katika jamii ya Abakuria mwanaume ni kinga dhidi ya shida, na matukio yoyote ya hatari. Panapotokea hatari yoyote aidha ya mnyama hatari au wezi wa kimabavu, mwanaume hutakikana kutekeleza wajibu wa kukinga jamii dhidi ya hatari hiyo. Aidha panapotokea shida katika jamii mfano njaa, ni sharti mwanamume ajikakamua kutafuta suluhisho.Taswira hii hubainisha wazi hali ya mwanaume kuwa wa kutegemewa katika jamii kwa hali yoyote. Wajibu ambao humjenga kuwa kiongozi na mwenye mamlaka katika familia na jamii.

Abamura bawaito nigamero
Nebo twigameye imbura indito
Eno yo omohioka

Vijana wetu wa kiume ni mwavuli
kwao tumejikinga mvua nzito
hii ya masika

Mvua ya masika (yo-omohioka) hunyesha kwa wingi kwa muda mrefu. Tukio hili huleta hasara kubwa; kwa mfano, mmomonyoko wa udongo, uharibifu wa mimea na mazao, huangamiza wanyama na hata binadamu. Mvua ya masika imetumiwa kijazanda kumaanisha hatari yoyote ambayo huenda ikajiri katika jamii bila kutarajiwa. Hivyo basi ni jukumu la wanaume kuwa kinga dhidi ya chochote kile ambacho kinaweza kuleta maafa au hali ngumu katika jamii. Hivyo, taswira hii ya mwavuli humchora mwanaume kama kimbilio na hifadhi

wakati wa hatari na taabu. Mwanaume sharti ahakikishe ameisitiri familia na jamii yake kwa hali na mali; na kwa kufanya hivi, mwanaume anajidhihirisha kama mwenye uwezo na mamlaka katika jamii. Bila yeye, jamii hukosa mhimili na mlinzi. Hali hii hufanya mtoto wa kiume kuthaminiwa na kupewa hadhi kubwa kuliko mtoto wa kike. Hii ni kwa sababu Wakuria huamini kuwa asiye na mtoto wa kiume hana mji.

5.4.3. Taswira ya Mwangaza (oborabu)

Palipo na giza huwa ni muhali kuona wala kutambua chochote hali hii huzua uhitaji wa mwangaza. Katika jamii ya Abakuria, mwanaume husawiriwa kama nuru ya jamii. Ufananisho huu unamfanya mwanamume kusawiriwa kama mwenye akili na hekima kuliko mwanamke. Kama nuru ya jamii, mwanaume hutakikana kuwa kiongozi mwema katika jamii anayeiongoza si kuielekeza kwa maafa bali kwa ufanisi.

Taata wanyiboye nekemenio, moreka tomahe
tui guchisora Rongararo, hara chikorara icha ababisa
chabo kiburuha na nyamahara, chaibora ametena amatebega
chitore Bwirege kobamura
chiche kobakikia abake bano.

Baba mzazi wewe ni kimulimuli cha radhi
mulika tuvuke, twende kuwafuata ng'ombe Rongararo
pale walalapo ng'ombe wa maadui
hudhurungi na wenye mabaku
wanaozaa mahuluti na wanene
waje Bwirege kwa mashujaa
ili wawakuze watoto wetu wachanga.

Kitendo cha kuwanyang'anya maadui ng'ombe kimabavu kilipewa sifa badala ya kushtumiwa. Miongoni mwa maadui wa jadi wa Wakuria ni Wamasai na wa jamii za Wakalenjini. Jamii hizi zote ziliamini kuwa wao ndio wenye haki ya kuwa na ng'ombe. Imani hii ilitokana na thamani ya kuwa na ng'ombe wengi. Vitendo hivi vya unyang'anyi vilitekelezwa na

wanaume mashujaa. Wanaume wenye umri mkubwa walisawiriwa kama mwangaza wa ajabu hali ambayo inabainisha baraka kwa mashujaa waliodhamiria kushambulia na kuvamia maadui kwa minajili ya kuiba ng'ombe wa maadui kimabavu. Ng'ombe waliobiwa walikuwa wa manufaa kwa jamii hasa zaidi kwa maziwa ambayo ni chakula muhimu kwa watoto wachanga. Mwanaume hujitokeza kama nuru ya ajabu ambayo hufananishwa na akili aliyo nayo ya kupanga, kuongoza, na kutekeleza maswala ambayo kwa wengi ni ya hatari Kinyume chake, mwanaume hujitokeza kama mwenye uwezo wa ajabu, na uwezo huu humwezesha kuwa na nguvu na kiongozi mwenye madaraka muhimu katika jamii. Hivi kwamba, bila yeye jamii hukosa mwelekeo na kuwa mfano wa kipofu asiyejua aelekeako wala atokeako.

5.4.4 Taswira ya Uyoga

Katika jamii ya Abakuria mwanaume hupewa sura ya uyoga, katika kumsawiri kama nguzo ya familia. Uyoga huweza kumea kokote ardhini hata jangwani. Kwa kawaida, uyoga huwa na mhimili mmoja. Mzizi na mhimili ni ishara ya mwanaume katika familia ilihali kichwa cha uyoga ni ufananisho wa familia ambayo hujumulisha mke na watoto. Hivyo, licha ya uzito wa kichwa, mhimili huwa imara pasipo kupinda hali ambayo huashiria uthabiti wa mwanaume katika familia yake. Sehemu ya mzizi na mhimili katika uyoga huwa ya muhimu sana, hivi kwamba ni kutokana na sehemu hizi ambapo kichwa hupata mahitaji ya kimsingi hali ambayo hufanya uyoga kukua, na hasa zaidi kichwa kupanuka. Hali hii hubainisha nguvu na uwezo wa mwanaume katika kuauni familia yake kwa mahitaji ya kimsingi na mengineyo. Uimara wa mhimili wa uyoga ni ufananisho wa hali halisi ambayo ni sharti mwanaume adhihirishe. Licha ya familia kubwa na shida andamizi, lazima mwanaume ajikakamue katika kukimu familia yake na aonyeshe uthabiti katika kuilinda, kuitunza na kuitosheleza mintarafu ya mahitaji muhimu. Kupinda kwa muhimili/nguzo ya uyoga ni ishara ya mwanaume kushindwa kutekeleza wajibu wake wa kijamii na wa kiitikadi wa kuikimu familia yake.

Gono go omogaka ngwitachere
Mona irrinyansaka rre kiribo
Nyamuri motambe

Mji huu wa mzee ni mithili ya
Uyoga wa jangwani
Wenye mzizi mrefu.

"Irrinyansaka" ni aina ya uyoga ambao humea kwenye vichuguu na hasa zaidi sehemu kavu. Jangwa limetumiwa kijazanda, kuonyesha shida na misukosuko ya kilimwengu ambayo ni ndaro kwa mwanamume katika kukimu familia. Urefu wa mzizi ni ufananisho wa uthabiti anaostahili kuujenga mwanaume ili kuukuza utambulisho wake wa kijinsia. Taswira hii hubainisha umuhimu wa kuwepo kwa mwanaume katika familia na jamii kwa ujumla. Familia isiyo na mwanaume huwa imekosa kiungo muhimu sana.

5.5 Taswira za Kitamaduni na Kijamii.

Hizi ni taswira ambazo ni zao la miundo msingi ya utamaduni wa jamii husika. Zinatokana na imani za wanajamii ambazo ni msingi wa kuhalalisha baadhi ya matendo ya mwanamume yanayomfanya kustahili hadhi ya juu; Kwa mfano, kuwa na wake wengi wa halali na wa nje ya ndoa. Miundo msingi ya utamaduni wa jamii huchangia falsafa ya jamii hiyo na utawala takribani sehemu zote za maisha ya wanajamii.

Katika kuangaza matumizi ya lugha katika nyiso za jando ni bayana kuwa kuna matumizi mengi ya taswira zinazomrejelea mwanaume. Taswira hizi hutoa picha, zinazoafiki mielekeo, itikadi na matarajio ya jamii kumhusu mwanaume Katika kufanya hivyo, taswira mwafaka ya mwanaume wa Abakuria hujitokeza. Taswira hizi hudhihirisha kwa kiasi cha haja dhana ya ujenzi wa uume miongoni mwa jamii ya Abakuria.

5.5.1 Taswira ya Kiongozi "Rosogiro"

Rosogiro ni mojawabo wa viongozi aliyewahi kutawala jamii ya Wamasai. Inasimuliwa kuwa alikuwa na idadi kubwa ya ng'ombe. Mwanaume wa Abakuria humithilishwa na kiongozi huyu.Katika jamii ya Abakuria mifugo walikuwa ishara ya utajiri na uwezo, walichukua asilimia kubwa ya mahari. Aidha, kwa sababu ya idadi hii, alipata kishawishi tosha cha kuoa wanawake wengi na matokeo yake ni kuwa na idadi kubwa ya watoto. Mji wake ulipanuka, na ilimlazimu

kuwa na nyumba nyingi, na hii ilikuwa ni sifa kubwa kwa mwanaume wa Abakuria. Alitolewa mifano palipohitajika. Hali hii haikuepukika katika utanzu huu wa fasihi simulizi ya Abakuria.

Taata wanyiboye wang'ana ng'we
Monto koreng'aine Ndosogiro
Omonto omotatiro umukumahe
Nyabihita binane

Baba mzazi nakulinganisha na Rosogiro
Mbabe wa mlango wa motatiro (mlango wa jamii ya wamasai)
Mwenye maboma manane.

Katika jamii ya Abakuria, kila boma huwakilisha mwanamke. Mwanaume hulazimika kuwa na idadi ya miji sawa na idadi ya wanawake aliye nao. Ni muhimu kutaja kuwa utajiri ni milki ya mwanaume miongoni mwa jamii ya Abakuria, na mwanamke huwa ni sehemu mojawapo ya utajiri wa mwanaume. Aidha, jamii ya Abakuria huamini kuwa ukwasi wa jamii hutokana na juhudi za wanaume.

Kupitia kwa nikaha mwanaume huwa na mamlaka juu ya uzazi na unyumba wa mwanamke. Uume huhusishwa na mwanaume kujidhibiti nafsi na hadhi yake. Matumizi ya mahari ni ishara ya 'ununuzi wa wanawake', kigezo ambacho humfanya mwanaume kuwa na madaraka zaidi kuliko mwanamke katika ndoa.

Inaaminika kwa kiasi kikubwa miongoni mwa Abakuria kuwa mwanaume mwenye kutunukiwa taadhima ni yule aliye na uwezo wa kuoa na kuhudumia wanawake wengi. Kuwa na wake wengi kunaandamana na umaarufu wa mwanamume katika jamii. Vilevile, ukwasi huangazwa kwa misingi ya idadi ya watoto. Mume aliye na watoto wengi wa kiume huaminika kuwa na ulinzi mkali na kutokana na juhudi na uwezo wao, bila shaka huwepo mali nyingi. Ilihali wingi wa watoto wakike huashiria wingi wa ng'ombe; hasa kutokana na malipo ya mahari.

Taata wanyiboye wang'ana ng'we,
Wang'ana Omotatiro omorraiboni
Omome wa iching'ombe na ichimburi
Hamwe na amang'ondi

Baba mzazi nakulinganisha na Motatiro
Kiongozi wa jamii ya Wamasai (Laiboni)
Tajiri wa ng'ombe, mbuzi na kondoo.

Wakuria wanapakana na jamii ya Wamasai, wanaamini kuwa ili kuwa kiongozi katika jamii ya ni sharti uwe umefikia kiwango fulani cha utajiri hasa wa mifugo kama ng'ombe. Uhusisho huu una ukuruba mkubwa na misingi ya kupima ukwasi wa mtu katika jamii ya Abakuria. Aidha, mwanaume hutarajiwa kutumia maarifa na juhudi katika utafutaji wa mali. Hivyo basi, baada ya tohara, kila kijana wa kiume huchukuliwa kuwa amefikia umri wa kujitegemea kimaisha. Bidii na nguvu zake ndiyo msingi wa kumwezesha kuishi bila kutegemea wazazi na jamii. Hii ni kwa sababu anachukuliwa kuwa ameingia kwenye kundi la wazalishaji mali katika jamii. Baada ya hatua hii ana uhuru wa kuoa na kukimu familia yake.

Mwanaume miongoni mwa jamii ya Abakuria husawiriwa kama mzalishaji mali huku utambulisho wa jinsia ya kike ukijitokeza katika ulaji na matumizi ya mali hiyo. Swala ambalo huwafanya wanaume kumiliki nafasi pana katika maamuzi yanaoyohusu maswala nyeti ya maendeleo katika jamii. Taswira hii ni zao la itikadi na mielekeo ya jamii chini ya utamaduni wa jamii ambayo hukuza na kuhalalisha sura hii.

5.5.2. Taswira ya "Umurisia"

Matarajio ya jamii kwa watahiriwa hubainishwa bayana kupitia kwa nyiso za jando. Ni utanzu muhimu ambao huonyesha wazi kuwa watahiriwa wamepiga hatua kutoka utotoni tayari kujiunga na kundi la watu wazima. Kwa wanaume, nyiso hudhihirisha umuhimu wa hatua hii. Mtahiriwa hujisifu kwa ushujaa na kujitolea kwake kuhimili uchungu wa kisu. maneno yake kupitia kwa nyiso hubainisha furaha yake ya kutoka utotoni "uburisia" na kuingia kwenye kundi la watu wazima.

Wanyora borina bogachoka
Bohika korototi
Rero mbotegeye abana abake
Bara bagukina kuya igoro

Aibu ya kuwa murisia (ambaye hajatahiriwa)
Ilikuwa imefika utosini, lakini tangu sasa
Nimewaachia watoto wadogo wanaokua

Kwa kawaida vijana wa kiume miongoni mwa jamii ya Abakuria hupashwa tohara wakiwa na umri wa kati ya miaka kumi na minne na kumi na minane (14-18). Katika umri huu mvulana huwa amegundua tofauti ya mtahiriwa na yule ambaye hajatahiriwa mintarafu ya majukumu, itikadi, mielekeo na matarajio ya jamii. Kabla ya kutahiriwa, mvulana hutekeleza majukumu ambayo kwa jamii ya Abakuria huchukuliwa kuwa ya kike. Kwa mfano, kupika, kuosha vyombo, kuteka maji, kukusanya kuni na kuosha watoto wadogo miongoni mwa majukumu mengine. Kwa wavulana ambao wamefikia umri wa kutahiriwa, wanaona kama majukumu haya yanawaaibisha. Kwani, ni kama kulinganishwa na wenzao wasichana au kunasibishwa na wanawake. Ni muhimu kutaja kuwa katika jamii ya Abakuria, ni muhali vijana wa kiume kuwachukulia wenzao wa kike kuwa katika rika moja hata kama wanalingana kiumri. Kwa kukataa sifa na majukumu ya kike, vijana wa kiume wanathibitisha juhudi za kila mwanaume kuendeleza utambulisho wa jinsia yake.

5.5.3 Taswira ya Daraja

Mwanaume pia anasawiriwa kama daraja la kufikia ufanisi katika jamii. Anatarajiwa kujizatiti vilivyo kwa nguvu na maarifa yake ili awe daraja imara la kuwezesha familia yake na jamii nzima katika kufikia upeo wa ufanisi.

Abamura bawaito na abakare
Bang'ana umwitaliano umukumahe
Newe agichenga iya kirumi
Amagari gagacha gakamboka
Gakagera Mwanza na Totoma

Hara haikareywe imigutano
Geno ge ikimira igikumahe
Kera bakorengi kurwa karre
Kurwa nyamburiti komakora

Vijana wetu wa kiume ni mashujaa
Ni mithili ya mzungu mwitaliano
Aliyejenga daraja la kirumi
Magari yakaja yakavuka
Kuelekea Mwanza na Dodoma
Panapofanyiwa mikutano maarufu
Ya wazee wenye hekima
Tangu zamani za kale, enzi ya kizazi
Cha Wanyamburiti.

Daraja la kirumi lipo katika mto Mara, mkoa wa Mara nchini Tanzania. Ni kiunganishi cha Tarime na Musoma na miji mingine kama Mwanza, Dodoma, Moshi, Shinyanga . Daraja hili lilijengwa kwa muda mrefu huku mara mwa mara likibomoka. Watu wengi waliangamia na mali nyingi kupotea. Kutokana na hali hii, daraja hili lilihusishwa na mashetani swala ambalo liliwaogopesha mainjinia wengi. Lakini kwa ushujaa, umaarufu, kujitolea na kujiamini kwa mainjinia waitaliano, daraja hili lilijengwa Hadi leo ni kisa cha kusisimua miongoni mwa Abakuria wa Kenya na Tanzania. Kwa hivyo kimehifadhiwa katika nyiso za jando. Kwa sababu ya Ukwasi wa maarifa, uvumilivu na ushupavu wa mainjinia hao, wanaume hupewa taswira hiyo, na kila mara kuhimizwa kutokufa moyo kabla ya kufaulisha tendo fulani. Daraja hili lina manufaa makubwa katika mkoa wa Mara na Afrika Mashariki mintarafu ya usafiri, ukuzaji wa uchumi na maendeleo. Kwa jumla, mwanaume kama mkimu familia na mwenye wajibu mkubwa katika uhakikisho wa maendeleo na ufanisi wa jamii, hupewa taswira hii ya Daraja ya Kirumi. Historia simulizi ya daraja hii hubanisha uhalalisho wa utamaduni juu ya sura ya mwanaume miongoni mwa jamii ya Abakuria.

5.6 Hitimisho

Mtazamo wa jinsia ya kiume hubainika kuwa na thamani ya juu; hivyo basi, itikadi za kiume na muundo wa kijamii humpa mwanamume uwezo na mamlaka ya juu zaidi ya mwanamke. Lugha kama kiambajengo muhimu cha utamaduni wa jamii huhusika, hudhihirisha tofauti za mahusiano ya kiuwezo baina ya mwanamume na mwanamke na huendeleza utofauti wa muundo wa itikadi muhimu za jamii.

Katika sura hii tumechanganua nyiso ishirini na nne ambazo zinamrejelea mwanamume. Kusudi kubwa lilikuwa kutathmini mchango wa nyiso za jando katika kujenga uwezo-uume na kubainisha taswira ya mwanamume wa Abakuria inavyojitokeza katika utanzu huu wa fasihi simulizi ya Abakuria. Ni muhimu kutaja kuwa idadi ya nyiso tuliyoishughulikia ni sehemu ndogo ya hazina kubwa ya nyiso za jando za Abakuria.

Kwa kuzingatia nyiso tulizozihakiki na kuzichanganua, inadhihirika bayana kuwa zina uhusiano mkubwa na mielekeo, mitazamo, matarajio, itikadi na utamaduni wa Abakuria. Nyiso hizi zote zimechota msamiati kutoka kwa mazingira ya jamii ya Abakuria. Falsafa, dhamira na maudhui yake yametokana na jumla ya matarajio na mitazamo ya utamaduni wa jamii ya Abakuria. Maana na madhumuni ya nyiso za jando hueleweka wazi ndani ya muktadha wa jamii hii.

Mitazamo na mielekeo ya mwanamume hutawala takribani katika asasi zote za jamii. Taswira mbalimbali ambazo tumezirejelea hubainisha mwanamume kama jinsia muhimu na yenye hadhi ya juu katika jamii ya Abakuria. Kwa mfano, kuwepo kwake ni hakikisho la ulinzi na usalama thabiti katika jamii. Mwanamume husawiriwa kama mkimu familia ambaye sharti ajitolee kwa udi na uvumba katika kuitosheleza familia yake kwa mahitaji ya kimsingi, kwa mfano, chakula , malazi na mavazi.

Mwanamume vilevile, amesawiriwa kama binadamu mwenye mamlaka zaidi kuliko mwanamke na ana wajibu wa kiitikadi katika kuhakikisha maisha ya jamii kiuzazi. Ana haki ya kitamaduni kuoa wanawake wawili au zaidi, hali ambayo huhalalishwa na mitazamo na matarajio ya jamii. Vilevile, katika mchakato mzima wa ujamiishaji, wanaume hujamiishwa hivi kwamba utumishi wa wanawake kwao ni halali kwa mujibu wa mielekeo, mitazamo, mila na desturi za jamii. Mwanamume hujamiisha na kuishi na imani kwamba mwanamke ni sehemu mojawapo ya milki yake. Hivyo basi, kwa mujibu wa utamaduni, itikadi na miundo ya mamlaka katika jamii, nyiso za jando huwa na mchango mkubwa katika kujenga na kukuza uwezo-uume

na kuhalalisha nafasi pana ya mwanamume katika jamii kama, kiongozi, mtawala, mlinzi na mwenye uwezo mkubwa zaidi ya mwanamke.

Kuna uwezekano kuwa baadhi ya falsafa katika nyiso hizi zimepitwa na wakati mintarafu ya maendeleo ya ulimwengu; hususan maendelea ya kielemu, kiuchumi na ya kidini. Hata hivyo nyiso za jando miongoni mwa Abakuria ni mchango madhubuti wa kubainisha mielekeo na matarajio ya jamii kumhusu mwanamume. Swala ambalo limetanda katika nyiso zote tulizozichanganua ni thamani na uwezo wa mwanaume; kuwepo kwake katika asasi mbalimbali kunathaminiwa zaidi ya kuwepo kwa mwanamke. Mtazamo huu hujengwa kutokana na umuhimu anaotunukiwa, majukumu na uhusika wake katika jamii ya Abakuria.

SURA YA SITA

MUHTASARI, MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

6.1 Utangulizi

Sura hii itashughulikia muhtasari, matokeo ya utafiti, aidha, na mapendekezo. Kimsingi utafiti huu umebainisha kwamba mwanaume wa Abakuria husawiriwa kwa njia chanya. Vilevile imejitokeza bayana kuwa, utamaduni, mielekeo, mitazamo na matarajio ya jamii ni mchango mwafaka katika ujenzi wa uwezo-uume. Matokeo yanayowasilishwa yametokana na madhumuni ya utafiti ilihali hitimisho limeibuka kutokana na matokeo ya utafiti.

6.2 Muhtasari

Tasnifu hii imeshughulikia nyiso ishirini na nne; ingawa kuna baadhi ya nyinginezo ambazo zinajikokeza hapa na pale ili kutilia nguvu zile tulizozichanganua. Azma kubwa ya utafiti huu ilikuwa kuibainisha sura ya mwanamume inavyojitokeza katika nyiso za jando miongoni mwa Abakuria na mchango wake katika kujenga na kukuza uwezo-uume. Ili kufanikisha madhumuni ya utafiti huu, uchanganuzi wa nyiso umefanywa chini ya mwongozo wa misingi ya nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi na ile ya Uwezo-Uume. Misingi ya nadhana hizi vilevile, imetumiwa katika kuitolea kauli taswira anayopewa mwanaume wa Abakuria. Ili kupambanua azma hii, uchanganuzi huu umezingatia itikadi za uwezo uume, tamathali za usemi hasa taswira na jazanda, thamani ya mantiki na yaliyomo katika nyiso za jando, majukumu ya kijinsia na mikakati ya kumsawiri mwanamume.

Tasnifu hii imegawika katika sura sita, sura ya kwanza inahusu utangulizi wa utafiti; sura hii imeeleza kwa kina usuli wa mada ya utafiti, mada ya utafiti madhumuni ya utafiti, nadharia tete za utafiti, Umuhimu wa utafiti na upeo wa utafiti. Sura ya pili inachanganua yaliyoandikwa kuhusu Abakuria; historia yao, fasihi yao na utamaduni wao juu ya uwezo-uume, pia pamebainishwa yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti. Sura hii imeweza kuonyesha baadhi ya tafiti za awali zinazokaribiana na utafiti wetu na jinsi tafiti hizo zinatofautiana na utafiti huu. Aidha pameelezwa mwanya ambao matokeo ya utafiti huu yanadhamiria kuziba. Katika sura hii, vilevile, pamepambanuliwa nadharia mbili zilizooangoza utafiti huu, nazo ni Uchanganuzi

Hakiki wa Usemi na nadharia ya Uwezo-Uume. Misingi ya nadharia hizi imefafanuliwa kwa kinagaubaga na jinsi ambavyo nadharia hizi zitatumika kama dira katika utafiti huu.

Sura ya tatu mmejadiliwa mbinu za utafiti na uchanganuzi wa data. Katika sura hii pameelezwa data ya kimsingi ya utafiti huu na jinsi data hii ilipatikana na jinsi ilichanganuliwa katika kukidhi malengo ya utafiti huu. Katika sura ya nne pamejadiliwa historia ya usuli wa jamii ya Abakuria kwa mtazamo wa fasihi simulizi; pameelezwa uzao wao, na uhamaji wao hadi pale wanapoishi hivi leo. Vilevile, katika sura hii pameelezwa utamaduni, itikadi, mila na desturi za Abakuria zinazotawala kila awamu ya maisha ya mwanamume kutoka kuzaliwa kwake hadi kifo chake; pamejadiliwa matarajio, mitazamo, na majukumu ya wanaume katika kila awamu; matokeo ni kwamba, utamaduni, mila na desturi za jamii hii zina mchango mkubwa katika kujenga na kukuza uwezo uume. Aidha, katika sura hii mmejadiliwa mifumo ya kijamii, kisiasa, kidini na kiuchumi ya Abakuria na jinsi mwanaume anavyosawiriwa katika mifumo hii. Ni bayana kuwa sura hii ni kiwiliwili cha utafiti, kwani imejadili na kuhakiki utamaduni, mielekeo, matarajio na itikadi za jamii ya Abakuria kama sehemu muhimu zinazojenga na kukuza sura ya mwanaume.

Sura ya tano inashughulikia taswira ya mwanamume katika nyiso za jando. Sura hii imejikita katika uchanganuzi wa nyiso za jando ishirini na nne; kusudi kubwa la uchanganuzi huu ni kudhihirisha picha halisi ya mwanaume inayojikeza katika nyiso hizo na mchango wake katika kujenga na kukuza uwezo uume. Uchambuzi huu umetoa taswira kamili ya mwanamume katika jamii ya Abakuria. Urejeleo wa uchanganuzi huu ni mwanamume katika utangamano na wanajamii wake. Mudhumuni ya utafiti yamezingatiwa katika uchanganuzi huu huku misingi ya nadharia za utafiti ikitumika kama mwongozo wa uchanganuzi.

Tamati ya tasnifu hii ni sura ya sita. Sura hii inabainisha kauli za mwisho za utafiti huu pamoja na kutoa muhtasari wa kila sura ya tasnifu. Aidha ndani ya sura hii pameelezwa matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo kutokana na utafiti huu. Mapendekezo yaliyotolewa yanahusu tafiti za baadaye ambazo huenda zikalenga kwa kina swala la mwanamume, sio tu katika nyiso za jando bali katika tanzu zingine za fasihi ya Abakuria.

6.3 Matokeo ya Utafiti

Mwanamume wa Abakuria katika nyiso za jando amesawiriwa kwa njia mbalimbali. Dhana ya mwanamume huanza kufundishwa, kufafanuliwa na kuhifadhiwa tangu utotoni, kipindi ambacho watoto wanapofunzwa majukumu na matarajio ya jamii kuwahusu (tazama sura ya nne). Wanajamii wanapokua huwa wanafahamu mfumo wa jamii yao. Mfumo huu husheheni kaida za kijamii, mielekeo, mila na majukumu.

Kwa mujibu wa utafiti huu, imebainika bayana kwamba, maksio yote ya awali tuliyoyaorodhesha kama nadharia tete za utafiti tuliolenga kuufanya yamethibitishwa. Tasnifu hii ambayo ndiyo matokeo ya utafiti tulioufanya, imebainisha wazi kwamba;

(i) Nyiso za jando zina mchango katika kujenga na kuhifadhi uume miongoni mwa jamii ya Abakuria.

(ii) Mwanaume katika jamii ya Abakuria husawiriwa kwa njia chanya.

Kutokana na data tuliyoikusanya na kuichanganua, kuna hoja kadhaa ambazo zinajitokeza kuhusiana na usawiri wa mwanaume miongoni mwa jamii ya Abakuria. Kwanza, imebainika kwamba mwanaume wa Abakuria huthaminiwa sana kuliko mwanamke, na thamani hii huhalalishwa na itikadi, imani, mila, matarajio na utamaduni kwa jumla. Mwanaume husawiriwa kama mkimu familia, hivyo basi ni wajibu wa mwanamume kujitolea mhanga katika kutosheleza familia yake mintarafu ya mahitaji ya lazima na mahitaji ya ziada. Aidha mwanaume ni mlinzi wa familia yake na jamii kwa jumla. Ni sharti adhihirishe ushujaa na ushupavu wake katika kuwalinda wanawake, watoto, wakongwe na wanyonge dhidi ya hatari yoyote. Sura hii inadhihirishwa kwa ukweli kwamba nyiso nyingi za jando husisitiza ushujaa, ushupavu na kujitolea kwa mwanaume kama mlinzi wa jamii.

Katika asasi ya ndoa, mwanaume husawiriwa kwa njia mbili, kwanza yeye ndiye humumiliki mwanamke na pili ana haki ya kitamaduni kuwa na wanawake wengi au hata kuwa na uhusiano wa kimapenzi nje ya ndoa.

Majukumu yanayotekelezwa na wanaume katika jamii huthaminiwa zaidi na kutiliwa mkazo. Wanaume husifiwa takribani kwa kila njia; wenye nguvu, watawala, wenye mamlaka,

hodari na wachumaji mali. Kwa mujibu wa imani na utamaduni wa Abakuria, mwanamume hutekeleza majukumu yanayohitaji nguvu nyingi na ya kutoa jasho ilihali mwanamke hutekeleza kazi ndogondogo za nyumbani ambazo hazihitaji nguvu nyingi. Hivyo basi, mchango wa mwanaume katika maisha ya ndoa na ya jamii kwa jumla ni kama jambo ambalo haliwezi kuepukika. Hali hii humtambulisha mwanamume kama binadamu mwenye uwezo na mamlaka.

Sababu za usawiri huu ni za kitamaduni na za kiitikadi. Kutokana na utafiti huu, imedhihirika wazi kwamba utamaduni wa Abakuria humlea mtoto wa kiume na kumkuza akifahamu na kutenda mambo yanayolingana na jinsia yake pamoja na maumbile yake. Anapokuwa mdogo hufunzwa thamani zinazoandamana na jinsia yake na anapokuwa mtu mzima sharti atambulishe umuhimu wake; kwa mfano, awe shujaa na shupavu katika kutetea na kuionea fahari jamii yake. Kwa hivyo, mafunzo hayo anayopewa huambatana na majukumu yake na thamani yake katika jamii siku za usoni.

Matarajio, mitazamo na mielekeo ya jamii huchukua shehemu kubwa katika kuratibu majukumu kiuana na kutathimini thamani ya kila jinsia katika jamii ya Abakuria. Majukumu anayotengewa mwanamume ni yale ya kuhitaji nguvu nyingi na hekima ya hali ya juu, hali hii humfanya mwanamume kuwa na mamlaka makubwa, kiongozi na mwenye uamuzi wa thamani katika jamii. Ikizidi, mwanamume ana wajibu wa kumtunza mwanamke na kumtimizia mahitaji yake yote.

Kwa ujumla, sura anayopewa mwanaume wa Abakuria humkuza, kwani kutokana na utafiti, umuhimu na wajibu wake haukadiriki na thamani yake hujitokeza tangu anapozaliwa hadi kifo chake. Aidha, uamilifu wa mwanaume katika jamii ya Abakuria hudhihirika kupitia uwezo wake wa sheria, siasa, utawala, uchumi na mamlaka juu ya maamuzi na maafikiano katika jamii. Kwa hivyo kuwepo kwa mwanamume katika familia au jamii ni ithibati ya kuendelea kwa jamii kiuzazi.

6.4 Hitimisho

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, usawiri wa mwanamke katika nyiso za jando miongoni mwa Abakuria ni zao la mielekeo, imani, itikadi, matarajio na mitazamo ya jamii. Taswira hizi zinadhirihisha sifa za kimsingi anazostahili kuzihodhi mwanaume katika jamii hii ili aweze kujenga na kuhifadhi utambulisho wake kama mwanamume. Ni sharti mwanamume siku zote kuepuka sifa za kike; mfano:uwoga, unyenyekevu, ukarimu, uaminifu na kulia. Sura hizi zimejengwa na mielekeo, itikadi na jumla ya utamaduni wa Abakuria katika muktadha halisi. Kwa hivyo ni ithibati ya hali halisi katika maisha ya Abakuria.

6.5 Mapendekezo

Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa mwanamume Mkuria, ndiye anayewekewa mzigo zaidi mintarafu ya majukumu yasiyo na idadi katika jamii. Kutokana na dai hili, tunapendekeza kuwa, kuna uhitaji wa tafiti za baadaye kuangaza zaidi nafasi ya mwanamke katika jamii ya Abakuria. Suala hili linaweza kutafitiwa katika utanzu wowote wa fasihi.

Kama tulivyodokeza katika sura ya kwanza, malengo ya utafiti huu yalikuwa, kutathmini mchango wa nyiso za jando katika kujenga na kukuza uume na vilevile kudhihirisha utambulisho wa jinsi mwanamume anavyosawiriwa katika jamii ya Abakuria. Katika utafiti huu, imedhihirika bayana kuwa nyiso za jando ni kiambajengo na ithibati ya mielekeo, matarajio, itikadi, imani na amali za jamii ya Abakuria kuhusu mwanamume; aidha, ni zao la jadi na tajriba ya jamii. Hivyo basi ni rai ya utafiti huu kufanyike utafiti zaidi katika tanzu mbalimbali za fasihi simulizi za jamii hii ili kujaribu kuambatanisha uamilifu wake na mabadiliko ya kilimwengu na ya kiwakati. Hii ni kwa sababu jamii hii imebadilika si haba. Mabadiliko haya ni zao la mifumo ya elimu na dini za kimagharibi; yote haya, kwa pamoja, yameathiri kwa njia moja au nyingine takribani mifumo yote ya kijamii. Aidha, tunapendekeza utafiti wenye kulenga wanajamii wengine wa Afrika kwa lengo la kuonyesha umuhimu wa itikadi, imani, mielekeo na utamaduni na jinsi yote haya huchangia katika kukuza mtazamo wa kilimwengu wa wanajamii wa Kiafrika juu ya sura ya mwanamume. Utafiti wa aina hii utakuwa mchango mkubwa katika kuielewa dhana nzima ya uwezo-uume.

Vilevile, tunapendekeza utafiti ufanywe wa kuchunguza jamii mbambali, jadi na asasi zake, ili kubainisha jinsi zinavyoweza kurekebishwa ili kuleta usawa wa kijinsia barani Afrika.

Mwisho ni matumaini yetu kwamba kazi hii itakuwa kichocheo kwa wasomi hasa wale wanaoazimia kutafiti fasihi simulizi na mchango wake katika kujenga uwezo-uume au hata kuihusisha na mabadiliko ya kijamii na kiwakati kwa minajili ya kuleta usawa wa kinjisia.

MAREJELEO

Vitabu

Abuso, P.A. (1980) **A Traditional History of Abakuria**. AD 1400-1914. Nairobi, Kenya Literature Bureau,.

Akivaga, K. na Odanga, A. (1982) **Oral Literature', A School Certificate**. Nairobi, Heinemann.

Svensson, A. B. (1994) **Kuria proverbs.** Nairobi Executive Printing Works Ltd.

Brown and Yule. (1983) **Discourse Analysis**. New York, Cambridge University Press.

Buchanan, I. and Claire, C. (eds) (2000) **Deleuze and Feminist Theory**. Edinburgh University Press.

Bukenya, A. na Nandwa, J. (1983) **Africa Oral Literature for Schools**. Nairobi, Longman.

Butter, J. (1990) **Gender Trouble, Feminism and the Subversion of Identity**. New York, Routledge.

Chimerah, R. and Njogu, K. (1999) **Ufundishaji wa Fasihi. Nadhanzi na Mbinu**. Nairobi, Jomo Kenyatta Foundation.

Clatterbaugh, K. (1990) **Contemporary Perspectives on Masculinity: Men, Women and Politics in Modern Society**. Westview, Boulder Co.

Collinge, N. E. (1990) **An Encyclopaedia of Language**. New York, Routledge.

Connel, R. W. (1998) **Men, Masculinities and Poverty in U.K.** Oxford, Oxfam GB.

Connel, R.W. (1995) **Masculinities**. Berkley, University of California Press.

Cornwall, A. and Lindisfarne, N. (1994) **Dislocating Masculinity: Comparative Ethnographies.** London, Routledge.

Coulthard, M. (1977) **An Introduction to Discourse Analysis**. New York, Longman Inc.

Crystal, D. (1987) **The Cambridge Encyclopedia of Language**. New York, Cambridge University Press.

Deacon, D., M. Pickering et al. (1999) **Researching Communications**. London, Arnold.

Diop, C. A. (1990) **Cultural Unity of Black Africa: The Domains of Patriarchy and Matriarchy in Classical Antiquity**: Chicago. Third World Press.

Diop, C. A. (1991) **Civilization or Barbarism,** New York, Lawrence Hill.

Fairclough, N. (1991) **Language in the News: Discourse and Ideology in British Press**. London, Routedge.

Fairclough, N. (1989) **Language and Power**. London, Longman.

Finnegan, R. (1970) **Oral Literature in African**. London, Oxford University Press.

Fowler, R. (1991) **Language in the News: Discourse and Ideology in British Press**. London, Routedge.

Frosh, S., Phoenix, A. and Patman, B. (2004) **Young Masculinities: Understanding Boys In Contemporary Society**. New York, Palgarave.

Heald, S. (Mh) (1997) **Praise Poems of the Kuria**. Nairobi, Phoenix Publishers Ltd.

Kimell, M. (1997). **Masculinity as homophobia: Fear, Shame and Silence', in Harry Brod and Michael Kaufman, Theorizing Masculinities**. Thousand Oaks, Sage.

Kimmel, M. (2000) **The Genderd Society**. New York, Oxford University Press.

Kress, G. (1985) **Linguistic Process in Socio-Cultural Practice**. Victoria, Deakin University Press.

Kuper, A. (1982) **Wives for Cattle: Bridewealth and Marriage in Southern Africa**. London, Rutledge and Kegan Paul.

Mackinnon, (1987) **In Men, Masculinity and Femenistry Theory**. Cambridge, Cambridge University Press.

Maclenness, J. (1998) **The End of Masculinity**. Backingham, Open University Press.

Richmond, A. M. (1992) **Masculine and Feminine: Gender Roles over the life cycle**. New York, McGraw-hill, Inc.

Max, W. (1910) **Die Volkerstamme in Norden Deutsch Ostafrikas**. Berlin

Mazrui, A. (1990) **Kilio Cha Haki**. Nairobi, Longhorn.

Mazrui, A. M. na Syambo, B.K. (1992) **Uchambuzi wa Fasihi**. Nairobi, East African Educational Publishers.

Morgan, D.H.G. (1992) **Discovering Men**. London, Routledge.

Mwaniki, H.S.K. (1986) **Categories and Substance of Embu Traditional Songs and Dances.** Nairobi, Kenya Literature Bureau.

Ochieng, W.R. (1974) **An Outline History of Nyanza upto 1914**. Nairobi, East African Literature Bureau.

Ochieng, W.R. (1975) **A Pre-colonial History of the Gusii of Western Kenya, A.D. 1500 to 1914.** Nairobi, East African Literature Bureau.

Otube, K.M. *et al*, (1982) **The Abakuria: The Art of Music and Dance**: Nairobi, KAERA.

Ruel, M.J. (1973) **The Problem of Cultural Origins: The Kuria Case**. University of Nairobi, Institute of African Studies, Mimeo.

Ruel, M.J. (1975) **Securing Growth. The Ritual System of An East African People**. Cambridge University, Clare College, Mimeo.

Sankan, S.S. (1971) **The Maasai**. Nairobi, Kenya Literature Bureau.

Schiffrin, D. (1994) **Approaches to Discourse**. Oxford, Blackwell Publishers Ltd.

Sengo, T.S.Y (1987) **Fasihi Simuli: Sekondari na Vyuo.** Dar es Salaam, Nyanza Publications Agency.

Senkoro, P. (1982) **Fasihi.** Dar es salaam, Press Publicity Center.

T.U.K.I., (2000) **English – Swahili Dictionary 2nd ed.** Mauritius, Book Printing Services Ltd.

Taylor, R (1981) **Understanding the Elements of Literature.** London, Macmillan.

Tobisson, E. (1986) **Family Dynamics Among the Kuria.** Sweden, Akademitryck Edsbruck.

Wallek, A. & Warren, A. (1949) **Theory of Literature.** Penguin Books.

Walsh, M. R. (1997) **Women, Men, and Gender: Ongoing Debates.** London, Yale University Press, New Haven.

Wamitila, K.W (2002) **Uhakiki wa Fasihi: Msingi na Vipengele Vyake.** Nairobi, Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila. K.W. (2003) **Kichocheo cha Fasihi: Andishi na Simulizi.** Nairobi, Focus Books.

Wamitila, K.W. (2003) **Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia**, Nairobi, Focus Publications.

Were, G.S (1967) **A History of the Abaluyia of Western Kenya.** Nairobi, East African Publishing House.

Wodak, R (1996) **Critical Linguistics and Critical Analysis:Handbook of Pragmatics.** Amsterdam, Benjamins.

Wodak, R and Van Dijik, T.A (eds) (2000). **Racism at the Top. Parliamentary Discourses on Ethnic Issues in Six European States.** Klagenfurt, Drava.

Wodak, R. (1999). Introduction in R. Wodak (ed), **Language Power and Ideology.** Amsterdam, Benjamins.

Tasnifu

Chacha, B.K. (1999) "Agricultural History of Abakuria into Modern Kenya, From the End of the Nineteenth Century to the Mid 1970's", M.A. Thesis Egerton University, Njoro. (Haijachapishwa).

Chacha, D. M. (1991) "Kitendawili Cha Vitendawili: Maana na Matumizi katika Jamii ya Wakuria", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Chacha, L. N. (1997) "Majigambo ya Kikuria. Matazamo wa Kiisimu", Tasnifu ya M. A., Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Choti J.N. (1998) "Language and Hierarchy. The Linguistic Portrayal of Gusii Woman", M.A. Thesis, Kenyatta University, Nairobi. (Haijachapishwa).

Imbosa, R. (1990) "Jazanda katika Ushairi wa Muyaka", Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Lugano, R.S. (1989) "Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi", Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Muindi A. (1990) "Usawiri wa Wahusika Makahaba" Katika Vitabu Vya Said Ahmed Mohammed", Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Mwita, B. M. (2005) "Dhima ya Ichingero za Wakuria Kusawiri Taswira ya Mwanamke", Tasnifu ya Ph.D. Chuo Kikuu Cha Moi, Eldoret. (Haijachapishwa).

Okindo, A.O. (1995) "Sura ya Mwanamke Katika Methali za Ekegusii": Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Egerton, Njoro. (Haijachapishwa).

Wandera S.P (1996) "Usawiri wa Mwanamke katika Ushairi wa Kiswahili: 1800-1900 Uhalisia au Ugandamiswaji?", Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Egerton, Njoro.

Makala

De Keijer, B. (2004) "Masculinities Resistance and Change", in Sundy Ruxton (ed). *Gender Equality and Men: Learning from Practice*. U.K., Oxfam G.B (Pg. 29-49).

Cory, H. (1945) "Kuria Law and Custom", Manuscript re-edited by Dobson E.B (1952), The Cory Collection, University of Dar es Salaam.

Hamilton, J.W. (1970) "Problems of Agricultural and Social Development Among the Kuria of Tanzania", Report Based on Fieldwork, September 1968-February 1969: U.S.A.I.D Dar es Salaam, Mimeo.

Hanke, R. (1998) "Theorizing Masculinity with/in the media", Communication Theory 8, (2) 183 – 203.

Holter G. O. (2005) "Social Theories for Researching Men Masculinities. Direct Gender Hierarchy and Structural Inequality": In Kimmel M.S, Hearn J and Connell R.W. (eds). *Handbook of Studies on Men and Masculinities*. New Delhi, Sage Publications. 2, 15-35.

Izugbara, C.O. (2005) "Hypothesis on the Origin of Hegemonic Masculinity", In *Sexuality in African Magazine*. Lagos, Africa Regional Sexuality Resource Centre 2 (1): 13-14.

Kenny, M.G (1977) "The Relation of Oral History to Social Structure in South Nyanza: Kenya", Africa Vol. 47:3.

Kirsten, A.K. and Svensson, A. B. (1988) "Kuria Pictures from 1904", Kenya Archaelogical and Ethnographic Research Agency (KAERA). Gosi Cultural Centre, Kuria.

Matteru, M.L.B. (1982) "The Image of a Woman in Kiswahili Prose Fiction", Kiswahili. Vol. 49/2.

Kitula, K. (2002) "Swala la Uana Katika Fasihi ya Kiswahili: Uhakiki wa Utafiti Kutoka Kenya", katika Inyani, S. K. (Mhariri). *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret, Moi University Press.

Mackinnon, C. A. (1983) "Feminism, Marxism Method and the State: Toward Feminist Jurisprudence". Signs 8 (4) 635-658.

Magayu, K. M. (1977) "East African Literature: An African Writer" Journal of East Africa Literature and Creative Arts.

Michele, A. and Coltrane, S. (2005) "Boys and Men in Families. The Domestic Production of Gender, Power and Privilege" in Kimmel M.S, Hearn J. and Connel. R.W (eds). *Handbook of Studies on Men and Masculinities.* New Delhi, Sage Publications. 14, 230-249.

Ndangam, L.N. (2005) "Masculinity and Male Circumcision in South African Media" Research Proposal to the Codesria. May, 2005 Gender Institute.

Plummer, K. (2005) "Male Sexualities" In Kimmel, S.M, Hearn, J. and Connell R.W (eds) *Handbook of Studies on Men and Masculinities.* New Delhi, Sage Publications. 11, 179-195.

Ratele, K. (2005) "Versions of Masculinity", *In Sexuality in Africa Magazine.* Lagos: Africa Regional Sexuality Resource Centre 2 (1): 3-4.

Ruel M.J. (1959) "The Social organization of the Kuria", A Fieldwork Report, Mimeo.

Ruel M.J. (1962) "Kuria Generation Classes", Africa Vol. 32 pp. 14-36.

Ruel, M.J. (1965) "Religion and Society among the Kuria of East Africa': Africa Vol. 35. pp. 295-306.

Russell, L. (2005) "Masculinity and Agression in South Africa", *in sexuality in Africa. Magazine*. Lagos: Africa Regional Sexuality Resource Center 4 (1) 14-15.

Rogers, S. (2004) "What Men Think About Gender Equality" Lessons From Oxfam GB Staff in Delhi and Dhaka. In Sandy Ruxton (ed). *Gender Equality and Men, Learning from Practice*. U.K. Oxfam GB.


Uchendu, E (2005) "Masculinities from Perspectives of Youth" Paper Presented at teh Gender Institute of CODESRIA

Wandera, S.P. (2002). "Utafiti wa Maswala ya Kijinsia katika Kiswahili", Katika Inyani,S. K. *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret, Moi University Press.

Wodak, R., (2001 b) "What CDA ia about – A summary of its History, important Concepts and Developments" in R. Wodak and M. Meyer (eds). *Methods of Critical Discourse Analysis: Introducing Qualititative methods*. London, Thousand Oaks and New Delhi. Sage Publications, 1 – 13.

KIAMBATANISHO A

RAMANI YA WILAYA YA KURIA



Ramani ya Wilaya ya Kuria

KIAMBATANISHO B

BAADHI YA NYISO ZA JANDO ZA ABAKURIA (IBIIKA)

1. Omotwe go umurisia mbonde gore
nigo okogomaha ogomanya
gonga ugwiritango rre gesaka.

Kichwa cha mvulana ambaye
hajatahiriwa ni tofauti,
unapokiona unakitambua ni
mfuno wa kichwa cha paka shume.

2. Taata wanyiboye wang'anake,
wang'ana talili ya abatali,
era ikururucha kuya igoro
ne emesanga gemo gerenyera,
abaiseke bachore bakembere,
basowabo ichintag'ana
chabo kiburuha na kerabu
batetwe bagende bohamate
batakaba ibiraya ibibasibwa
ibitaya mogondo.

Baba mzazi nakumithilisha
na ndege ya watalii ipaaayo
juu kwa kasi, shanga zilizo
ndani yake zikimwagika
wasichana weu wakusanye
wajipambe na kujing'arisha
ili wapate mabwana, wawalipie mahari
na kuolewa nchi za mbali,
ili wasije wakawa malaya na
wakose maana katika jamii.

3. Wang'ana Selina wabarabu
newe akubinyenga ibiriniki
baracha gwiturani
baibole akalisia ngasagane
akarabu iga che kirigoro
reno rre Mangucha.

Nakulinganisha na mzungu
Selina ndiye anajenga kiliniki
wanawake wajigungue watoto
wa kiume na wa kike weupe
kama theluji hii ya Mangucha

4. Baaba wanyiboye wang'anake
wang'ana ekewanda gichingebo
kera gukurusia tabotabo
chabo metimeti nyarubisi
nyamekanda konda.

Mama mzazi nakulinganisha
na kiwanda cha nguo
kinachotengeneza nguo kwa wingi na za
kisasa mfano
"metameti" yenye mikanda mbele na nyuma

5. Roseromogongo tarichoka
mahe amaino gao mona gare
mona gatabaine mona imigwi
mona ugwigicholi.

Dadangu jitokeze nikuone
nione meno yako jinsi yalivyo
yalivyopangana mithili ya
mishale ndani ya podo.

6. Sokoro wabotaata wakunguha
nyora nuni Yesu ngosabere
ngokore chabani akana agake
kano kagukina mona engano yu umuhandi
nkombari amabegi komareko
ne ichimbiri chimo inchinkumahe
hano tugachinyora ntokameha
togore obogari obotagisi
bohete kwimange boramenia
abanto bakwimange batwitani.

Babu wa upande wa baba,
ningekuwa Yesu ningekuombea
ufanywe kijana mdogo
yule anayekua mfano wa
ngano ya mahindi, nikuwekee
mabegi ya fedha begani,
tutakapozipata hizo pesa
tututajirika tununue gari ndogo,
zipite Kwimange
zikimeremeta, watu wa Kwimange
waanzishe
vita kwa ajili ya wivu

7. Gooko wabotaata wakunguha
nyora nuni mongo nkohonchore
ngokore agasule nyamwiriga
wirige kunyancha gategate
omahere wang'wena na wangubo
bore bakwibira komariba

Nyanya wa upande wa baba
umezeeka, nigekuwa mungu
nikugeuza uwe ndege
upae katikati ya ziwa
uwaone mamba na kiboko
jinsi wanavyoogelea ndani ya maji

8. Mokwe wichingo'mbe tarichoka
nkohe umuchonge gone gorameni
gokogera seto na burugo
nanteramoroni.

Shemeji wa ng'ombe toka nje,
nikupe sime yangu
ikimeremeta, uendee vita
vya uvamizi katika himaya
za maadui

9. Abamura bawaito mong'anahe
mong'ana irikombora irikumahe
retema amanyumba amagoroba
gaika gucha hanse.

Vijana wetu wa kiume, ni
mithili ya kombora
la ajabu ambalo limeamgusha
majumba makubwa.

10 Mahera Gitang'a hano ahira
arrema ibikongo biasira ho
ichingo;mbe chawaito nchiraikobe
motakaba kewe ndabageya

Niambie alikoelekea Giting'a
amelima eneo lote la malisho ya mifugo
ngo'mbe wetu watakonda
nawasihi msije makawa kama yeye.

11. Rerro mbaye omosacha ke abande
nikura giringa nendahike
tebete eking'ori kya abamura kera
bakong'ora

Leo nimekuwa mwanaume
kama wengine, ndumo
ijaposikika sehemu za mbali
nitafika nitekeleze wanachotekeleza
wanaume wengine.

12. Taata wanyiboye neke kana
ndaigwa ndakogora torangana
nyora nakonaha unyabere.

Baba mzazi mbona nakusifu
na hauitikii, iwapo nimekukosea
naomba msamaha.

13. Abaiseke bawaito ndabasaba
hano mogosarwa mokoroka
mutige ubiringu nubwihechu
bara ba amakora mbaihechere
bakarwa amang'ondi nichimburi
hamwe na ichimbura

Wasichana wetu nawasihi,
baada ya kutahiriwa na kutoka
unyagoni, muache
matao na mbwembwe, wale
wa vizazi vya awali
walifanya hivyo wakalipiwa
mahari ya mbuzi, kondoo na punda.

14. Wanyoseye wang'anake
wang'ana esahabu yamosege
era tugutuka torameha
togora amagari waito hano
twikari abakungu kuburito
baraya omotera go Tarime
gokombora ichiswi na ichingebo
barente waito guchisoko
tunyora egetati kegosohia
Hamwe na ikinyero

Dadangu nakumithilisha na
dhahabu ya mosege, ndiyo
tunayochimba na kutajirika,
tunanua gari hapa kwetu
tunawasafirisha kina mama kwa
wingi, kwendo soko la Tarime
kukomboa samaki na nguo
wanaleta kwa masoko ya hapa
kwetu, angalau tunapata kipande
cha nguo na kitoweo.

15. Rose rromogongo nagukumia
kigirre ngambe nagukimia
nigo bogokeigo orakigora
heta ngenda kobahiri
niyakobatebia urrusiko
rorra ndegogwa na irikebi
nirwe kuburisia abobe bono
botare na wabo.

Dadangu unastahili sifa,
kwani kila kuchao unanifungulia
lango la zizi letu, ninapita kwenda
kuwaalika jamaa wetu kwa
sherehe ya tohara yangu, siku
ambayo nitachijwa na jisu
nitoke kwa hali hii isiyo na kwao.

15. Baaba wanyiboye wang'anake
wang'ana wangoncho
nyamebari niyo yasiringi'
kubisaka
amabina ga waito

Maama mzazi nakufananisha na
chiriku, ndiye ameimba
nyimbo za kikwetu
vichakani na katika
mito.

16. Kansala wawaito nagukumia
kigire ngambe nagukumia
nigo igukura uchirwa nyuma
agenda witana uringa nacho
uchiringia waito kubienecho
hata mburi otareye

Kansala wetu nakuonea fahari
kwani pindi ngo'mbe wetu
wanapoibwa wewe hufuata
nyayo, unapigana na maadui na
kuwatoa ngo'mbe hao, unarudi nao
peke yako, unawarudishia wenyewe
bila hata kuchukua mbuzi.

17. Mahera maswega hano ahira
andusi uburisia obobe bono
bondekia ntatara kabamura
nkeribwe isamwita

Niambie Maswega alikoelekea
anitoe "uburisia" (anitahiri)
hali hii imenifanya kutengwa
na waliotahiriwa aidha kutosalimiwa
"isamwita" na wasichana .

18. Gooko wabo taata numwikumia
wanga ababirira abanting'uli
abaruga mabere na maguta
na nyama ya boke.

Nyanya wa upande wa baba
ni mstaarabu nakufananisha
na watu wa tabaka la juu
wenye kupika maziwa, mavuta
na nyama ya asali.

19. Abamura bawaito taibohera
mboroki iching'ombe kwireboko
nomosagane amo amokemosi
okobore korora kogechoka
kobora amorobi.

Mashujaa wetu jitayarisheni
kwa vita, niwaonyeshe ngo'mbe
uvukoni, ni msichana ambaye
hajatahiriwa anazo, anatumia mkono
wa kushoto, mkono wa kulia umevunjika,
umekosa tabibu.

20. Abateti bawaito ndabageya
mutige oboteti abohariki
irrimenya rre rero reya igoro
nairoba retaho.

Nawatahadharisha mliooa
muache ndoa ya wake wengi
maisha yameenda juu
na ardhi ni haba.

21. Gono gomogaaka gong'anake?
gong'ana irrirengo regichere
niryo chikorara iching'era
chagira resokwa na ababisa
bangagucha waito

Huu mji wa mzee unalingana
na jabali la Gichere
pale nyati wanapozunguka
pameheshimiwa na maadui
na limekuwa kizuizi cha uvamizi hapa
kwetu.

22. Baaba gento korenteye nichinseru
otomere emekanda na imichibi
osorre omokamona gucha wao
hano akuhika igo agosekere
amogoti omogango na amagiha
arogere chabani abana abake
barra bagukina mona engano
mona iyumuhindi.

Mama mzazi kile nimekuletea ni
shanga, ushone mikanda na
mishipi, ufuatie mkazamwana
kuja kwako, mara atakapofika umpatie
mwiko na maviga,
awapikie watoto wadogo
wanaokua mfano wa ngano
ya mhindi.

23. Taata wanyiboye wanganake?
wang'ana irirengo richinguku
rerra chikwinara ichihuburi
egaini ya waito ekonga ng'ora
erainara amaguku ga Nyandege
nago nagamaha namarage
nego gasamba mona ebara
yo omomera hanse

Baba mzazi nakulinganisha
na jambali mlimani,
linalozungukwa na vifaru,
fahali wetu aungurume polepole
azunguke milima ya nyandege
kwani milima huu wa ajabu ni
mfano wa majabali ya
chumvi ambayo yamemea ardhini.

24. Abamura bawito mong'anake
mong'ana nyamwaga niyo enene
niyo ekondobayi mona insikai
mona iyo omogaka

Vijana wetu wa kiume ni
mithili ya mlima nyamwaga
ndio mkubwa ambao ni
mfano wa kofia teule ya
wazee sawa na mlima wa
"samadi ya ng'ombe"

25. Ikihita getaata neekenene
ngisere abasungu bakuname
barente ichisendi chiekenene
ogore ichigari na ichindege
tohagache waito

Lango la zizi la baba ni kubwa
linatosha wazungu wapite
walete fedha kwa wingi
tununue gari na ndege na
tujenge kwetu.

26. Taata wanyiboye
kere nkohaye ne inguba engare
abamura bagote baitanerre

Baba mzazi kile nimekupatia ni
ngao pana, mashujaa watumie
katika vita.

27. Ikihita geatata nkikuname
kegere amaguta na
nyama ya boke

Baada ya kutahiriwa,
nikipita katka lango la zizi la
baba mavuta na nyama ya
asali vitatiririka.

28. Mame amona mwiho
niganana regusika bori gukihita
osekera imihingo

Mjomba wangu mpwa ni mithili
ya mti maalum "iriganana" wa
kufungia lango la zizi la ng'ombe
hatimaye miti mingine "imihingo hufuata

29. Nyamakanga hero taya utune
ogende ubusurusi orente
ibere otetere mokao.

Maskini hohehahe
nenda utafute mali, ufanye
biashara ununue ngombe wawili
ulipe mahari.

30. Ikihita getaata nekenene
kerarenta bairo na bageni
na bako ba ng'ombe

Lango la baba ni kubwa
linaleta shemeji na wageni
na shemeji wa ng'ombe

31. Tiga ngore baaba umwene ibisa
newe biare gwita komagiha
araikara araibonda mona obota
bokogera seto na burugo
nantera moroni.

Namsifu mama aliyenizaa
ndiye aliyehisi uchungu wa
uzazi, uchungu ukamfanya kujikunja mithili
ya upinde karibu na maviga, kama
upinde wa kwendea vita na
uporaji wa ng'ombe katika nchi za maadui.

32. Kere ngosooka na abamura
nebo bagitere rogakong'a
nkanyora rroika kurwa igoro
rroracha waito kubihita
hara tokoraria ichintang'ana
hamwe na ichimori

Ninachoheshimu ni mashujaa
ndio walioziba ua imara
ambao ulikuwa umeanguka
na kuacha mwanya katika
zizi letu, wanapolala ng'ombe
wetu.

33. Abamura bawaito monga nkoba
mete mogosara na binyege
na nkomo cha biara

Vijana wetu wa kiume ni mithili
ya radi, hupasua mapandikizi ya
miti kwa mikono na makucha
ya vidole.

34. Abakare bawaito ibohera
tui guchisora Rongararo
hara chikorara icha ababisa
chabo kiburuha na nyamahara
chaibora matena amatebega
chitore Bwirege kobamura
chiche kobakinia abake bano

Mashujaa wetu jitayarisheni
twende kuwafuata ng'ombe Rongararo,
pale wanapolala ng'ombe wa maadui,
hudhurungi na wenye mabaku,
wanaozaa ng'ombe mahuluti na
wanene, waje hapa Bwirege kwa
mashujaa, wawakuze watoto wetu
wachanga.

35. Baaba wanyiboye ikara ogome
nkagena waiboye akahiku
agasachasacha

Mamangu kaa utulie
ulikazaa kajiwe ambako
kamekomaa, mwanamume kamili
na imara

36. Taata waya orantoka iga amatobore
nauni ndagotebia iga ningitire
mona oboori boo ubuya bono.

Baba umekuwa ukinilinganisha na
kuni, nami nakwambia mimi ni
ua imara kama hili zizi lako
zuri.

37. Taata wanyiboye noramehe
kigire ngotebi noramehe
nontoma kubiaro nindahike
ndete nyagatoke na ikoroso
totokere boori gategate
chitagacha kwibwa chihete ho
boke tohanene kuya moyo
tui turakura ichikurate
mona monto akwa

Baba mzazi utatajirika
kwani ujapo nituma himaya
za mbali nitafika,
nilete talasimu tuifukie zizini
katikati,
tuzuie ng'ombe wetu wasije
wakaibwa, asubuhi yake
tufuate nyayo kwenda mbali
huku tukipiga mayowe, kana
kwamba tumefikwa na msiba.

38. Abairege baito tegerra
montoma kurioba nendahike
niyi ntache umweri nookogoro
na akarato kane karameni
ndete mahene gokebara
keno ke bwirege

Wairege wetu nisikilize
hata mkinituma angani nitafika
nikanyage mbalamwezi kwa mguu
huku kiatu changu kikimetameta
nilete ukweli ulimwenguni
hasa hapa kwetu bwirege

39. Abamura bawaito bang'anake?
bang'ana agakendo akangotera
kamera romara gategate
kararenda wandwi na wangubo
na ibikurang'ati

Vijana wetu wa kiume ni mfano
wa mchikichi (mtende) ambao
umemea mto mara katikati
ukilinda simba, kiboko na mbweha.

40. Taata wanyiboye wang'anake?
wang'ana oroseng'enge rro kiribo
mokare ataroke akoroheta agusima mbarera

Baba mzazi nakulinganisha na
Ua uliojengwa kwa seng'enge
Ya siku hizi, usioweza
Kuvukwa na shujaa yeyote yule

41. Abairege baito ndabatakia
abaikwabe barwera komaguku
baambaye ibibeti komareko
bagora ichawaito ncharu
totagaitwa na ubwiro

Wairege wetu nawatahadharisha
wamasai wametokezea milimani
huku wametundika mikoba ya
pesa begani, wamenunua ng'ombe
wetu wengi, tusije tukaangamia
kwa unyafuzi

42. Abamura bawaito muyi ng'ora
ichitinyi chaya aharrai
abagemu mbabaita na ichikong'u
mutige abasino kunyanyi

Mashujaa wetu mwende pole,
wanyama wa pori wameenda mbali,
walinzi watawaua kwa
silaha kali, muwaache
wajane kwa shida.

43. Taata wanyiboye wang'anake?
wang'ana irrirongwe rrya abasubi
rera rekogamba baikomana
amasubi amang'aini gacha hamwe

Baba nakulinganisha na baragumu
maalum ya wazee
wa kimila (jadi), inayotumika
kuwakusanya, wazee
wenye hekima kuja pamoja

44. Gikuburi waito giche ng'ora
giche keraburia ko-bamura
abangiri bawabo

Anayepanga uvamizi kwetu
aje polepole, aulizie kwanza
huku akijua kuwa ni kwa
mashujaa, watetezi wa kwao

45. Rerro nchongewe ikaramu
eno itagusira wino

Leo nimechongewa kalamu
isiyoisha wino

46. Rerro ntiriribwe umuhio
ogogwitaniria ababisa

Leo nimenolewa upanga
wa kupigana na maadui

47. Naya ndaboronga mona eng'era
rrero nkuhusiande ki'omokama
gono go Muyuyi

Nimekuwa nikiunguruma
kama nyati, lakini kwa sasa
ninavuma kama tufani
itokeayo Muyuyi

48. Taata wanyiboye wang'anake?
wang'ana retinde nyamegogo
rekorara ichindwe na inchinsabi
na ichinguruneti

Baba mzazi nakulinganisha na
chaka la retinde, lenye
mapandikizi ya mti,
wanamoishi simba na majoka
hatari pamoja na wanyama
wengine wakubwa wa kuogofya.

49. Abakare bawaito mong'anake?
mong'ara akabwaro kagesaka
kara kagusika amaroboko
gara gibing'eng'i

Mashujaa wetu ni mithili ya kifaru
azibaye vivuko vya mto
vya kuelekea kwenye majabali
ya chumvi

50. Sokoro waito no omonene
wang'ana Romara niyo enene
niyo itakahoye ekogatoka
chikunywa agasense

Babu wetu ni mkuu,
ni mithili ya mto Mara
ndio mkubwa, haujawahi kukauka
hadi mifugo wanywe mchanga

51. Abamura bawaito nigamero
nebo twigameye imbura indito
eno yo omohoika

Vijana wetu wa kiume ni
mwavuli, kwao tumejikinga
mvua nzito hii ya masika

52. Gono go omogaaka ngwitachere
mona irrinyasaka rre kiribo
nyamuri motambe

Mji huu wa mzee ni mithili
ya uyoga wa jangwani
wenye mzizi mrefu

53. Taata wanyiboye nkemenio
moreka tomahe tui guchisora
Rongararo, hara chikorara
icha ababisa
chabo kiburuha na nyamahara,
chaibora amatena amatebega
chitore bwirege kobamura
chiche kobakinia abake bano

Baba mzazi wewe ni kimulimuli cha radi
mulika tuvuke, twende kuwafuata
ng'ombe Rongararo, pale walalapo
ng'ombe wa maadui
hudhurungi na wenye mabaku
wanaozaa mahuluti na wanene
waje bwirege kwa mashujaa
ili wawakuze watoto wetu wachanga

54. Taata wanyiboye wang'ana ng'we?
Monto kereng'aine Ndosogiro
Omonto Omatariro Omukumahe
nyabihita binane

Baba mzazi nakulinganisha na Rosogiro
mkabe wa mlango wa Motatiro
(mlango wa jamii ya Wamasai)
mwenye boma manane

55. Taata wanyiboye wang'ana ng'we?
wang'ana Omotatiro Omorraiboni
Omome wa iching'ombe na ichimburi
hamwe na amang'ondi

Baba mzazi nakulinganisha na
Motatiro, kiongozi wa jamii ya
Wamasai (Laiboni), tajiri wa
ng'ombe, mbuzi na kondoo

56. Wanyora borina bogachoka
bohika korototi
rerro mbotegeye abana abake
bara bagukina kuya igoro

Aibu ya kuwa "Murisia" (ambaye
hajatahiriwa) ilikuwa imefika
utosini, lakini tangu sasa
nimewaachia watoto wadogo
wanaokua.

57. Taata wanyiboye wang'ana ng'we?
wang'ana Gesogiro Omukumo otarito
wae itakaheye ekoba iberi

Baba mzazi nakulinganisha na Gesogiro
tajiri wa
ukoo wa Tatiro ambaye
kwake hakujawahi kuchomeka
na kuwa jangwa

58. Abamura bawaito na abakare
bang'ana Umwitaliano umukumahe
newe agichenga iya kirumi
amagari gagacha gakamboka
Gakagera Mwanza na Totoma
hara haikareywe imigutano
geno ge ikimira igikumahe
kera bakorengi kurwa karre
kurwa nyamburiti komakora

Vijana wetu wa kiume ni mashujaa
ni mithili ya mzungu Mwitaliano
aliyejenga daraja la kirumi
magari yakaja yakavuka
kuelekea Mwanza na Dodoma
panapofanyiwa mikutano maarufu
ya wazee wenye hekima
tangu zama za kale, enzi ya
kizazi cha wanyamburiti

59. Taata wanyiboye no omonene
kere koreng'aine ne Isengere
omona wa umukira gokorasa
arasa nyamongo kobakari
arasa ngurueme kobakari
arasa bwirege kobamura
kobasachasacha
hano nkamogota gokoboko
nkamotema ikinyimbo kibigoti
haru magogo na umuchonge gone

Babangu mzazi ni mkuu
nakufananisha na isengere
shujaa wa mlango wa bukiira
kwa shabaha, amefaulu
kushambulia Nyamongo na
ngurueme kwa wanawake
amejaribu bwirege kwa wanaume
kamili, nikimshika kwa mkono,
nimpige fimbo ya shingo, kisha
nimchinje kwa sime yangu.

60. Taata wanyiboye wang'ana ng'we?
wang'ana Girari omerenchoka
wabo itakaheye ekoba iberi
ekomera amanyansi

Baba mzazi nakulinganisha
na Girari wa ukoo wa
warenchoka, mji wao
haujawahi kuteketea
na kuwa chaka.

KIAMBATANISHO C

ORODHA YA WAHOJIWA

Moronya O'Gituni, umri miaka 90

Mkaazi wa Gitungi, anafanya kazi ya ukulima na ufugaji

Matiko O' Mariko, umri miaka 78

Mkaazi wa Nyantira, anafanya kazi ya ukulima

Mutundi Wairoga, umri miaka 58

Mkaazi wa Kangariani, anafanya kazi ya ukulima na ufugaji

Moffat Masambe, umri miaka 70.

Mkaazi wa Bungurere, anafanya kazi ya ufugaji na ukulima

Mwita Kirutu, umri miaka 35.

Mkaazi wa Bungurere, anafanya kazi ya ualimu na ukulima

Julius Juma, umri miaka 28.

Mkaazi wa Gwitembe, anafanya kazi ya ualimu

Nchangwa O'gimunta, umri miaka 88.

Mkaazi wa Makararangwe, anafanya kazi ya ukulima

Marwa Ramadhan, umri miaka 18.

Mwanafunzi wa shule ya upili

Mohagachi Wilfred, umri miaka 15.

Mwanafunzi wa shule ya upili

Makubo Stephen Marwa, umri miaka 16.

Mwanafunzi wa shule ya upili

Andrew Giriago, umri miaka 16.

Mwanafunzi wa shule ya upili

Kohe Meshak, umri miaka 16.

Mwanafunzi wa shule ya upili

Magoge Lamech Nyamosi, umri miaka 16.

Mwanafunzi wa shule ya upili

Chacha Daniel, umri miaka 14.

Mwanafunzi wa shule ya upili

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY